# UCHANGANUZI KIMOFOSEMANTIKI WA ANTHROPONIMU ZA KIMARAGOLI ZINAZOJENGWA NA NOMINO ZA KAWAIDA ZA KISWAHILI

**NA**

**ODARI MORRIS SALANO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA MINAJILI YA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**SKULI YA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII**

**CHUO KIKUU CHA MASENO**

**© 2024**

## IKIRARI

Nakiri kuwa, tasnifu hii ni zao la utafiti wangu mwenyewe asilia na haijawasilishwa Chuoni humu wala katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote. Ni makosa na hatia kutolesha nakala au sehemu ya Tasnifu hii bila ya idhini yangu na/au ya Chuo Kikuu cha Maseno.

(**Mtahiniwa**)

**Odari Morris Salano**

MA/FA/00037/017

Saini: …………………..……… Tarehe: ………………….

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa na idhini yangu kama msimamizi /mshauri niliyeteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Maseno wa mzamili

**Prof. Florence Indede**

Idara ya Kiswahili & Lugha nyingine za Kiafrika

Skuli ya Sanaa na Sayansi za jamii

Chuo Kikuu cha Maseno.

Saini: …………………..……… Tarehe: ………………….

**Dkt. Benard Odoyo Okal**

Idara ya Kiswahili & Lugha nyingine za Kiafrika

Skuli ya Sanaa na Sayansi za jamii

Chuo Kikuu cha Maseno.

Saini: …………………..……… Tarehe: ………………….

**SHUKRANI**

Ama kwa hakika masuala ya kiakademia hayakamilishwi ‘vivi hivi tu’ pasi na usaidizi wa hapa na pale. Siwezi kujigamba na kudai kuwa jitihada zangu pekee zingeniwezesha kufua dafu pasi na mchango wa watu wengine wengi ambao naona fahari kubwa kuwataja majina, ingawa siwezi kuwataja wote. Kwanza kabisa, natoa shukrani zisizo na ukomo kwa Mwenyezi Mungu aliyeumba dunia na vyote vilivyomo. Yeye ndiye alikuwa nahodha mkuu wa kazi hii hadi kutua nanga salama ufukoni mwa bahari tesi. Ninamshukuru kwa kunitunuku fursa hii adimu kuendeleza masomo yangu kisha kunijalia afya, kibali, neema na baraka lukuki. Nasema kwa unyenyekevu, shukrani Mungu, wewe ni mwaminifu.

Pili, ninawashukuru sana wazazi wangu Bw. Ezara Salano na Bi. Agreta Salano. Shukrani sana kwa kuniombea kila wakati na kunihimiza kutegemea Mwenyezi Mungu. Kakangu Evance Avugwi, kwa hisani yako. Umejinyima mengi maishani ili nipate elimu. Shukrani kunipa nafasi hii ya kipekee ambayo wengi wameikosa, kwa hakika pasi na juhudi zako nisingefika viwango vya juu vya usomi.

Tatu, kwa heshima kuu na taadhima, naomba kutoa shukrani chekwachekwa kwa wasimamizi wangu; Prof. Florence Indede na Dkt. Benard Okal. Nawashukuru sana kwa kutumia unajimu wenu, kwa uvumilivu mkubwa mkajitolea kwa moyo mkunjufu tangia hatua ya kuandaa pendekezo la utafiti, ukusanya data, uchanganuzi wa data na uandishi wa tasnifu hii; pamoja na kunipa ushauri wa busara. Ufanisi wa tasnifu hii ni matokeo ya jitihada zenu kubwa. Nilipowauliza swali, kutoka kwenu nilipata zaidi ya majibu. Niliponyong’onyea, mlinitia moyo. Nilipolaza damu, mlinikumbusha manufaa ya kuikamilisha kazi hii kwa wakati. Nilipokanyaga chechele upesi mlinirejesha kwa njia. Wakati wote nilipowapokeza faslu za utafiti huu mlizipokea, mkazisoma kwa wakati hatimaye, mkanielekeza ipasavyo licha ya kuwa na majukumu mengi ya kitaaluma na kifamilia. Kwa hakika mmeninoa vilivyo. Sina maneno ya kukifu ya kutoa shukrani kwenu, nawaombeeni kutoka kwa Mwenyezi Mungu afya tele na maisha marefu. Daima nitaishi kuukumbuka wema wenu.

Ninawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika kwa ushauri wenu na maelekezo yenu kwangu wakati wa masomo yangu katika Chuo Kikuu cha Maseno tangu digrii ya kwanza hadi sasa, ninawathamini sana. Mmenitia ukakamavu maishani

na kuathiri mwonoulimwengu wangu wa maisha kwa njia chanya mbali na kunitia uchu wa kuipenda lugha hii ashirafu, Kiswahili. Shukrani jazila kwenu Dkt. Amukowa, Dkt. Lumwamu, Dkt. McOnyango, Dkt. Asiko, Dkt. Mulwale, Bw. Muga na Bw. Kiptanui, kwa kunipa msingi imara wakati wa shahada ya kwanza na pia kunifunza vizuri Uzamili, Mungu awape mbawazi njema.

Aidha, ninashukuru sana mradi wa *Kenya Languages Corpus (KenCorpus Project)* chini ya mtafiti mkuu Dkt. Lilian Wanzare na mradi wa *Princeton in Kenya/Kenya Global Seminar* uliosimamiwa na Dkt. Mahiri Mwita. Miradi hii ilinipa tajriba ya kipekee katika ukusanyaji data, uchanganuzi, tafsiri na marupurupu ambayo yaliniwezesha kukamilisha karo yangu ya Uzamili mbali na kujifunza mambo mengi katika lugha za Kiafrika, hususan Kiswahili na Kimaragoli. Ninashukuru Baraza la Wazee la Wamaragoli kwa kunipa data niliyoihitaji na kunifunza mambo mengi yanayohusiana na jamii hii. Kwa wengine wote mlionifaa katika utafiti huu shukurani sana hata kama sijawataja kwa majina, Mwenyezi Mungu awabariki.

## TABARUKU

Kwa

Mungu mwenye uweza, muumbaji wa milele, mwenye nguvu zote. Alfa na Omega, sifa na utukufu ni zako! Neno lako ni kweli! Yeremia, 32:27: Mimi ndimi BWANA, Mungu wa wote wenye mwili. Je, kuna jambo lolote lililo gumu nisiloliweza? Mwenyezi Mungu, kazi hii ni dhihirisho hakuna! Uliianza kazi hii njema, ukaiendeleza na sasa umeikamilisha kwa wakati wako. Jina lako lihimidiwe daima!

## IKISIRI

Maana za maneno zinaweza kubadilika kulingana na muktadha wa ufasiri, hali inayoweza kutinga uwasilishaji wa maana ikusudiwayo. Mabadiliko ya kimaana kama haya yanadhihirika pia katika uchunguzi wa anthroponimu za Kimaragoli. Ingawa tafiti zimefanywa kuhusu maana kileksika za anthroponimu za Kimaragoli, vyanzo vya anthroponimu hizo kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili, mbinu za kimofolojia zinazounda anthroponimu hizo, pamoja na mabadiliko yake kimaana hazijashughulikiwa. Kutokana na msingi huu, utafiti huu ulichanganua kimofosemantiki anthroponimu za Kimaragoli zilizoundwa kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo: kuainisha nomino za kawaida za Kiswahili zijengazo anthroponimu za Kimaragoli katika vikoa maana; kufafanua mabadiliko ya kisemantiki katika anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo kwa nomino za kawaida za Kiswahili; na kuchanganua mbinu za kimofolojia za uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo kwa nomino za kawaida za Kiswahili. Uchunguzi huu uliongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksia iliyoasisiwa na Blutner (1990). Nadharia hii huchunguza maana ya leksimu kipragmatiki. Kwa kuzingatia muundo wa kimaelezo, utafiti ulifanyika maktabani na nyanjani katika gatuzi Dogo la Sabatia, kaunti ya Vihiga. Usampulishaji dhamirifu ulitumiwa kuteua nomino za kawaida za Kiswahili, watafitiwa, hospitali pamoja na eneo la utafiti. Data ya anthroponimu za Kimaragoli ilikusanywa kutoka kwa baraza la wazee la Wamaragoli pamoja na sajili za majina katika hospitali teule. Data ya utafiti ilikusanywa kwa kutumia mbinu za upekuzi maktabani na usaili usorasmi, na vifaa vya utafiti vilijumuisha orodhahakiki na mwongozo wa usaili. Uhalali, ukubalifu na utegemezi wa data ulithibitishwa na wataalamu wa lugha na jamii ya Wamaragoli. Maadili ya utafiti yalizingatiwa kabla, wakati na baada ya utafiti kwa mujibu wa matakwa ya kibali cha utafiti kutoka MUERC na NACOSTI. Data ilichanganuliwa kimaudhui na kuwasilishwa kimaelezo na katika majedwali. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa nomino za kawaida za Kiswahili zinaweza kuainishwa katika vikoa maana vya wanyama, ndege, vifaa, na mimea. Mabadiliko ya kimaana katika anthroponimu za Kimaragoli zilizojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili hujumuisha upanuzi, kisio na ubanaji wa maana. Aidha, anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili huzingatia mbinu za kimofolojia kama vile ukopaji, uhusishaji, uradidi, mwambatanisho na uhulutishaji. Utafiti ulipendekeza tafiti zaidi zifanywe kuhusu mchango wa aina nyingine za nomino pamoja na kategoria zingine za maneno katika ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli na lugha nyinginezo. Matokeo ya utafiti huu yanachangia mijadala ya dhima ya Kiswahili katika kuendeleza misamiati ya lugha nyingine za kiasili, maarifa ya semantiki, mofolojia na onomastiki. Aidha, utafiti huu ni kanzi inayoelimisha kuhusu anthroponimu za Kimaragoli, mabadiliko ya kimaana katika anthroponimu hizo na pia mbinu za kimofolojia zinazozijenga kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili.

## ABSTRACT

Meanings of words can change depending on the context of interpretation, a situation that can interfere with the communication of the intended meaning. Such changes in meaning are also evident in the study of Maragoli anthroponyms. Although studies have been done on the lexical meanings of the Maragoli anthroponyms, their sources from common Kiswahili nouns, their semantic changes, as well as the morphological strategies that are used in deriving them have not been addressed. In this regard, the study analysed morphosemantically Maragoli anthroponyms that are derived from the common Kiswahili nouns. The study was guided by the following objectives: to classify Kiswahili common nouns that form Maragoli anthroponyms into semantic fields; to describe semantic changes in Maragoli anthroponyms that are derived from Kiswahili common nouns; and to analyse the morphological strategies employed in the derivation of Maragoli anthroponyms from Kiswahili common nouns. The study was guided by the Lexical Pragmatics theory propounded by Blutner (1990). The theory pragmatically examines lexical meaning. Based on the descriptive design, the research was conducted in the library and in the field in Sabatia Sub-County, Vihiga County. Purposive sampling was used to select Kiswahili common nouns, respondents, hospitals and also the study area. Data on Maragoli anthroponyms was collected from the council of Maragoli elders as well as names in the registers from selected hospitals. Data collection methods involved observation in the library and informal interviews. The research instruments included checklists and an interview guide. The validity, acceptability and reliability of data were verified by experts on Maragoli language and community. Research ethics were considered before, during and after the study in accordance with the requirements of the research permit issued by MUERC and NACOSTI. Data was thematically analysed, and descriptively presented and in a tabular form. The research findings showed that Kiswahili common nouns can be classified into semantic fields of animals, birds, equipment, and plants. Semantic changes in Maragoli anthroponyms derived from Kiswahili common nouns include broadening, approximation and lexical narrowing,. In addition, Maragoli anthroponyms derived from Kiswahili common nouns rely on morphological strategies such as borrowing, conversion, inflection, reduplication, compounding and blending. The study suggested that further research needs to be conducted on the contribution of other types of nouns and other parts of speech on the derivation of Maragoli anthroponyms and other languages. The study outcome contributes to the discourses on Kiswahili language and development of vocabularies of other indigenous languages, knowledge on semantics, morphology and onomastics. In addition, the findings of this study are a repository that educates about Maragoli anthroponyms, especially the semantic changes in those anthroponyms, and also morphological strategies used in their derivations from Kiswahili common nouns.

## YALIYOMO

IKIRARI ... ii
SHUKRANI ... iii
TABARUKU ... v
IKISIRI ... vi
ABSTRACT ... vii
YALIYOMO ... viii
VIFUPISHO NA AKRONIMU ... xii
FASILI ZA ISTILAHI ... xiii
ORODHA YA MAJEDWALI ... xiv
ORODHA YA VIELELEZO ... xvi
**SURA YA KWANZA: MSINGI WA UTAFITI ... 1**
1.1 Utangulizi ... 1
1.2 Usuli wa Mada ... 1
1.2.1 Dhana ya Anthroponimu ... 4
1.2.2 Jamii ya Wamaragoli ... 5
1.2.3 Tafiti Zinazohusu Kimaragoli ... 7
1.2.4 Suala la Utafiti ... 9
1.3 Madhumuni ya Utafiti ... 10
1.4 Maswali ya Utafiti ... 10
1.5 Upeo wa Utafiti ... 11
1.6 Misingi za Uteuzi wa Mada ... 11
1.7 Umuhimu wa Utafiti ... 12
1.8 Nadharia ya Utafiti ... 14
1.9 Hitimisho ... 17
**SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI ... 18**
2.1 Utangulizi ... 18
2.2 Uainishaji wa Nomino katika Vikoa Maana ... 18
2.3 Mofolojia ya Uundaji wa Anthroponimu ... 24
2.3.1 Mbinu za Kimofolojia za Uundaji wa Anthroponimu ... 27

2.3.1.1 Ukopaji ... 27
2.3.1.2 Mwambatano ... 28
2.3.1.3 Unyambulishaji ... 29
2.3.1.4 Ufupishaji ... 29
2.3.1.4.1 Akronimu ... 29
2.3.1.4.2 Ufupishaji-Mkato ... 30
2.3.1.4.3 Uhulutishaji ... 31
2.3.1.5 Uradidi ... 32
2.3.1.6 Ubunaji ... 33
2.3.1.6.1 Kubuni Kinasibu ... 33
2.3.1.6.2 Uhusishaji ... 33
2.3.1.7 Uhamishaji Maana ... 34
2.4 Mabadiliko ya Kisemantiki katika Maneno ya Lugha ... 35
2.5 Hitimisho ... 41
**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ... 43**
3.1 Utangulizi ... 43
3.2 Muundo wa Utafiti ... 43
3.3 Eneo la Utafiti ... 44
3.4 Idadi Lengwa ... 45
3.5 Usampulishaji na Sampuli ... 46
3.6 Mbinu na Vifaa vya Ukusanyaji Data ... 48
3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji Data ... 48
3.6.1.1 Upekuzi ... 49
3.6.1.2 Usaili ... 49
3.6.2 Vifaa vya Ukusanyaji Data ... 50
3.6.2.1 Orodhahakiki ... 50
3.6.2.2 Kinasa Sauti ... 50
3.6.2.3 Mwongozo wa Usaili ... 51
3.7 Utafiti Awali ... 51
3.8 Utegemevu na Ukubalifu wa Vifaa vya Ukusanyaji Data ... 52
3.9 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ... 53

3.10 Maadili ya Utafiti ........................................................................................................ 54
3.11 Hitimisho........................................................................................................................ 57
**SURA YA NNE: UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA ............................... 58**
4.1 Utangulizi ......................................................................................................................... 58
4.2 Vikoa Maana vya Nomino za Kawaida za Kiswahili ........................................................ 58
4.2.1 Kikoa Maana cha Wanyama ........................................................................................... 59
4.2.1.1 Wanyama Wanaofugwa ................................................................................................ 60
4.2.1.2 Wanyama Mwitu........................................................................................................... 62
4.2.2 Kikoa Maana cha Ndege ................................................................................................. 63
4.2.2.1 Ndege Wafugwao.......................................................................................................... 63
4.2.2.2 Ndege Mwitu ................................................................................................................ 64
4.2.3 Kikoa Maana cha Mimea na Viungo .............................................................................. 66
4.2.4 Kikoa Maana cha Vyakula na Vinywaji ......................................................................... 67
4.2.5 Kikoa Maana cha Vifaa .................................................................................................. 69
4.2.5.1 Vyombo vya Usafiri...................................................................................................... 69
4.2.5.2 Vyombo vya Matumizi Jikoni ....................................................................................... 70
4.2.5.3 Vifaa vya Ujenzi ........................................................................................................... 71
4.2.6 Kikoa Maana cha Elimu.................................................................................................. 72
4.2.7 Kikoa Maana cha Samani ............................................................................................... 73
4.2.8 Kikoa Maana cha Magonjwa .......................................................................................... 74
4.2.9 Kikoa Maana cha Viungo vya Mwili.............................................................................. 75
4.2.10 Kikoa Maana cha Jamii na Utaifa................................................................................. 76
4.2.11 Kikoa Maana cha Mavazi ............................................................................................. 76
4.2.12 Kikoa Maana cha Majira/Wakati .................................................................................. 77
4.2.13 Kikoa Maana cha Silaha ............................................................................................... 78
4.2.14 Kikoa Maana cha Wadudu............................................................................................ 79
4.2.15 Kikoa Maana cha Ukoo ................................................................................................ 79
4.2.16 Kikoa Maana cha Taaluma ........................................................................................... 80
4.2.17 Kikoa Maana cha Sekta ya Kilimo ............................................................................... 81
4.2.18 Kikoa Maana cha Mapambo ......................................................................................... 82
4.2.19 Kikoa Maana cha Sekta ya Uchumi.............................................................................. 82

4.3 Mofolojia ya Uundaji wa Anthroponimu za Kimaragoli ........................................................ 83
4.3.1 Mbinu ya Ukopaji ........................................................................................................ 83
4.3.2 Mbinu ya Uhusishaji ..................................................................................................... 86
4.3.2.1 Sifa za Kimaumbile....................................................................................................... 86
4.3.2.2 Sifa za Kitabia.............................................................................................................. 87
4.3.3 Mbinu ya Uhulutishaji .................................................................................................. 87
4.4 Mabadiliko ya Maana katika Anthroponimu za Kimaragoli ................................................ 89
4.4.1 Ubanaji wa Kileksia...................................................................................................... 90
4.4.2 Upanuzi wa Kileksia..................................................................................................... 92
4.4.2.1 Upanuzi wa Kisitiari .................................................................................................... 93
4.4.2.2 Chuku.......................................................................................................................... 94
4.4.3 Kisio la Maana ............................................................................................................. 95
4.5 Hitimisho....................................................................................................................... 96
**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO............................ 98**
5.1 Utangulizi...................................................................................................................... 98
5.2 Muhtasari wa Tasnifu .................................................................................................... 98
5.3 Mahitimisho .................................................................................................................. 99
5.3.1 Vikoa Maana vya Nomino za Kawaida za Kiswahili ......................................................... 99
5.3.2 Mbinu za Kimofolojia za Uundaji wa Anthroponimu za Kimaragoli .............................. 100
5.3.3 Mabadiliko ya Maana katika Anthroponimu za Kimaragoli ............................................ 100
5.4 Mapendekezo ............................................................................................................... 101
5.4.1 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye .............................................................................. 101
5.4.2 Mapendekezo ya Kisera na Kiutekelezi.......................................................................... 103
**MAREJELEO ................................................................................................................ 104**
**VIAMBATISHO ............................................................................................................ 111**

## VIFUPISHO NA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| **AU** | *African Union* |
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili Tanzania |
| **BAKIZA** | Baraza la Kiswahili Zanzibar |
| **CBC** | *Competence Based Curriculum* |
| **Kiamb.** | Kiambatisho |
| **MUERC** | *Maseno University Ethics Review Committee* |
| **NACOSTI** | *National Commision for Science, Technology and Innovation* |
| **PAG** | *Pentecostal Assemblies of God* |
| **TUKI** | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| **UNESCO** | *United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization* |

## FASILI ZA ISTILAHI

**Anthroponimu:** Majina ya watu.

**Onomastiki:** Taaluma ya kiisimu inayochunguza au kutalii majina ya viumbe na mahali.

**Wamaragoli:** Jamii ya watu waliozaliwa na kukulia katika tamaduni za Mulogooli na wanazungumza lugha ya Kimaragoli.

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Aina za Udondoshaji katika Ufupisho-Mkato ........ 30
Jedwali 4.2: Kikoa Maana cha Mifugo ........ 61
Jedwali 4.3: Kikoa Maana cha Wanyama Mwitu ........ 62
Jedwali 4.4: Kikoa Maana cha Ndege Wafugwao ........ 64
Jedwali 4.5: Kikoa Maana cha Ndege Mwitu ........ 65
Jedwali 4.6: Kikoa Maana cha Mboga na Viungo ........ 67
Jedwali 4.7: Kikoa Maana cha Vyakula na Vinywaji ........ 68
Jedwali 4.8: Kikoa Maana cha Vyombo vya Usafiri ........ 69
Jedwali 4.9: Kikoa Maana cha Vyombo vya Matumizi Jikoni ........ 70
Jedwali 4.10: Kikoa Maana cha Vifaa vya Ujenzi ........ 71
Jedwali 4.11: Kikoa Maana cha Elimu ........ 72
Jedwali 4.12: Kikoa Maana cha Samani ........ 73
Jedwali 4.13: Kikoa Maana cha Magonjwa ........ 74
Jedwali 4.14: Kikoa Maana cha Viungo vya Mwili ........ 75
Jedwali 4.15: Kikoa Maana cha Jamii na Utaifa ........ 76
Jedwali 4.16: Kikoa Maana cha Mavazi ........ 77
Jedwali 4.17: Kikoa Maana cha Majira/Wakati ........ 77
Jedwali 4.18: Kikoa Maana cha Silaha ........ 78
Jedwali 4.19: Kikoa Maana cha Wadudu ........ 79
Jedwali 4.20: Kikoa Maana cha Ukoo ........ 80
Jedwali 4.21: Kikoa Maana cha Taaluma ........ 80
Jedwali 4.22: Kikoa Maana cha Sekta ya Kilimo ........ 81
Jedwali 4.23: Kikoa Maana cha Mapambo ........ 82
Jedwali 4.24: Kikoa Maana cha Sekta ya Uchumi ........ 82
Jedwali 4.25: Ubanaji wa Kileksia ........ 90
Jedwali 4.26: Upanuzi wa Kisitiari ........ 93
Jedwali 4.27: Chuku ........ 95
Jedwali 4.28: Kisio la Maana ........ 96

Jedwali 4.29: Ukopaji wa Kiutohozi ........................................................................ 84
Jedwali 4.30: Ukopaji Sisisi ........................................................................ 85
Jedwali 4.31: Uhusishaji Kimaumbile ........................................................................ 86
Jedwali 4.32: Uhusishaji Kisifa ........................................................................ 87

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 2.1: Uundaji Maneno kwa Mbinu ya Uhulutishaji ........................................................ 31
Kielelezo 4.2: Uundaji wa Anthroponimu *Samoja* kwa Uhulitishaji ........................................... 88
Kielelezo 4.3: Uundaji wa Anthroponimu *Sambili* kwa Uhulitishaji ........................................... 88
Kielelezo 4.4: Uundaji wa Anthroponimu *Satatu* kwa Uhulitishaji ............................................. 89
Kielelezo 4.5: Uundaji wa Anthroponimu *Satano, Sasita na Sakomi* .......................................... 89

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inautanguliza uchunguzi huu kwa kufafanua taratibu zilizozingatiwa. Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na: usuli wa utafiti, suala lichunguzwalo, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi wa mada, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti. Pia, misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti imeelezwa kabla ya kuwasilisha muhtasari wa yaliyomo kama hitimisho la sura.

## 1.2 Usuli wa Mada

Uundaji wa maneno huchanganuliwa katika kiwango cha mofolojia. Mofolojia ni istilahi itumiwayo kuurejelea utanzu wa isimu unaochunguza muundo wa maneno na michakato ya uundaji wa maneno katika lugha (Yarlesis & wenzie, 2009). Taaluma ya mofolojia inaweza kugawika katika matawi mawili makuu, yaani mofolojia ya uundaji wa maneno na mofolojia ya uambishaji wa maneno (Katamba, 1993; Massamba, 2004). Suala la uchanganuzi wa vijenzi vya maneno limewashughulisha wanaisimu kwa muda mrefu huku mofolojia ya uundaji wa maneno katika lugha ikipuuzwa au kukosa kutiliwa maanani zaidi katika tafiti za kiisimu (Yarlesis & wenzie, 2009). Ingawa walitoa kauli hii zamani kidogo bado maoni yao hayajatiliwa maanani, haswa katika taaluma ya onomastiki ambapo kwa mujibu wa uhakiki wa maandishi, utafiti uliochukua mkondo huo ni muhali kupatikana; hali iliyouchochea utafiti huu kutoa mchango wa kitaaluma katika mofolojia ya uundaji wa maneno kwa kuchunguza majina.

Kwa vile takribani lugha zote ulimwenguni ni mifumo hai, hubadilika (Reeve, 2011). Laura (2009) anafafanua kuwa majina ya watu huweza kubadilika kimaana kwa mujibu wa hatua za maisha anazopitia mtu kutoka utotoni hadi utu uzima. Anaendelea kudokeza kuwa zipo tafiti chache kuhusu majina, hasa katika Afrika Mashariki. Majina katika hali yao ya upekee hayapashi ujumbe kikamilifu ingawa yana fahiwa na kimsingi huwa hayatumiki katika ombwe tupu kwani hutumikizwa katika muktadha ili kuwasilisha maana (Cruse, 2000). Kwa hivyo, hali hii ina maana kuwa majina aghalabu huwa na uwezo wa kudhihirisha maana anuwai kutegemea muktadha wa matumizi yake.

Uchanganuzi wa maana katika lugha hushughulikiwa katika taaluma ijulikanayo kama semantiki. Semantiki huchunguza uhusiano baina ya umbo na maana (Obuchi & Mukhwana, 2015). Lugha kama chombo cha mawasiliano ya binadamu huhitaji fasiri ya maana

zilizobebwa na maneno ili kutimiza hilo jukumu lake. Maneno yanapohusiana kwa njia ama ya ufinyu au ya upana kimaana huleta ukoa maana (Habwe & Karanja, 2004). Hivyo basi, semantiki hutalii maana katika viwango vyote vya lugha na ili kuielewa lugha bayana, aghalabu huchunguzwa kupitia viwango vyake kama vile: fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki (Lyons, 1981). Nerlich na Clarke (1997) wanaongezea kiwango cha pragmatiki ambacho wanakielezea kuwa ni falsafa ya lugha. Kazi za wataalamu wanne, yaani Charles Sanders, William James, John Dewey na John Austin zinajipambanua zaidi kwenye ulingo wa falsafa ya lugha. Falsafa ya lugha aghalabu hujishughulisha na nadharia za maana, matumizi ya lugha, utambuzi wake na uhusiano uliopo kati ya lugha na uhalisia wake katika maisha ya binadamu. Kwenye siku za hivi karibuni, Pragmatiki imehusishwa na kazi za mwanafalsafa Charles Morris anayezamia taaluma ya semiotiki (Levinson, 1983). Pragmatiki huonyesha uhusiano uliopo baina ya lugha na muktadha wake wa matumizi na huchangia uteuzi wa maneno yanayotumiwa katika mawasiliano ili kuwasilisha maana (Levinson, 1983).

Aitchson (2001) anaelezea kuwa kila kitu katika ulimwengu huu kipo katika mabadiliko. Akiyahusisha mabadiliko hayo na lugha, Sapir (1949) anaeleza kuwa, hakuna kitu ambacho ni tuami kwa asilimia mia moja. Kila neno, elementi ya kisarufi, msemo, sauti au mkazo hubadilika na kurekebishwa na mkondo usiodhahiri. Shukla na Linton (2006) wanaeleza kwamba lugha zote hubadilika kulingana na wakati. Kila lugha ni zao la mabadiliko na huendelea kubadilika kadri inavyotumiwa na jamii ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Aidha, Katamba na wenzie (1996) wanaeleza kwamba, sifa mojawapo ya lugha ni kubadilika katika vipengele vyake vyote vya kisarufi hasa maumbo na maana. Katika kufafanua suala la mabadiliko ya lugha Crystal (2003) na Campbell (2004) wanadokeza kuwa mabadiliko ya lugha ndio uhalisia wenyewe wa maisha ya lugha kwani hayawezi kuzuilika wala kuepukika. Kwa misingi hiyo, mabadiliko ya lugha yanaweza kufasiriwa kuwa mchakato ambao sauti, maumbo ya maneno, msamiati, maana, muundo na vipengele vingine vya lugha hubadilika.

Kutokana na tabia hii ya lugha ya kubadilika katika vipengele vyake vyote, ni dhahiri kuwa mfumo wa maana pia huathiriwa. Shukla na Linton (2006) wanadokeza kuwa mabadiliko haya ya maana katika lugha yanajibainisha zaidi katika ngazi ya neno. Wakiishadidia hoja hiyo, Wijaya na Yeniterzi (2011) nao wanakubaliana kuwa maana za maneno si tuami bali hubadilika kulingana na matumizi yake. Wakifafanua zaidi suala la mabadiliko ya maana za maneno, Ullmann (1970) pamoja na Wijaya na Yeniterzi (2011) wanaeleza kuwa neno linaweza kutunza maana yake ya msingi na likiendelea kupata maana nyingine za ziada kadri

linavyotumika katika miktadha tofauti. Maana hizi za ziada huweza kupata mashiko zaidi na hivyo kutumiwa zaidi na wazungumzaji wa lugha kuliko ile maana ya msingi.

Majina ya watu hutoa nafasi bora katika uchunguzi wa taaluma ya semantiki, mofolojia na sintaksia. Hii ni kwa sababu maana ya majina haya hutegemea kile mtoa jina anataka kuwasilisha kwa jamii na ndio huathiri umbo la jina hilo analoteua ili kuwasilisha maana hiyo (Lupenga, 2006). Vilevile, Msanjila na wenzie (2010) wanasema kwamba, majina ya jamii yanapochanganuliwa huwa yanakisi muundo wa lugha inayohusika. Hoja hiyo inashadidiwa na Thiong'o (1986) anaposema kuwa elimu ya mofolojia ya maneno katika lugha na misingi yake huimarisha uelewa wa lugha inayohusika kwa kiasi kikubwa. Kutoa jina ni kuwasiliana (Muzale, 1998). Hii inaashiria kwamba jina linaweza kupewa fasiri mbalimbali kutegemea muktadha, hali inayoweza kupelekea kubadilika kwa maana yake. Ingawa kuna utafiti mwingi kuhusu majina ya watu (Chauke na wenzie, 2015; Mutunda na wenzie, 2016; Odesanya na wenzie, 2017; Mensah, 2017; Alima, 2018), utafiti huu umekitwa mno katika kuchunguza vigezo vya kitamaduni vya utoaji wa majina na utambulisho katika jamii mbalimbali. Hali hii pia inaonyesha kuwa pana haja ya utafiti wa kiisimu kuhusu majina ili kuchangia ukuaji wa taaluma mbalimbali za isimu pamoja na kukuza maarifa ya majina kiisimu ya jamii ya Wamaragoli. Suala hili linashadidiwa zaidi na Kohnlein (2015) anaposema kuwa majina ya watu hayajatiliwa maanani sana katika utafiti kwa misingi ya kiisimu.

Kuna baadhi ya tafiti zilizofanywa kuhusu majina katika jamii ya Abaluhya. Mathalani, Lwangale (2016) anachunguza ruwaza za uhusiano wa kinasaba na kifamilia katika lahaja za Kiluhya huku akitumia data ya majina ya watu. Utafiti wake ulijihusisha sana na mfanano katika utamaduni wa kutoa majina hayo miongoni mwa jamii za Waluhya ambapo aligundua kuwa kuna mfanano na uhusiano katika utamaduni huo wa utoaji majina. Japo utafiti wa Lwangale (2016) haujishughulishi na mofolojia ya uundaji wa majina hayo, Baerman na Corbett (2007) wanasema kuwa kati ya vipengele vyote vya lugha, kipengele cha mofolojia ni cha lugha mahususi na hakiwezi kuchunguzwa katika utafiti kimajumui. Hali hiyo ndiyo iliyochochea utafiti wa uchanganuzi kimofosemantiki wa anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo na nomino za kawaida za Kiswahili.

Aidha, Malande (2011) anachunguza semiotiki katika majina halisi ya jamii ya Wamaragoli akiongozwa na nadharia ya Semiotiki. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha aina mbili za maana kisemiotiki katika majina hayo: maana halisi na maana husishi. Riemer (2010)

anasema kuwa namna bora ya kueleza maana ni kujitenga na dhana ambazo hazionekani na zisizodhibitika. Badala yake, inashauriwa tujikite katika uhalisia wa lugha katika kushughulikia maana. Yaani, maana ishughulikiwe kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya lugha. Kwa vile Malande (2011) anajibana kwenye thamani ya umbo anapochunguza maana kiishara katika majina pekee ya Wamaragoli, kuna haja ya kuchunguza anthroponimu kwa kuzingatia muktadha na dhima ya nomino za Kiswahili katika ujenzi wa anthroponimu zenyewe. Isitoshe, utafiti wake haujishughulishi na mabadiliko ya kisemantiki wala mbinu za kimofolojia zinazopelekea upatikanaji wa majina hayo ya Kimaragoli. Pana hitaji la kuyachunguza majina ya Kimaragoli upya kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ili kukuza maarifa zaidi ya kiisimu kuhusu mabadiliko ya kisemantiki na mbinu za kimofolojia zitumikazo kuyajenga majina hayo.

Nadharia ya Pragmatiki Leksia huchunguza maana ya maneno kwa mujibu wa muktadha wa kimatumizi ambao kwa kiasi fulani huathiri maana ya maneno hayo kiisimu. Hata hivyo, utafiti unaoongozwa na nadharia hii kuyachunguza majina ya watu ni muhali kupatikana. Hivyo basi, uchanganuzi wa kiisimu wa anthroponimu kwa misingi ya nadharia ya Pragmatiki Leksia unahitajika ili kuchangia kuikuza nadharia hii katika tafiti zaidi za kiisimu. Anindo (2016) anachunguza mofosemantiki ya majina ya mahali katika jamii ya Wamaragoli. Hata hivyo, utafiti wake unaegemea toponomastiki, tawi la taaluma ya onomastiki linalochunguza majina ya mahali. Hali hii inaangazia haja ya utafiti kufanywa katika tapo la anthroponomastiki kuchunguza majina ya watu ili kukuza maarifa ya kiisimu. Isitoshe, Anindo (2016) hakujihusisha na mbinu za kimofolojia wala mabadiliko ya kimaana katika uchunguzi wake wa majina ya mahali; hali inayobainisha pengo la kitaaluma linalohitaji kuchunguzwa. Kimsingi, uchunguzi wa majina ya watu hufanywa katika tawi la onomastiki linalojulikana kama anthroponimu.

### 1.2.1 Dhana ya Anthroponimu

Anthroponimu ni istilahi inayotumiwa katika taaluma pana ya onomastiki. Onomastiki ni sayansi maalumu inayochunguza au kutalii majina ya viumbe (Crystal, 1987). Taaluma hii hujishughulisha na njia za kubainisha majina ya mahali na watu. Majina ya watu hurejelewa kama anthroponomastiki au anthroponemia, istilahi ifupishwayo kuwa ni anthroponimia. Kwa upande mwingine, taaluma ijishughulishayo na majina ya mahali hujulikana kama toponomastiki, inayofupishwa kuwa toponimia au toponemia. Hivyo basi, taaluma ya onomastiki inagawika katika matapo mawili: anthroponomastiki ambayo huchunguza majina ya binadamu na toponomastiki ambayo huchunguza majina ya mahali. Utafiti huu ulijikita

katika tapo la anthroponomastiki ambapo lengo kuu lilikuwa ni kuchunguza mofosemantiki ya majina ya Kimaragoli yaliyojengwa kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili. Kimsingi, anthroponimu inahusu majina ya pekee ya watu.

Wataalamu wengi wanarejelea anthroponimu kuwa ni nomino za pekee. Mathalani, Saluhaya (2010) anabainisha kuwa nomino za pekee hutambulisha mtu binafsi, mahali, wazo au kitu mahususi kwa kukirejelea kwa jina lake maalum kama vile: bahari, siku za wiki, majengo, miezi, raia, maziwa, makabila, milima, n.k. Baadhi ya nomino za pekee ni kama vile: Uhuru, Bahari la Hindi, Agosti, Makavazi ya Kitaifa, Turkana, Dar es Salaam, Wakenya, Mwembetayari, Selemani na Ziwa Victoria. Masebo na Nyangwine (2014) wanaonekana kukubaliana kuwa majina ya pekee ni majina maalumu ya watu au mahali na aghalabu hudhihirisha upekee kwa watu au vitu hivyo. Wanaendeleza kuwa, majina ya watu yanajumuisha majina ya watu kama vile: Wanjiku, Onyango, Aziza, n.k. Pia, majina ya mahali ni kama vile: Njoro, Mogadishu, Ushelisheli, Moshi, Marekani, n.k. ni nomino za pekee. Khamisi (2011) akichangia kuhusu nomino za pekee anasema kuwa jina la pekee lina sifa ya umbo la kitu hicho au tabia yake na kuwa kitu hicho huwa kimoja katika ulimwengu mzima kwa mfano, majina ya nchi, watu na mahali. Wataalamu hawa wanaonekana kukubaliana kuwa majina ya watu ni miongoni mwa nomino za pekee. Hata hivyo, utafiti huu haujachunguza nomino zote za pekee bali ulijikita katika kipengele kimoja cha majina ya pekee, ambacho ni majina yanayojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Istilahi 'nomino' ni tafsiri ya neno la Kilatini linalotumika kutajia dhana kama vile: vitu, watu, hali mbalimbali, mahali na vitendo na kadhalika (Habwe & Karanja 2004).

Habwe na Karanja (2004) pamoja na Kihore na wenzie (2009) wanakubaliana na wanaisimu wengine kuwa nomino za Kiswahili ni za aina nyingi na zinajumuisha: nomino za pekee, dhahania, jamii, kitenzi-jina, kawaida, mguso na zinazohesabika. Utafiti huu ulilenga nomino za kawaida za Kiswahili zinazochangia uundaji wa majina ya Kimaragoli. Nomino za kawaida aghalabu hurejelea vitu, viumbe au dhana ambazo si mahususi. Yaani, vitu ambavyo havihodhi sifa za upekee kama vile samaki, mkono, kunguni, kalamu, maji, n.k. (Matinde, 2012).

### 1.2.2 Jamii ya Wamaragoli

Wamaragoli ni jamii mojawapo katika jamii pana ya Abaluhyia. Jamii hii huzungumza lugha ya *Lulogooli*, yaani Kimaragoli. Lugha ya *Lulogooli* ni lugha ya Kibantu. Guthrie (1948) alijumuisha lugha ya Kimaragoli katika kundi la lugha za Kibantu za Kati na akaianisha

katika kundi la E42 huku lugha ya Ekegusii ikiwekwa JE43 ikifuatwa na Kikuria (JE44) kwa ukaribu sana. Herufi ‘E’ inasimamia Mashariki, yaani *East* katika Kiingereza ambalo ni kundi la Bantu la Mashariki. Ethnologue (2015) inaainisha Kimaragoli kuwa ni mojawapo ya lugha za Kibantu zipatikanazo Afrika Mashariki. Lugha ya Kimaragoli ina asili yake katika lugha azali ya Naija-Kodofani. Vinginevyo, Kimaragolo hurejelewa kama *Luragoli, Llogole, Logoli, Rogoli, Llugule, Maragoli,* au pia *Uluragooli.* Akiielezea zaidi kuhusu jamii hii, Anindo (2016) anasema, mzizi *-logooli* unaweza kupachikwa viambishi awali mbalimbali na kuwasilisha maana tofauti tofauti kama vile: *Lulogooli* - lugha, *Evologoli* - mahali wanakoishi wazungumzaji wa *Lulogooli, Mulogooli* - mzungumzaji wa lugha ya *Lulogooli*, *Valogooli* - wazungumzaji wengi wa lugha ya *Luloogoli.* Anafafanua kwamba ‘Maragoli’ ni istilahi inayotumika sana ikirejelea mtu kwani wazungumzaji wa *Lulogooli* wanaamini kuzaliwa kutoka kwa baba yao, Mulogooli. Wazungumzaji wa Kimaragoli wanapatikana sana kwenye Kaunti ya Vihiga, katika eneo la Magharibi mwa Kenya ambalo kiisimu, linaaminika kuwa chimbuko la lahaja za Kiluhya kama vile: Kinyore, Kikhayo, Kiisukha, Kikisa, Kitiriki, Kitachoni, Kibukusu na kadhalika (Wangila, 2014).

Tafiti zinazohusiana na jamii ya Wamaragoli zinasema kuwa Wamaragoli walihama kutoka nchi ya Kameruni, wakiwa na Wabantu wengine (Nurse & Philippson, 2003; Sangili, 2017). Hata hivyo, kupitia elimu na maarifa wanayotoa katika fasihi simulizi zao, wanaonekana kuamini kuwa walitoka nchi ya Misri. Kwa mujibu wa Sangili (2014) Wamaragoli walihama kutoka sehemu inayojulikana kama Eluhya kusini mwa nchi ya Misri sehemu ijulikanayo kama Lok Kitang, Turkana ya sasa, Kaskazini mwa Kenya. Mchakato huo wa kuhama ulifanikishwa chini ya uongozi wa mzee Andimi. Mzee huyu alikuwa na familia tatu. Mulogoli anayeaminika kuwa mwanzilishi wa jamii hii alizaliwa katika familia ya mke wa kwanza. Mulogoli baadaye alioa na kujaliwa watoto watano - wa kiume wanne na wa kike mmoja. Watoto wa kiume walifunga ndoa na kujaliwa kupata watoto wengi ambao wanaunda koo za jamii hii (Sangili, 2014).

Hata hivyo, kuwepo kwa Watoto wengi na wale walioendelea kuzaliwa kulipunguza mashamba hali iliyofanya Wamaragoli kuhamia maeneo mengine. Kutokana na usaili uliofanyiwa baraza la kuu la wazee Wamaragoli wakati wa utafiti huu[1], Wamaragoli walianza kuhamia maeneo mbalimbali mwaka wa 1920 kama vile, Lugari, Migori, Kitale, Nandi na maeneo mengine. Kwa mujibu wa Baraza kuu la wazee wa jamii hii, sababu zilizopelekea

baadhi ya Wamaragoli kuhama ni nyingi na tofauti. Hata hivyo, sababu kuu ilikuwa kutafuta shamba. Hatua hii ilichochewa na shughuli kuu ya kujikimu na kujipatia kipato ya jamii hii ambayo ni kilimo. Hivyo basi, walihama wakitafuta shamba la kuendeleza kilimo cha mahindi, mboga na ufugaji wa mifugo mbalimbali.

Aidha, kwa mujibu wa Baraza la wazee Wamaragoli, Wamaragoli wengi ni Wakristo na waumini wa dhehebu la Marafiki (Friends Church, yaani Quakers). Hii ni kwa sababu Wamishenari wa dhehebu la Quakers walipowasili Magharibi mwa Kenya kutoka Uingereza, walifululiza hadi Kaimosi mnamo mwaka wa 1902 mbapo walijenga afisi kisha wakaanza shughuli za kuhubiri Injili ya Kristo miongoni mwa jamii ya Wamaragoli. Hatua hii ilipeleke wengi kujitokeza kujifunza kusoma na kuandika huku wakihubiriwa na kuombewa.

### 1.2.3 Tafiti Zinazohusu Kimaragoli

Kuna tafiti chache zimefanywa kuhusiana na masuala mbalimbali ya mfumo wa lugha ya Kimaragoli. Baadhi ya tafiti hizo zinaonekana katika Adagala (1979), Bwonya (1998), Kabaji (2005), Jumba (2007), Ambuyo (2008), Aseyo (2011) na Sangili (2017, 2019). Adagala (1979) anachunguza namna viambishi *Tsi* na *Tsya* vya Lulogooli vinavyotumika katika lugha na fasihi katika shule za msingi. Utafiti wake unafafanua kwamba viambishi *Tsi* na *Tsya* haviachani katika sentensi za lugha hii na aghalabu vikitokea kama viambishi awali, *Tsi-* huonyesha wingi ilhali *Tsya-* hutumika kama kiambishi nafsi kimilikishi kwa mfano *Tsingombe Tsya dada* (Ngo'mbe wa baba). Kama viambishi tamati *-tsya* hujitokeza kwenye vitenzi kuonyesha dhana ya kwenda kwa mfano, *vakana vatsya kotenya mmuritu* (wasichana walienda kutafuta kuni msituni). Kwa upande mwingine, a*vakana vatsi* (wasichana wamekuja). *-tsi* kama kiambishi tamati kinaonyesha dhana ya kuja. Iligunduliwa kwamba fanani katika jamii hii hutumia sana *Tsi* na *Tsya*.

Bwonya (1998) anachunguza taswira ya mwanamke katika nyimbo za harusi za jamii ya Wamaragoli. Inabainika kwamba nyimbo za harusi za jamii ya Wamaragoli hutungwa na wanawake na aghalabu huimbwa na wanawake ili kuwasilisha ujumbe maalum wa ndoa kwa bibi harusi, matarajio ya kijamii kwa mwanamke anayepata nyumba kupitia harusi na katika nyimbo hizo mwanamke ndiye huchukua nafasi ya mbele na anayelengwa kuliko mwanamme. Licha ya kumtayarisha yeye pamoja na familia yake kuwa atatoweka, nyimbo hizi humchorea hali ngumu ya maisha ya ndoa kwa mfano, *wimbo wa nuvudinyu kutura winyu kuzia handi*.

Kabaji (2005) anachunguza maudhui ya kijinsia katika muktadha wa kitamaduni wa jamii ya Wamaragoli huku akijikita katika ngano za jamii hii. Akitumia nadharia ya Ufeministi, utafiti wake unaweka wazi namna ngano za jamii hii zinakweza jinsia ya kiume na kudunisha jinsia ya kike. Kupitia wahusika na uhusika katika ngano za jamii hii ambapo mwanamke anachorwa kama mwoga anayeogopa mizimwi ya kiume, pia inaupa nguvu uhusika wa kiume dhidi ya kike, wahusika wanyama, ndege, mimea, vitu, mizimwi na miungu ya kiume inaonekana yenye nguvu nyingi kuliko ile ya kike.

Jumba (2007) anatafitia mofosintaksia ya kishazi tegemezi katika Lulogooli. Utafiti wake unajikita katika sentensi za Lulogooli ambapo unagundua kuwa lugha hii ina mpangilio wa kiashiria, kitenzi na kiashiriwa na aghalabu nomino inayozungumziwa hutajwa mwanzoni mwa sentensi kwa mfano, *Kibisu aragira uvuchima* (Kibisu anakula ugali). *Kibisu* ni mtendaji, *aragira* (anakula) ni kitenzi *kikuu* na (uvuchima) ni ugali. inabainika kwamba katika lugha ya Lulogooli, wazungumzaji hutumia kiimbo na mkazo kubainisha maana mahususi katika sentensi wanazozitoa.

Vilevile, Ambuyo (2008) anachunguza uamilishi dhima katika sentensi ya Lulogooli akiongozwa na nadharia ya Sintaksia Finyizi. Anadhihirisha kuwa sentensi ya Lulogooli huundwa kutokana na maneno kisarufi. Maneno hayo yanaweza kuwa maneno leksia au amilishi. Maneno leksia huhusisha mojawapo ya maneno kama vile, nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi na vihusishi na virai vyao. Maneno amilishi huhusisha vibainishi, shamirisho na viunganishi. Utafiti wake pia unaonesha jinsi uhamisho wa dhima mbalimbali katika sentensi ya Lulogooli huathiri muundo wa sentensi kwa ujumla. Kila uhamisho huacha hamishe inayotambulika kisintaksia, kwa kuzingatia kanuni arifishi, kanuni nyinginezo zinazojitokeza ni kanuni ya ufungami, kanuni ya theta na kanuni hamishe katika sentensi za Lulogooli.

Aseyo (2011) anachunguza iwapo maneno ya Lulogooli yanaweza kuingizwa katika mfumo wa *open source spellchecher* wa kutabiri na kukamilisha maneno ya Lulogooli yanayopigwa chapa katika tarakilishi. Katika mradi wake, anafaulu kuingiza baadhi ya maneno ya lugha hii katika mfumo wa kidijitali wa *spellchecker,* haswa vitenzi. Kwa mfano, PFX5180-Vata: vitenzi vinavyojitokeza vya kukamilisha kitenzi kilichoanzishwa kupiga chapwa ni; *vatadeka, vatagenda, vatakuza, vataseka, vatahama, vatamonya, vatamira, vatamiga* n.k

Sangili (2017) anahakiki namna mazingira ya Wamaragoli yanavyochangia na kuathiri kubuniwa kwa methali za jamii hii. Kwa kuongozwa na nadharia ya Ubuntu, utafiti wake

unagundua kwama methali nyingi za Wamaragoli zimetokana na mazingira ya jamii hii kwani kuna methali zinazozungumzia miti, nyasi, milima, mito n.k. Kwa mfano, *evembe nivina utavina ku dave*. Katika methali hii *evembe* ni aina ya nyasi inayomea katika mazingira ya jamii hii iliyokuwa ikitumika kuezeka nyumba kabla ya mabati kuanza kutumika. Kutokana na wingi wake, wanajamii wanashauriwa kuwa watu hata wawe wengi kivipi wakifanya jambo usifanye tu kwa sababu wanafanya, jiulize kwa nini wao wanatekeleza jambo hili na litakuathiri vipi? Kwa hivyo *evembe* ni watu ilhali *kuvina* ni kutekeleza jambo fulani.

Vilevile, Sangili (2019) anachunguza namna Lugha ya Kimaragoli inavyodumishwa katika eneo bunge la Uriri gatuzi la Migori, Kenya. Utafiti wake unabainisha mikakati inayoathiri udumishaji wa lugha ya Kimaragoli katika eneo la Uriri. Mikakati hiyo ni pamoja na mkakati wa kufundisha Kimaragoli, mkakati wa kutumia Kimaragoli katika kuabudu kanisani, kutumia Kimaragoli katika idhaa, kutumia Kimaragoli katika kuendesha shughuli za mikutano ya vyama, kuzungumza Kimaragoli nyumbani, kutembelea wengine, kuandaa makongamano ya kitamaduni na uhimizaji wa mabaraza ya machifu kuendeshwa katika Kimaragoli. Aidha, utafiti wake ulibaini kuwa maneno mengi ya Kiluo hayajaingizwa katika Kimaragoli japo kulikuwa na kuathiriwa kwa Kimaragoli cha zamani.

Ingawa tafiti hizi zinahusu lugha na jamii ya Wamaragoli, pangali pana mwanya na pengo la kiakademia ambalo halijapewa uzito unaostahili, hasa uchanganuzi wa anthroponimu za jamii hii zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili kwa kutumia maarifa ya kiisimu.

### 1.2.4 Suala la Utafiti

Anthroponimu ni kipengele muhimu cha maarifa ya kiisimu. Maana ya anthroponimu hufungamana na lugha pamoja na miktadha ya kijamii; hali hii hutatiza ufasiri wa maana inayokusudiwa. Ufasiri kisemantiki wa anthroponimu ni zaidi ya uchanganuzi wa mofu na maana msingi inayowasilishwa. Maana msingi ya anthroponimu aghalabu hutofautiana na maana iliyosimbwa kwenye miktadha mahususi ya matumizi kijamii. Kwa hivyo, maana ziwasilishwazo na anthroponimu zinaweza kufafanuliwa kwa kuchunguza usimbaji wa ujumbe pamoja na mbinu zisababishazo uundaji wa maneno katika lugha inayohusika. Tafiti za awali kuhusiana na maana za kileksika za anthroponimu za Wamaragoli zimeonesha mabadiliko ya kimaana kwenye miktadha ya kijamii kwa ujumla. Hata hivyo, vipengele vya miundo ya kimofolojia pamoja na maana za kipragmatiki za anthroponimu hizi havijashughulikiwa kwa kina. Isitoshe, dhima ya nomino za kawaida za Kiswahili katika

ujengaji wa anthroponimu za Kimaragoli haijaangaziwa kwa kina.tafiti hizi za awali zilishughulikia majina ya wamaragoli kwa kulenga mitazamo ya upeanaji wa majina kv majira, mazingira, nyakati, matukio nk. Hata hivyo, inabainika kuwa uchunguzi wa majina ya Kimaragoli yanayojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili haujapewa kipao mbele. Hii ndiyo chachu iliyochochea uchunguzi kimofosemantiki wa anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili. Pamoja na kufafanua mabadiliko ya kisemantiki ya anthroponimu za Kimaragoli kwenye miktadha ya kijamii, uchunguzi huu unadhihirisha pia mbinu za kimofolojia zinazopelekea kuzalishwa kwa maumbo anuwai ya anthroponimu hizi.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliazimia kuchanganua kimofosemantiki anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Ili kuifikia azma hii, shabaha maalumu zifuatazo zilishughulikiwa:

i) Kuainisha nomino za kawaida za Kiswahili zijengazo anthroponimu za Kimaragoli katika vikoa maana.

ii) Kuchanganua mbinu za kimofolojia za uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

iii) Kufafanua mabadiliko ya kisemantiki katika anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Ili kuafikia madhumuni ya utafiti huu maswali yafuatayo yalizingatiwa:

i) Nomino za kawaida za Kiswahili zinazotumika kujenga anthroponimu za Kimaragoli zinaweza kuainishwa katika vikoa vipi vya maana?

ii) Mbinu zipi za kimofolojia hutumika katika uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili?

iii) Mabadiliko yepi ya kimaana hujitokeza katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili?

## 1.5 Upeo wa Utafiti

Kuna majina mbalimbali; ya watu, wanyama, mahali, mimea na kadhalika katika jamii ya Wamaragoli. Anthroponimu ni istilahi inayotumika katika taaluma ya onomastiki kurejelea majina ya watu (Crystal, 1987). Hivyo basi, anthroponimu zilizochunguzwa katika utafiti huu ni zile za pekee za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Utafiti ulitekelezwa katika eneo la kijiografia la Gatuzi Dogo la Sabatia lipatikanalo katika kaunti ya Vihiga.

Pamoja na eneo la kijiografia, utafiti uliegemezwa pia katika maeneo yafuatayo ya kiisimu: taaluma ya onomastiki na isimujamii. Onomastiki ni taaluma maalumu inayochunguza kwa undani majina ya viumbe (Crystal, 1987) na isimujamii huchunguza matumizi ya masuala ya kiisimu kwa mujibu wa jamii inayohusika. Taaluma ya onomastiki inajumuisha mbinu za kutambua majina ya watu na mahali. Hivyo basi, hugawika katika matawi mawili makuu: anthroponomastiki tawi linalochunguza majina ya binadamu na toponomastiki tawi linalochunguza majina ya mahali. Utafiti huu uliegemea tawi la anthroponomastiki huku mabadiliko ya kimaana kipragmatiki na vilevile mbinu za kimofolojia zinazounda anthroponimu hizo zikizingatiwa.

Ingawa lugha hukumbwa na mabadiliko ya aina nyingi kama vile: badiliko la kifonolojia, badiliko la kileksia, badiliko la kimofolojia, badiliko la kisintaksia, badiliko la kisemantiki na badiliko la kiothografia. Utafiti huu ulijishughulisha na badiliko la maana. Aidha, maana ilishughulikiwa katika kiwango cha neno wala sio katika viwango vingine vikubwa vya lugha kama vile kirai, kishazi au katika kiwango cha sentensi. Maneno ambayo yalishughulikiwa katika utafiti huu ni majina ya wamaragoli yanayojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Isitoshe, utafiti huu uliongozwa na nadharia moja, nadharia ya Pragmatiki Leksia.

## 1.6 Misingi za Uteuzi wa Mada

Kuna mjadala wa kitaaluma unaoendelea kuhusu nadharia ya onomastiki, yaani ni nadharia ipi iliyo na uwezo wa kushughulikia taaluma hii. Hivyo basi, kutekeleza utafiti huu ni ari ya kutaka kushiriki mjadala huu wa kiakademia wa kimataifa kwa kuonyesha kuwa masuala ya kionomastiki yanaweza kushughulikiwa kwa kutumia nadharia ya kiisimu, hasa nadharia ya Pragmatiki Leksia. Isitoshe, wataalamu wengi wa taaluma ya onomastiki wameshughulikia sababu za kitamaduni za utoaji majina bila kushirikisha maarifa ya kiisimu katika uchunguzi wao, hasa pragmatiki na mofolojia. Hali iliyochochea zaidi uteuzi wa suala hili ili kuchangia onomastiki kutumia mawazo ya kiisimu.

Vilevile, tafiti nyingi zimefanywa katika taaluma ya mofolojia ambazo zilihusisha mofolojia ya uambishaji. Kwa mfano, mofolojia ya uambishaji wa vitenzi; hali inayoonesha kuwa mofolojia ya nomino, hasa mofolojia ya uundaji wa anthroponimu haijachunguzwa kwa kina. Hali hii ilichochea utafiti huu kufanywa ili kufafanua mofosemantiki ya anthroponimu za Wamaragoli katika misingi ya nadharia ya kiisimu.

Aidha, kuna fikra kuwa muundo wa majina na mfumo wake wa maana unalandana katika lugha zote duniani (Lehrer, 1974). Kutokana na hali hii ya ujumuishaji wa masuala ya lugha, majina pia huchukuliwa kuwa na sifa ya ubia katika jamii zote ulimwenguni (Khoo & Na, 2006). Hivyo basi, mada hii iliteuliwa ili kung'amua hali halisi iliyoko katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili.

Licha ya uwepo wa tafiti nyingi zinazohusu Wamaragoli, ni muhali kupata utafiti wa kina uliozamia suala la mbinu za kimofolojia za uundaji wa majina ya Wamaragoli yanayojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili na mabadiliko ya maana katika majina hayo. Hali ambayo ilipelekea uteuzi wa mada hii ili kufidia mwanya huu wa kitaaluma. Shirika la UNESCO na azma maarufu, Azma la Asmara chini ya Muungano wa mataifa ya Afrika (AU) walitoa wito kwa watafiti kuchunguza lugha asili ili kuzidumisha lugha hizo na kukabiliana na tatizo la kufa kwa lugha (UNESCO, 2003; AU, 1995). Wito huo ulichochea utafiti huu uliochanganua mofosemantiki ya athroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili.

### 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti aghalabu hutarajiwa kunufaisha mtekelezaji wa uchunguzi huo, asasi mbalimbali zinazohusika na utafiti huo au kuinufaisha jamii kwa ujumla (Oso na Onen, 2005). Nao Njoroge na Gatambuki (2012) wanaendeleza zaidi kwa kusema kuwa zawadi ya thamani kubwa ambayo mzazi anaweza kumpa mtoto wake ni kumfunza lugha ya kiasili na utamaduni. Hii ni kwa sababu lugha ya kiasili ina umuhimu mkubwa kwani ndiyo hutoa nafasi kwa watumiaji kuelewa ulimwengu wao. Hivyo basi, utafiti huu una umuhimu mwingi kwa mtafiti, jamiii ya Wamaragoli na wanaisimu kwa ujumla.

Utafiti huu unahusu anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili una umuhimu mkubwa katika kuonyesha mchango wa lugha ya Kiswahili katika kuendeleza lugha za kiasili za Kiafrika. Licha ya kuwa lugha ya Kiswahili imetumika kikamilifu kuutekeleza kuanzia hatua ya mwanzo hadi hatua ya uandishi wa tasnifu, nomino

zake za kawaida zilitumika kujenga anthroponimu za Kimaragoli. Hali hii inaweza kuchochea tafiti zaidi za lugha za Kiafrika kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu unaitanabaisha serikali na wanajamii kwa ujumla katika kuhifadhi lugha za kiasili kwani vipengele fulani vya lugha kama vile majina husheheni maarifa mengi muhimu ambayo hayajahifadhiwa. Kwa mfano, maarifa kuhusu maana na mofolojia za anthroponimu za Wamaragoli zinaweza zikatumika katika mfumo mpya wa elimu ya mtalaa wenye msingi wa kiumilisi yaani *Competency Based Curriculum* (CBC) ambao unapendelea lugha za kiasili. Kwa vile elimu na udumishaji wa lugha za kiasili ni masuala ambayo hayaachani, utafiti huu unaathiri uundwaji wa sera na utekelezwaji wa mtaala na uendelezaji wa lugha asilia.

Aidha, mchango wa utafiti huu kitaalamu unadhihirika katika taaluma ya isimu, hii ni kwa sababu, kupitia kwa nadharia ya Pragmatiki Leksia iliyoongoza utafiti huu watafiti wa baadaye wataelimishwa kuhusu uwezo wake wa kushughulikia masuala ya onomastiki na ya kiisimu kama vile pragmatiki (mabadiliko ya maana) taaluma ya mofolojia hasa mbinu za kimofolojia za uundaji wa maneno.

Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa wataalamu mbalimbali wa sayansi za kijamii kama vile: wanaisimuanthropolojia, wanaanthropolojia, wanaethnografia na wanasosholojia kwa sababu wataurejelea utafiti huu katika tafiti zao zinazohusu Wamaragoli na sayansi ya kijamii na lugha nyingine zinazokaribiana na Kimaragoli. Fauka ya hayo, utafiti huu utawanufaisha wanaleksikografia ambao wanahusika na uundaji wa kamusi za majina ya lugha za Kibantu, hasa Kimaragoli, kuelewa mbinu zilizopelekea kuundwa kwa majina ya Wamaragoli na mabadiliko mbalimbali ya maana katika majina hayo.

Utafiti huu unachocheo wasomi na watafiti wa baadaye kuchunguza masuala ambayo hayajashughulikiwa katika utafiti huu. Aidha, utasaidia katika kuendeleza lugha ya Kimaragoli ikizingatiwa kuwa lugha za kiasili ziko katika hatari ya kufa na kusahaulika na wanajamii wa kisasa hivyo basi, kule, kuchunguza lugha hii kutasaidia kuidumisha. Kwa vile utafiti unalenga kushughulikia mabadiliko ya kimaana katika muktadha na mbinu za uundaji wa majina, matokeo yake yatasaidia kukuza viwango vya lugha hii kwa wasomaji kwani watapata ufafanuzi wa kipekee utakaowawezesha kutengeneza maneno zaidi na kufidia upungufu wa msamiati wao kwa ujumla. Utafiti huu unaashiria namna Kiswahili kilivyokua na dhima yake katika kutekeleza majukumu muhimu kama vile utafiti hivyo basi kuchochea kukumbatiwa kwa matumizi yake katika mawanda mengineyo.

## 1.8 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu unaongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksia iliyoasisiwa na Blutner (1990). Baadaye, nadharia hii iliendelezwa na Wilson (2003) kwenye mihadhara yake katika Chuo Kikuu cha Havard. Iliendelezwa pia na Wilson na Carston (2007).

Nadharia ya Pragmatiki Leksia imejikita katika uchunguzi na uchanganuzi wa maana na jinsi maana inavyobadilika katika muktadha. Aidha, Nadharia ya Pragmatiki Leksia inachunguza maana ya kimsingi kabla ya kuangalia maana ya kimuktadha ya maneno. Inafafanua kwamba, vipashio vya kileksika vya lugha aghalabu huchanganuliwa kwa utaratibu. Vilevile, vipashio hivi hufasiriwa kwa mujibu wa muktadha mahususi. Hata hivyo, mchango wa semantiki katika ufasiri wa kijumla wa tamko umebanwa kuliko namna ilivyodhaniwa mwanzoni. Pragmatiki Leksia hujaribu kuelezea hali za kipragmatiki zilizojumuishwa na semantiki hiyo chini ya umahususi wa vipashio vya kileksika.

Nadharia Pragmatiki Leksia ina mihimili mingi ila ile iliyoufaa utafiti huu katika uchanganuzi wa data ya utafiti ndiyo inayofafanuliwa. Mihimili hiyo ni pamoja na Semantiki Leksika pamoja na Michakato ya Kipragmatiki Kileksika. Semantiki Leksika hujishughulisha na maana katika kiwango cha neno. Maneno huchukuliwa kuashiria vitu katika ulimwengu au katika dhana kutegemea mtazamo mahususi wa Semantiki Leksika. Kwa mujibu wa Mbwanga (2010) vitengo vya maana katika Semantiki Leksika humwezesha mzungumzaji wa lugha kuongezea maana kwa mfululizo maishani pamoja na ujifunzaji wa maneno mapya na maana zao.

Mhimili wa Semantiki Leksia uliusaidia utafiti huu kuafikia lengo la kwanza la utafiti. Yaani, kubainisha nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli katika vikoa maana. Nao mhimili wa michakato ya kipragmatiki kileksika ulizingatiwa katika madhumuni ya pili  kuchanganua mbinu za kimofosemantiki za uundaji wa anthoponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili pamoja na madhumuni ya tatu. Yaani, kufafanua mabadiliko ya kisematiki katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili

Mhimili wa Semantiki Leksia unazingatiwa katika utafiti huu ambapo, anthroponimu zinazohusiana kimaana zinawekwa moja kwa moja katika kikoa maana kimoja. Kikoa maana ni dhana ya kisemantiki iliyotumika kuainisha vipengele vya kileksika kwenye makundi anuwai ya kimaana. Akiwarerejelea Wilson (2003) na Cartson (2002), Blutner (2011) anafafanua mambo ya msingi yanayoshughulikiwa na Pragmatiki Leksika. Mambo yenyewe

huainishwa kwenye makundi kama vile ubanaji wa kileksika, upanuzi wa kisitiari, kisio la maana na uundaji wa maneno.

**a) Ubanaji wa Kileksika**

Kwa mujibu wa Kolaiti na Wilson (2012) ubanaji wa kileksika ni mchakato unaohusisha matumizi ya neno kuonyesha dhana mahususi au maana finyu zaidi kuliko maana iliyosimbwa kiisimu, yaani maana pana ya neno ambayo ndiyo ilisimbwa kiisimu. Ubanaji unapofanyika, maana au dhana inayopatikana kwenye muktadha wa matumizi aghalabu huwa ndogo au finyu kuliko ilivyokuwa katika maana msingi. Maana inayojitokeza huwa ni kijisehemu tu cha maana pana ambayo imesimbwa. Katika ufafanuzi wake, Anusu (2015) anatumia mfano, '... niko *ndani ndani ya Jubliee.'* Neno 'ndani' katika Kiswahili linafumbata dhana ya NDANI. Ili kuelewa kikamilifu maana ya '*ndani',* msikilizaji lazima afasiri kwa mujibu wa muktadha wa matumizi unaohusika. Maana ya '*ndani ndani'* ni pana kwa kiasi fulani. Horn na Ward (2004) wanaueleza ubanaji kuwa ni mchakato unaoweza kusawazishwa na kwamba hutegemea muktadha wa matumizi. Maana iliyosimbwa inaweza kubanwa katika viwango mbalimbali kutegemea muktadha. Kwa hivyo, maana pana ya mfano huu ni *ndani wala sio upande wa nje,* ilhali maana mahususi ni 'ndani ya chama cha Jubilee' na kwamba hakuna kinachoweza kumtoa humo.

Mfano mwingine mwingine anaotumia Anusu (2015) ni, *Onyango ana kirusi*. Neno 'kirusi' katika utungo huu limesimba dhana ya KIRUSI inayojumuisha 'aina nyingi za virusi vinavyoweza kusababisha magonjwa mbalimbali.' Hata hivyo, kwenye muktadha huu, maana ya 'kirusi' imebanwa zaidi kwa maana ya 'maradhi ya Ukimwi.' Kwa mujibu wa Blutner (1998) ubanaji ni kutumia faridi ya kileksika kuwasilisha maana iliyobanwa zaidi kuliko maana msingi ambayo imesimbwa kisemantiki. Kisemantiki, dhana 'kirusi' ina maana ya 'kiini kisababishacho ugonjwa' (Mdee na wenzie, 2011) ilhali kwenye muktadha wa mazungumzo, neno 'kirusi' lina maana ya 'kirusi cha Ukimwi.' Virusi vingine vimetengwa katika muktadha huu (Anusu, 2015). Mhimili hiki kilitumiwa kuonyesha fahiwa mahususi zaidi kuliko ile iliyosimbwa katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili; hali iliyobainisha maana finyu zaidi ya anthroponimu zinazohusika katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli.

**b) Upanuzi wa Kileksika**

Kwa mujibu wa Fromkin na wenzie (2011), upanuzi wa kileksika ni mchakato ambao kwao maana ya neno huongezeka au kutanuka kwenye muktadha wa matumizi. Neno linaakisi

maana msingi ya awali pamoja na kuzidisha maana nyinginezo. Kwa hivyo, neno linapopanuka kimaana huwa limeongezewa vitajwa vingine; hali inayopelekea neno hilo kuwa na fahiwa nyingi zaidi ya maana yake kisemantiki. Maneno yanayohusika aghalabu hupewa maana nyingine moja au zaidi pasipo kuipoteza maana asilia (Ullmann, 1970). Maana asilia na maana ya pili hudhihirika sambamba ilimradi pasikuwepo mkinzano (Anusu, 2015). Mhimili huu ulisaidia kubainisha namna maana ya athroponimu za Kimaragoli ilivyopanuka pasipo kupoteza maana yake asilia.

**c) Upanuzi wa Kisitiari**

Upanuzi wa kisitiari hufasiliwa kuwa ni mchakato unaopelekea maana ya neno kuwa mbali na maana tambuzi (Simiyu, 2016). Sitiari ni uhamishaji wa maana kutoka kwa kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vikoa maana vinavyohusika katika uhamishaji huu angalau vinatofautiana kwa sifa ya kisemantiki moja ya msingi (Odoyo, 2006). Kwa hivyo, kinachohamishwa ni tabia, sura au dhima ya kitu kwa kukihusisha na tabia, sura au dhima ya kitu kingine (Lakoff & Johnson, 1980).

Kuifafanua dhana hii, Anusu (2015) anatoa mfano wa tungo, *Onyango ni mburukenge*. Mburukenge ni mnyama ilhali Onyango ni binadamu. Kwenye muktadha huu, Onyango anafananishwa na mburukenge kwa sababu ya tabia zake. Hata hivyo, leksimu hii ya 'mburukenge' inasimba dhana MBURUKENGE. Msikilizaji anatenga dhana za dharau kama vile, 'mburukenge ni mnyamapori mwenye akili punguani.' hata hivyo, ukweli ni kwamba hicho sicho anachomaanisha msemaji. Msikilizaji anachukulia kwamba Onyango 'ni mjinga.' Kwenye sitiari ya kiasili, vitu amba vinavyolinganishwa huwa na uwezekano wa kutofautiana na vikoa maana tofauti, au hata kulandana (Aitchison 2003). Sitiari za kiasili zinalingana kwenye sifa chache za kawaida. mhimili huu wa upanuzi wa kisitiari uilifanikisha uchunguzi wa mabadiliko ya upanuzi wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

**d) Kisio la Maana**

Katika nadharia ya Pragmatiki Leksika, kuna pia mchakato wa kipragamatiki wa kisio la maana. Hili ni badiliko linalopelekea neno lenye maana thabiti kiasi kupanuliwa ukingoni na kujumuisha mawanda ya makundi ambayo kwa hakika yanapatikana nje ya maana yake kamili ya kiisimu. Matumizi kilegevu ya takwimu za kukadiria, msamiati ya kijiografia pamoja na misamiati inayoelezwa kwa njia ya kukanusha ni mifano ya kisio la maana (Wilson, 2003). Hapa, dhana inayowasilishwa na neno linalotumika inajitenga zaidi na dhana

iliyosimbwa. Katika kisio la maana, maana tambuzi inadondoshwa ili kuwezesha uzalishi wa maana iliyosimbwa (Carston, 2002). Mhimili huu ilitumiwa kuchunguza namna maana ya anthroponimu inavyobadilika, haswa maana ya kawaida inapodondoshwa na kuibuliwa kwa maana mpya iliyosimbwa katika anthroponimu zinazohusika.

**e) Uundaji wa Maneno**

Nadharia ya Pragmatiki Leksika pia hujishughulisha na kitengo cha uundaji wa maneno mapya pamoja na uzalishaji wa maana mpya (Wilson, 2003). Maneno yanayoundwa aghalabu huichangia nadharia hii data zaidi kwa kueleza michakato ya kiakili na hali za kimaumbile zinazohusika. anatoa Baadhi ya mbinu za kimofolojia zinazotumika katika uundaji wa maneno ya lugha ni pamoja na: ukopaji, uhusishaji, uradidi, uambatishaji, tafsiri na kadhalika (Ohly, 1977). Mhimili huu wa uundaji wa maneno ulifanikisha ushughulikiaji lengo la tatu kuhusu mbinu za kimofolojia zizingatiwazo kwenye uundaji wa anthroponimu. Kwa hivyo, mhimili huu ulifanikisha ufafanuzi wa mbinu za kimofolojia zinazohusika katika uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imewasilisha ufafanuzi wa masuala ya kimsingi yaliyouwekea utafiti huu usuli wa suala lichunguzwalo. Vipengele vilivyoelezwa ni pamoja na usuli wa utafiti unaoangazia dhana ya anthroponimu, jamii na utafiti unaohusu Kimaragoli; suala lichunguzwalo; malengo na maswali ya utafiti; misingi ya uteuzi wa mada pamoja na upeo wa utafiti. Mbali na kuueleza umuhimu wake, mihimili ya nadharia iliyoongoza ya utafiti huu pia imefafanuliwa na muhtasiri wa yaliyomo kuwasilishwa kama hitimisho la sura. Sura inayofuata inahakiki maandishi yanayohusiana na mada kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahakiki maandishi tangulizi yahusianayo na mada inayochunguzwa. Uchambuzi wa maandishi na nadharia mbalimbali zinazohusiana na nadharia ya Pragmatiki Leksia pia umefanywa. Upembuzi maandishi na kazi za wanaisimu waliotangulia uliazimia kupata taswira ya kijumla kuhusu suala la mofosemantiki kwenye taaluma ya onomastiki. Mbali na kurazinisha pengo la utafiti, uhakiki wa maandishi unadhihirisha upungufu na/au mianya ya kiakademia inayojazwa utafiti huu. Uhakiki wenyewe umetekelezwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti kwenye sehemu kama vile: uainishaji wa nomino katika vikoa maana, mofolojia ya uundaji wa anthroponimu pamoja na mabadiliko ya kisemantiki katika maneno ya lugha. Hatimaye, hitimisho la sura linawasilishwa kwa kuangazia upungufu, mianya na pengo lililojazwa na uchunguzi huu.

## 2.2 Uainishaji wa Nomino katika Vikoa Maana

Vikoa maana vimefasiliwa kwingi kuwa ni dhana katika ufafanuzi wa maana ambayo huzingatia fasili za kileksika ambazo zina karibiana kimaana (Massamba, 2004; Matinde, 2012). Kwa hivyo, vikoa maana vinajitokeza katika lugha kama vifungu cha maneno yaliyowekwa pamoja kwa kuzingatia mahusiano ya kimaana katika maneno yanayohusika. Masuala kuhusu maana aghalabu huzingatiwa katika taaluma inayojulikana kama semantiki. Hivyo basi, semantiki hutalii na kutoa ufafanuzi wa maana za maneno, sentensi, pamoja na maana kwenye matini za usemaji (Kempson, 1977). Kama chombo cha mawasiliano, lugha hutegemea ufasiri wa maana iliyofungamanishwa kwenye faridi anuwai za kisarufi ili kutimiza dhima zake.

Kwa hivyo, maana aghalabu hujitokeza kwa namna mbalimbali. Kwanza, ipo maana inayojitokeza kwenye muktadha mahususi wa mawasiliano na ambayo huchunguzwa na taaluma ya pragmatiki (Obuchi & Sangili, 2015). Aina hii ya maana huelezea alichokusudia msemaji katika mawasiliano. Pili, ni maana kileksia ambayo huakisi maana tambuzi ya kila neno kwenye mfumo wa lugha inayohusika (Odawo, 2015). Maana hii hufasiliwa na vidahizo katika kamusi za lugha anuwai na ndiyo maana tambuzi isiyobadilika. Uchunguzi huu ulizamia nomino za kawaida za Kiswahili, hususan zile zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli. Nomino zenyewe zilichanganuliwa na kufafanuliwa kwa mujibu wa maana zao kwenye miktadha ya lugha na jamii ya Wamaragoli.

Mahusiano ya kisemantiki hupelekea maneno kwenye mfumo wa lugha kuunda wavu unaotawaliwa na mahusiano ya kifahiwa (Lyons 1981). Aidha, mahusiano haya huunda vikoa maana; yaani maneno yaliyopangika katika makumbo ya maeneo au nyanja ambapo maneno hayo huwa yanahusiana kimaana. Hivyo basi, Maneno yahusianapo kwa njia tofautitofauti husababisha ukoa maana. Kimsingi, ukoa maana ni uhusiano wa kimuundo usababishao ufinyu au upana wa maana za maneno (Habwe & Karanja, 2004). Katika utafiti huu, ukoa maana ulitumika kurejelea tapo la majina lenye maana inayohusiana.

Halliday na Clemmer (1940) wanaainisha msimbo wa lugha unaotumiwa na wafungwa gerezani nchini Marekani. Msimbo wenyewe unaainishwa katika vikoa maana vya: mapenzi na ngono , sehemu za mwili, ufafanuzi wa wenzao, mihadarati na pombe, msimbo kuhusiana na jela pamoja na matusi. Msimbo wa lugha na anthroponimu ni mambo mawili tofauti, pana haja ya kuchunguza anthroponimu na kuziainisha katika vikoa ili kubaini hali ilivyo katika majina. Hata hivyo, utafiti wao ulikuza maarifa yetu kuhusu namna ambavyo maneno yanaweza kuainishwa katika vikoa maana kwani kupitia kwa maelezo yao, utafiti huu ulinufaika na maarifa yaliyopelekea uainishaji wa nomino za kawaida za Kiswahili zinazochangia uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zilizoainishwa vilevile katika vikoa maana mbalimbali.

Akitafiti kuhusu mifumo ya majina ya Kimarekani, Kipoli na Kirusi, Wierzbicka (1992) anagawa majina katika makundi mawili:- majina yanayoweza kugawika na majina yasiyogawika. Ingawa anajaribu kuyagawa majina ya watu, suala la ukoa maana halipewi kipaumbele. Ni dhahiri kwamba hakudhamiria kuyagawa katika makundi kwa kutumia maana yake; suala ambalo utafiti huu umelitalii kwa kuainisha anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili katika vikoa maana mbalimbali.

Garry (2000) anaeleza kwamba majina ndiyo kitu kimoja kilicho sawa kwa watu, wanyama, mahali na miti. Katika utafiti wake, Garry (2000) anashughulikia majina 4,500, yakiwemo majina ya watu na miti, kote ulimwenguni. Anajikita katika uchunguzi wa etimolojia ya majina hayo na kisha kuyaainisha majina hayo kwa misingi ya kijinsia. Anagundua kuwa, etimolojia inayohusishwa na jina moja inatofautiana kutoka jamii moja hadi jamii nyingine. Ingawa utafiti wa Garry unajaribu kuainisha majina, haukulenga kuainisha majina yanayohusika katika vikoa maana. Pia, utafiti wake ulilenga majina ya watu na miti, utafiti huu ulilenga anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili. Isitoshe, utafiti wa Garry haujihusishi na ulinganishi wa aina yoyote ile. Hata

hivyo, uelewa wetu kuhusu taaluma ya onomastiki, haswa uainishaji wa majina ya watu na miti ulichangiwa na utafiti huu.

Akichunguza mfanano katika utoaji wa majina ya watu katika nchi mbalimbali, Musere (2000) anasema kuwa, majina katika jamii nyingi hutolewa kwa kuzingatia siku au miezi watoto wanazaliwa. Hali hii ni dhahiri nchini Uganda, Ghana na kwingineko Afrika Magharibi. Mbiti (1991), Shilington (1995) na Sitati (2007) wanaishadidia hali hii kwa kueleza kuwa majina ya watu yanaweza hutokana na siku, wiki, mwaka, misimu, matukio fulani katika jamii, mahali alimozaliwa mtoto, tabia za anayehusika na hata sifa za kimazingira au maumbile ya mtoto anayehusika. Kazi za wataalamu hawa zilifanikisha uelewa wa misingi ya uainishaji wa athroponimu. Hata hivyo, utafiti huu ulipiga hatua zaidi ya uainishaji wa anthroponimu hizo katika vikoa maana kwa kuzichunguza zaidi na kubaini suala la mabadiliko ya kimaana pamoja na mbinu za komofolojia zinazopelekea kujengwa kwa anthroponimu zinazohusika.

Majina ya watu yanaainishwa na King'ei na Kisovi (2005) kwa kuzingatia vigezo kama vile koo ambapo mtu hupewa jina linaoonyesha amezaliwa katika familia au koo gani. Kwa mfano, *Mbaka* (ukoo wa Mbaka). Kutokana na misimu, mtoto anaweza kupewa jina linaloambatana na shughuli inayoendelea kwenye kipindi maalumu cha mwaka. Kwa mfano, *Syombua* (msimu wa mvua kwa Wakamba). Kazi, hasa wanazoshughulika nazo wazazi wa mtoto, kama vile *Mwini* (uimbaji miongoni mwa Wakamba). Wakati na mahali alipozaliwa kwa mfano, *Adhiambo* (mtoto wa kike aliyezaliwa wakati wa jioni miongoni mwa Waluo). Jina kutokana na tabia kama vile: *Mvita* (mpenda vita miongoni mwa Waswahili) na kutokana na maumbile kama vile *Mwelu* ambaye ni mweupe kama mzungu miongoni mwa Wakamba. Mengine hutokana na viongozi maarufu waliosifika katika historia, kwa mfano, *Kenyatta, Mboya, Ngei*, *Mandela* na wengineo. Utafiti huu umetofautiana na ule wa King'ei na Kisovi (2005) kwani katika utafiti wao walikuwa wanachunguza vigezo vya utoaji majina katika jamii mbalimbali ilhali, utafiti huu umeegemea zaidi katika ubainishaji wa vikoa maana katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili. Suala la vigezo vya utoaji wa majina hayo halikuchunguzwa. Hata hivyo, utafiti wao ulitueleweshа kuhusu vigezo vya uainishaji wa anthroponimu ambavyo hatimaye vilitufaa katika uainishaji wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili katika vikoa maana.

Katika uchunguzi wake wa utoaji majina miongoni mwa utamaduni wa jamii ya Akan nchini Ghana, Agyekum (2006) anayaainisha majina katika makundi matatu:- majina yanayohuhusiana na utamaduni wa jamii, falsafa za jamii, na majina yanayohusiana na mazingira. Ingawa utafiti wake ulijikita pakubwa katika kuchunguza suala la utoaji majina kitamaduni, utafiti wake ulikuza uelewa wetu wa majina kwa ujumla na hasa vigezo alivyozingatia katika uanishaji wake. Aidha, utafiti huu umetofautiana na utafiti wake kwa kupiga hatua ya kuainisha majina kiisimu na kufafanua mabadiliko ya maana katika majina hayo, swala ambalo utafiti wake haukujishughulisha nao.

Akiainisha leksimu mbalimbali za Sheng katika vikoa maana, Mugambi (2007) anafafanua kwamba leksimu za Sheng zinaweza kuainishwa katika vikoa maana kama vile mapenzi, elimu, biashara, utawala na michezo. Kwenye kikoa maana cha elimu anafasili maana ya leksimu za Sheng kama vile: *kemu, bayo, swa* na *fizo.* Leksimu hazi zinahusiana kwa sababu zinarejelea masomo tofautitofauti yafundishwayo katika shule za upili. Kwenye kikoa maana cha michezo aneleza michezo mbalimbali inayorejelewa kwa leksimu za Sheng kama vile *kagutha, voli, bake,* na *futa*. Ijapokuwa kazi ya Mugambi inajishughulisha na maana kwenye msimbo wa Sheng, suala lisilohusiana na anthroponimu, kazi hiyo ilikuwa na umuhimu mkubwa kwetu kwani ilituhami na maarifa ya kuainisha anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili kwenye vikoa maana mbalimbali.

Watoto hupewa majina kutokana na mitazamo mbalimbali kama vile kutazama nyakati za usiku, majira, sura au sifa bainifu za mtoto anayehusika (Kihore na wenzie, 2009). Kwa mfano, jina *Jamila* humaanisha sura nzuri au urembo katika jamii ya Waswahili. Wanaendelea kufafanua kuwa, mwelekeo huu unaweza pia kuwa wa mfuatano wa kuzaliwa, mfuatano wa majina ya wakwe, na matukio mbalimbali. Licha ya kufaidi maarifa kuhusu mitazamo ya utoaji wa majina ya watu kwa ujumla, utafiti wa Kihore na wenzie (2009) ulijikita katika majina ya kiasili ya jamii ili kubaini mitazamo hiyo wakati ambapo utafiti wetu ulijikita katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

Dirk (2010) anafasili vikoa maana kuwa ni jozi za maneno yenye maana zinazohusiana na ambazo maana zake hutegemeana kuwasilisha dhana ya kimuundo yenye uhalisia ndani mwake. Anatoa mfano wa matunda: maembe, machungwa na paipai. Anaendelea kufafanua kwamba hakuna kanuni ya uainishaji wa vikoa maana na kwamba mahusiano katika kila kikoa yanaweza kuibua vikoa vingine vidogo vidogo. Kwa hali hiyo, kikoa maana kinaweza

kikafasiriwa kuwa ni mchakato ya mahusiano yanayotokana na seti ya maneno na seti yenyewe aghalabu huwa kwenye kundi mahususi kimantiki. Mawazo haya yalitanua na kukuza welewa na maarifa kuhusu vikoa maana, sifa za vikoa maana na namna vinavyojengwa wakati wa uchanganuzi wa data.

Akigusia uainishaji wa anthroponimu kwenye taaluma ya onomastiki, Okal (2012) anafafanua kuwa anthroponimu zinaweza kuainishwa katika makundi mbalimbali kama vile: anthroponimu funge, anthroponimu siha, anthroponimu ya kifamilia, anthroponimu thioforiki, anthroponimu lakabu, apotropiki, teknonimu, paidinimu, animonimu, aptronimu, matronimu na patronimiki. Uanishaji huu ulichangia kukuza maarifa yetu kuhusu taaluma ya onomastiki, hasa tawi la anthroponomastiki linalochunguza majina ya watu. Hili lilituhami na maarifa ya kuainisha majina kwa ujumla. Hatimaye, anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida ziliainishwa kwa mujibu wa vikoa maana vinavyohusika.

Mahusiano ya vikoa vya maana yamefasiliwa kwingi kuwa ni uhusiano wa kimuundo wenye ufinyu au upana wa maana ambapo neno moja aghalabu hutumika kwenye mfumo wa lugha fulani kutajia dhana au kitu kinachotajwa kwa maneno mawili au zaidi kwenye mfumo wa lugha nyingine (Trier, 1934; Nida, 1964; Palmer, 1981; Matinde, 2012). Mifano kadha ya vikoa maana inatolewa kwenye mifumo ya lugha mbalimbali. Mathalan, lugha ya Kimeksiko inayo maneno sita yanayorejelea dhana ya *kelele*; watoto wanapolia, watu wanapoongea kwa sauti ya juu, watu wakijadiliana, watu wanapozungumza kwa hasira, makelele ya kuongezeka na makelele kwenye msiba. Neno katika kikoa maana fulani aghalabu huwa na uhusiano na neno lingine kwenye kikoa maana kinachohusika. Kwa mfano, neno 'nyumba' katika Kiswahili linao uhusiano msonge na maneno kama vile pembe, ghorofa, n.k. Ingawa wataalamu hawa wameshughulikia maneno ya Kiswahili, hawakujishughulisha na suala la ubainishaji wa nomino za kawaida zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli katika vikoa maana. hata hivyo, mifano yao iliupa utafiti mwanga katika mchakato wa uanishaji wa nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli katika vikoa maana.

Wakijadili aina za majina wanayopewa watoto katika jamii, Odesanya na wenzie (2017) wanasema kuwa mtoto anaweza kupewa jina kulingana na yaliyompata mama wakati wa kuilea mimba, baada ya kujifungua au kutokana na ramli iliyopigwa. Uchunguzi huu unaoegemea utoaji wa majina kwa watoto unasawiri mielekeo miwili inayosababisha matapo

makuu ya majina: majina yanayohusiana na ujauzito na majina yanayohusiana na upigaji ramli. Ingawa utafiti wetu ulichukuwa mkondo wa kisemantiki, utafiti wao ulitufaa katika kuelewa misingi mingineyo ya uanishaji majina.

Akichanganua agoti inavyotumika miongoni mwa wafungwa, Okoth (2019) anainisha agoti kwenye vikoa maana anuwai. Agoti za wafungwa zinaanishwa kwenye vikoa maana kama vile: kikoa cha mahusiano ya kimapenzi kinachojumuisha agoti ya *maua* (inayorejelea mfungwa atekelezaye dhima za mke kwenye uhusiano wa kimapenzi gerezani), *mende (*mfungwa mwenye jukumu la mume kwenye uhusiano wa kimapenzi gerezani), *gundu (*kisirani kinachohusishwa na mfungwa baada ya ngono gerezani), *marufuku* (mfungwa mwenye wapenzi wengi gerezani) pamoja na *malaya* (mfungwa msaliti anayefichua siri kwa maafisa wa polisi) n.k. Utafiti huu unainisha vikoa zaidi vya agoti za wafungwa kama kikoa cha marufuku na dawa za kulevya kama vile:- *gife, godee, gari, simu, unga, wembe, redio* nk. Kikoa cha wafungwa wa magereza hasa *mashujaa, kairo, nyoka, trekta, warogoti, mwewe* nk na kikoa cha maafisa wa magereza k.v *gavaa*, *malilio*, *mzazi*, *mastone*, *uzi tatu*, *uzi mbili,* n.k. Utafiti wa Okoth uliimarisha na kutanua uelewa wa utafiti huu kuhusu uanishaji wa vikoa maana. Hata hivyo, ulitofautiana pakubwa ambapo wakati Okoth anachanganua agoti za wafungwa utafiti huu ulilenga anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili.

Ni dhahiri kuwa kuna upungufu wa tafiti zilizofanywa kuhusu ubainishaji wa nomino za kawaida za Kiswahili zinazotumika kujenga anthroponimu katika lugha nyingine hasa Kimaragoli na kuziainisha katika vikoa maana. Nyingi katika tafiti zilizofanywa zimechunguza majina kitamaduni huku zikishughulikia sana suala la utoaji wa majina hali iliyochochea haja ya kuainisha majina kiisimu kwa kuzingatia nadharia ya isimu ili kukuza taaluma ya isimu haswa onomastiki. Wakati huo huo ni muhali kupata utafiti uliochunguza anthroponimu zinazojengwa kwa nomino za Kiswahili katika jamii yoyote hali iliyorazinisha zaidi pengo la kiakademia ambalo utafiti huu ulinuia kulijaza. Japo kuna nomino za aina mbalimbali za Kiswahili kama vile, za pekee, kawaida, mguso, dhahania, jamii au jumuishi, kitenzi jina, zinazohesabika na zisizohesabika (Kihore na wenzake, 2009), utafiti huu ulijishughulisha tu na nomino za kawaida za Kiswahili zinazotumika katika ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli. Mifano ya nomino hizo za kawaida za Kiswahili ni kama vile: sahani, kikombe, meza, makate, dawati, kalamu, kiti na kadhalika.

**2.3 Mofolojia ya Uundaji wa Anthroponimu**

Uundaji wa maneno huchanganuliwa katika kiwango cha isimu kijulikanacho kama mofolojia. Mofolojia ni tawi la isimu linalochunguza muundo wa maneno na michakato ya uundaji wa maneno hayo (Yarlesis na wenzake, 2009). Taaluma ya mofolojia inaweza kugawanywa katika matawi mawili: yaani mofolojia ya uundaji wa maneno na mofolojia ya minyambuliko ya maneno (Katamba, 1993; Massamba, 2004). Utafiti huu umejikita katika mofolojia ya uundaji wa maneno. Kama ilivyodokezwa awali, nadharia ya Pragmatiki Leksika pia hujishughulisha na uundaji wa maneno katika kitengo cha upanuzi wa maana (Wilson, 2003). Pamoja na kuchangia nadharia Pragmatiki Leksika data zaidi, ufafanuzi wa anthroponimu za Kimaragoli pia unatanua wigo wa maarifa kuhusiana na michakato ya kiakili na mbinu zinazopelekea maumbo hayo kupatikana. Leksia huashiria umbo lenye maana msingi kama vile kitenzi au nomino (Buliba, Njogu & Mwihaki, 2006). Utafti huu unachunguza mbinu zinazopelekea kuundwa kwa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

Buren (1977) anatafitia muundo wa majina ya kike ambayo hubuniwa kwa kutumia mbinu ya muundo nyuma kwa mfano, majina kama *Beck* kutokana na *Becky, Pen* kutokana na *Penny* au *Deb* kutokana na *Debbie* n.k. Anagundua kuwa, uundaji huu hudhihirisha uchangamfu mwema wa kibinafsi na uhusiano maalum katika mahusiano ya kawaida ya watu wanaojitambulisha. Pia, anabainisha kuwa, kwa kutumia muundo huu wa -ie- au -y- huonekana kama wenye dhana ya kitoto na kwa hivyo hutumia muundo maalumu kama uhusiano wao ulivyo maalumu. Buren anagundua kuwa, katika shule za upili wasichana wanaweza kuita rafiki zao kwa mtindo huo kama vile *Lydia - Lyd, Jackie - Jaq, Alison -Al, Debbie - Deb* n.k. Hata hivyo, walimu wao hawawezi kuwaita wakirejelea vifupisho vya majina yao kutokana na tofauti katika mahusiano yao. Ingawa Buren alichunguza mofolojia ya majina ya kike kwa kuangazia ukatwaji wake pamoja na mahusiano yaliyopo baina ya wahusika, utafiti wake unatofautiani pakubwa na utafiti huu. hata alijikita. Utafiti wa Buren haujishughulishi na mbinu za kimofolojia zinazopelekea uundwaji wa majina hayo; suala ambalo linapewa kipaumbele kwenye uchunguzi huu.

Kwa mujibu wa Wierzibickar (1992) kimuundo, majina huwasilisha dhana ya udogo iwapo mzizi wa jina linahusika unaishia kwa herufi (r) ambapo kiishio *-k-* na *-ok-* hutumika kuonyesha dhana ya udogo. Mifano ya majina kama vile Mark - Marik, Sora - Sorik, Jura – Jurik, n.k. inachanganuliwa. Pamoja na kuonyesha hali ya udogo, kiambishi *-k-* hutumiwa katika lugha nyingi kuonyesha dharau au dhana ya kupuuza na kukashifu kwa kupunguzia

hadhi ya anayerejelewa. Anaendelea kusema kuwa, majina yenye kiambishi hiki hutumiwa hasa na watu wazima kuwarejelea watoto au watoto kwa watoto wenyewe na vilevile miongoni mwa vijana. Kwa Warusi kiishio hiki hutumiwa kwa watu wa hadhi ya chini kama vile wakulima. Matumizi yake baina ya vijana, watu wazima na wachanga ni kuleta dhana ya uelewano, kutaniana na kukuza umoja. Hata hivyo, yapo majina mengine ambayo ingawa yanaambishwa *-uska-* ya udogo bado huonyesha dhana ya kuthaminiwa badala ya ukubwa kwa mfano, Vera - Veruska au Andre - Andrejuska. Wiezibickar anaendelea kudai kuwa baadhi ya majina huwa na viishio vya udogo lakini dhana yenyewe ijitokezayo si ya udogo bali ni ya mahaba na utunzaji. Dhana hii inalinganishwa na hali ambapo mtoto hulinganishwa na kikembe kumaanishwa anapendwa. Ingawa utafiti huo ulichunguza mofolojia, uliegemea katika mofolojia ya uambishaji; hali inayoutofautisha utafiti huo na utafiti huu kwani utafiti huu umeshughulikia mofolojia ya uundaji wa majina, haswa mbinu mbalimbali za kimofolojia zinazopelekea kuundwa kwa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

Oduyoye (1982) na Essien (2000) walichunguza miundo ya majina ya Ibibo, Igbo na Yoruba mtawalia. Matokeo ya tafiti zao yanaonyesha kwamba majina ya watu katika jamii hizo yanaakisi sarufi ya lugha za jamii hizi. Wanasema kuwa majina ya watu hujumuisha aina za maneno ambayo yana maana na yanayodhihirisha maumbo mbalimbali katika kuwasilisha maana hizo. Katika tafiti zao, wataalam hawa hawajishughulishi na mabadiliko ya maana. Hata hivyo, mwelekeo waliochukua kuhusu mofolojia ni tofauti na ule unauchukuliwa hapa kwa sababu katika kazi zao hawakujishughulisha na mbinu za kimofolojia zinazopelekea kuundwa kwa majina hayo. Vinginevyo, tafiti zao zilichangia welewa kuhusu uchanganuzi wa majina ya watu kimofolojia. Rubanza (2000) alifanya utafiti linganishi wa majina ya watu katika jamii ya Kihaya na jamii ya Yoruba. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwa ingawa tamaduni za jamii hizi mbili zitofautiana, ruwaza za utoaji majina katika jamii hizi mbili ulifanana sana, majina yote yalichukuwa viambishi linganifu vya kijinsia. Utafiti wake ulichangia welewa na uimarishaji wa maarifa kuhusu mofolojia ya uambishaji wa majina ya watu. Hata hivyo, utafiti huu ulipiga hatua na kuchunguza mofolojia ya uundaji wa majina hayo; suala ambalo halikushughulikiwa katika utafiti wake. Pia, utafiti ulijikita katika kutafitia anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino ya kawaida za Kiswahili wala haujalinganisha majina hayo na ya jamii nyingine.

Mwangi (2015) na Lupenga (2006) wanachunguza mofolojia ya majina ya Kiyoruba na Gikuyu mtawalia wakiongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksia. Matokeo ya tafiti zao

yanaonesha kwamba majina katika jamii hizi yanaakisi sarufi ya lugha za jamii hizi. Kwa mfano: mofu {*ku-*} ikiongezwa kwenye mzizi *-guru* panapatikana jina *Kuguru* lenye maana ya mguu, mofimu {*mu*} ikipachikwa kwenye mzizi *-tundu* jina *Mutundu*. Tafiti zao ziliufaa utafiti huu kuelewa namna nadharia ya kiisimu inaweza kutumiwa kuchunguza majina. Hata hivyo, utafiti huu unachunguza maana kimuktadha, mbinu za kimofolojia zinazopelekea majina hayo kuundwa katika lugha na mabadiliko ya kimaana katika majina hayo. Vipengele hivi havijashughulikiwa katika kazi zo. Isitoshe, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Pragmatiki Leksia.

Katika utafiti wake wa mofosintaksia ya majina ya Kikristo ya kisasa ya jamii ya Ewe, Kongo (2016) anagundua kuwa majina anayochunguza yanaweza kuchanganuliwa katika mofu ambazo zina maana. Utafiti wake unaweka wazi miundo mbalimbali ya majina ya kisasa ya Kikristo. Yaani, majina ambayo hayawezi kugawika katika mofu zake, yale ambayo yana mofu mbili na yale ambayo yana mofu nyingi. Ingawa utafiti huu haukujihusisha na majina ya Kikristo katika jamii ya Wamaragoli, utafiti wake unasaidia katika ushughulikiaji wa mofolojia ya majina ya watu kwa ujumla. Hata hivyo, kipengele cha kiisimu cha sintaksia hakikuchunguzwa umeegemea kwenye mofolojia na semantiki katika uchunguzi wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

Pamoja na tafiti hizi, imethibitika kwamba ni muhali kupata utafiti unaozamia anthroponimu za Wamaragoli. Mathalani, Anindo (2016) anachunguza mofosemantiki ya majina ya mahali katika jamii ya Wamaragoli. Anagundua kuwa pahali panaweza kupewa jina kutokana na vigezo mbalimbali kama vile, kutokana na mtu maarufu, miti mikubwa, shughuli za kijamii, mimea fulani, na kadhalika. Ingawa anagundua pia majina hayo yana maana, hajishughulishi na mabadiliko ya maana katika majina hayo ya mahali. Pia, anapofafanua mofolojia hajishughulishia na mbinu za kimofolojia zinazopelekea kuundwa kwa majina hayo ya mahali; hali inayobainisha pengo linaloshughulikiwa katika utafiti huu.

Kwa upande wake, Malande (2011) anachanganua maana ishara katika majina ya Wamaragoli huku akiongozwa na nadharia ya Semiotiki. Utafiti wake unabaini kuwa kuna maana halisi na maana husishi katika majina hayo. Ingawa utafiti wake ulitufaa kuelewa jamii hii ya utafiti na maana ishara katika majina yao, utafiti huu unatofautiana na utafiti wake kwa vile utafiti huu unaainisha majina hayo katika vikoa maana, kuchunguza mabadiliko ya maana katika majina hayo na kufafanua mbinu za kimofolojia zinazopelekea kuundwa kwa majina hayo; masuala ambayo utafiti wake haujishughulishi nayo.

### 2.3.1 Mbinu za Kimofolojia za Uundaji wa Anthroponimu

Uundaji wa anthroponimu za Wamaragoli unachukuliwa kuwa na uhusiano wa karibu sana na uundaji wa maneno katika jamii nyinginezo kwani anthroponimu zimefafanuliwa na wataalam kama aina za nomino; nomino za pekee (Kapinga, 1983, Habwe & Karanja 2004, Saluhaya, 2010). Uundaji wa maneno katika lugha hufanyika kwa kutumia mbinu tofauti tofauti, kila mbinu hutegemea kanuni maalumu zinazotumika kuzalisha maumbo ya maneno yenye sifa zinatofautiana. Uzalishaji wa maneno mapya hutegemea mbinu kama vile unyambulishaji, mwambatano, ukopaji, ufupishaji, akronimu, uhulutishaji na mbinu ya kubuni (Temu, 1984, Mdee, 1986 na Shitemi, 2011). Akishadidia wazo hili Jefwa (2010) anafasili uundaji wa maneno kuwa ni uambatanishaji wa mofimu moja au zaidi kufikia kiwango cha mofimu hiyo au hizo kuleta maana kileksika katika lugha yoyote ile. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, mbinu za kimofolojia zitumikazo katika uundaji wa maneno ni pamoja na: unominishaji, ukopaji, utohozi, uhulutishaji, akronimu, uambatishaji, uambishaji, uradidi, ubunaji, ufupishaji na kadhalika.

#### 2.3.1.1 Ukopaji

Ukopaji ni utaratibu wa kuchukua maneno kutoka lugha chanzi hadi katika lugha lengwa (Massamba, 2004). Huu ni utaratibu inaojumuisha uhamishaji wa kipashio fulani kutoka lugha moja na kukiingiza kwenye mfumo wa lugha nyingine. Kwa hali hivyo, huwa kuna aghalabu lugha changizi na lugha pokezi (Jefwa, 2010). Ukopaji ni uhamishaji wa leksimu mahususi, seti ya leksimu au faridi fulani kutoka lugha moja au lahaja moja hadi nyingine. Kuna aina mbili za ukopaji: ukopaji sisisi na ukopaji tohozi. Ukopaji sisisi ni pale ambapo leksimu fulani inahamishwa kutoka katika lugha changizi hadi lugha lengwa bila ya kufanyiwa marekebisho yoyote. Mathalan, nomino ‘ugali’ na ‘safari’ zimekopwa kisisisi na kuingizwa kwenye mfumo wa Kiingereza jinsi zilivyo bila kubadilisha maumbo. Poplack (1988) anahoji kuwa nomino ndizo aghalabu hukopwa kwa mbinu hii. Maneno yanaweza kukopwa kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza au kutoka lugha ya Kiingereza hadi katika lugha ya Kiswahili. Katika mbinu ya ukopaji tohozi, maneno huchukuliwa kutoka kwa lugha ya kigeni au lugha nyingine na kuingizwa kwa mfumo wa lugha inayolengwa ili yaafiki kanuni za kifonolojia na kimofolojia. Mifano ya aina hii *bank - benki, change - chenji, atlas – atlasi,* n.k. (Brynon, 1977 na Campbell, 1998).

Brynon (1977) na Campbell (1977) wanaainisha kategoria mbili za ukopaji: ukopaji utohozi na ukopaji sisi. Wanaeleza kuwa katika ukopaji utohozi, maneno kutoka lugha kopeshi hunukuliwa kwa kuzingatia mfumo wa kiisimu wa lugha pokezi ilhali kukopa sisisi ni

ukopaji wa moja kwa moja; mbinu hii huchukua maneno jinsi yalivyo katika lugha kopeshi na kuyatumia jinsi yalivyo katika lugha pokezi. Utohozi husababisha: upanuzi maana, ufinyizi wa maana, uimarikaji maana, udhalililikaji wa maana, tasfida na usogezi maana. Upanuzi wa maana hutokea pale ambapo maana za maneno huongezeka ili kutumika katika miktadha mingi ya mawasiliano kuliko ilivyokuwa awali. Ufinyizi wa maana nao huwa kinyume cha upanuzi; miktadha ya matumizi ya neno linalohusika hupunguka. Uimarikaji wa maana hutokea pale ambapo maneno yaliyokuwa yamekataliwa na jamii kwa sababu za kitamaduni hukubalika na kuanza kutumika. Haya hutokea kupitia ama mabadiliko ya kisaikolojia au ya mpito wa wakati. Udhalilikaji wa maana nao ni kinyume cha uimarikaji; kudhoofika kwa maana ya maneno hutokea kwa sababu za kitamaduni. Kuyatamka maneno haya aghalabu huwa ni mwiko (Crowley, 1992; Campbell, 1998).

Crowley (1992) na Campbell (1998) wanaendea kusema kuwa, kila jamii huwa na vigezo vya utamaduni na miiko ambayo huelekeza na kuendesha matumizi ya lugha. Vigezo hivi vya kitamaduni katika mawasiliano ni tasfida. Utaratibu wa usogezi wa maana hutokea pale ambapo maana ya neno hujongezwa katika lugha pokezi. Mbinu kadha hutumika kufafanua usogezi maana – sitiari, metonimu na sinedochi. Sitiari hutumika kuonyesha uhusiano wa kimaana kwa mujibu wa matumizi yake huku metonimu ikifafanua mabadiliko ya maana inapopanuka na kuhusisha maana zingine. Sinedochi ni pale ambapo sehemu ndogo ya dhana hutumika kuwasilisha sehemu kubwa. Mawazo ya wataalamu wa mbinu hii yalitanua maarifa ambayo yalisaidia utafiti huu kuchanganua mbinu hii ya kimofolojia namna inavyopelekea kuunda anthroponimu za Wamaragoli.

#### 2.3.1.2 Mwambatano

Mwambatano ni mbinu ya kuunda maneno kwa kuunganisha maneno mawili au zaidi ambayo kwingineko yanaweza yakajisimamia kama maneno huru kutengeneza neno moja (Mrikaria, 2004; Libben 2006). Nenounde huitwa neno ambatani (Mdee 1986; Wesani-Chomi, 2003). Mbinu ya mwambatano huunda maneno yenye ruwaza mahususi (Frawley, 2003). Vijenzi vyake vikipanguliwa, maana ya neno linalohusika hubadilika kabisa. Hii ina maana kuwa neno kama *askarijela* likipanguliwa na kuwa **jelaaskari,* litapoteza maana asilia. Neno ambatani hujengwa kwa maneno mengi yanayofanya kazi kama neno moja (Mdee 1986; Kahigi, 2007). Mdee (ameshatajwa) anabainisha vigezo vifuatavyo kutambua neno ambatani:

(a) Maana ya neno ambatani si jumla ya maana ya vijenzi vinavyohusika moja kwa moja. Kwa mfano: *kifunguakinywa* ni staftahi.

(b) Vijenzi vya maneno haviwezi kubadilishwa pasipo kuathiri maana yake. Kwa mfano: Kifunguakinywa -**kifunguamdomo*

(c) Neno linaweza kuwa na sinonimu moja ambayo inaweza kuwa halisi au inayokaribiana. Kwa mfano: *mwananchi = mzalendo*

(d) Neno linaweza kuwa na kisawe cha neno moja katika lugha nyingine. Kwa mfano: *Mrejeosabaki- anaphora (kiingereza)*

Wesani-Chomi (ameshatajwa) anaeleza kuwa mwambatano ni mbinu mojawapo ya kuunda nomino ambatano ambapo kategoria mbalimbali za maneno yanahusika kama vijenzi; si nomino pekee. Mawazo haya yalifaidi utafiti huu kwani ndiyo yaliupa msingi wa kuchanganua namna anthroponimu za Wamaragoli zilivyoambatishwa.

#### 2.3.1.3 Unyambulishaji

Unyambulishaji ni aina ya uambishaji unaohusika na uundaji wa maneno katika lugha ambapo viambishi mbalimbali vinaongezwa kwenye mzizi wa neno ili kupata neno jipya ambalo si lazima liwe la kategoria moja na lile la awali (Katamba 1993; Kihore, Massamba & Msanjila, 2004). Mifano ya uundaji maneno wa aina hii ni :

*Enda →mwendo, Mwenda, kwenda*
*Imba → wimbo, mwimbaji, uimbaji, mwimbiwa*
*Safiri→ safari, msafiri, kusafiri, usafirishaji, msafirishaji.*

Anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili zinadhihirisha uundwaji kupitia mbinu hii. Mawazo ya wataalamu hawa yalikuza elewa katika utafiti huu ya namna ya kutenga viambishi mbalimbali na kutambua namna anthroponimu za Wamaragoli zinavyonyambuliwa.

#### 2.3.1.4 Ufupishaji

Ufupishaji ni mbinu inayotumiwa katika uundaji wa maneno kwa kupunguza kundi la maneno au neno ili kupata neno moja. Uundaji wa maneno kwa hii unaweza kugawanywa katika kategoria tatu. Yaani, uhulutishaji, akronimu na ufupishaji-mkato (Kiango, 2004; Kahigi, 2007). Kila mojawapo ya mbinu hizi hudhihirisha taratibu mahususi.

##### 2.3.1.4.1 Akronimu

Mbinu ya akronimu hutumia herufi au silabi za mwanzo za maneno katika kuunda neno jipya (Kiango, 2004; Mohochi, 2005). Wanafafanua kuwa dhana inayowakilishwa na mlolongo mrefu wa maneno inakuwa rahisi kutajwa kwa kutumia neno moja lililofupishwa. Njia hii husaidia kuleta mkato wa kuwasilisha dhana katika maandishi na mazungumzo. Kwa mfano,

badala ya *Baraza la Kiswahili la Taifa*, kifupisho *BAKITA* kinaundwa kuwakilisha dhana nzima. Akronimu huainishwa kulingana na namna zinavyotamkwa. Wataalamu hawaafikiani kuhusu mipaka ya neno liundwalo kwa akronimu. Baadhi ya kamusi kama vile *Cambridge Advanced Learner's Dictionary* toleo la tatu na *The Oxford American Dictionary* toleo la pili husisitiza kuwa akronimu sharti zitamkike kama maneno, yaani vifupisho/alfabeti, haviwezi kuitwa akronimu. Wataalamu wengine hutambua aina zote mbili za vifupisho kama akronimu. Kuna aina mbili kuu za akronimu katika mfumo wa lugha ya Kiswahili. Kwanza, akronimu zinazotamkwa kama maneno. Kwa mfano:

| **Akronimu** | **Maelezo** |
|---|---|
| Ukimwi | ***U**pungufu wa **ki**nga **mwi**lini* |
| TUKI | ***T**aasisi ya **u**chunguzi ya **Ki**swahili* |
| FOKISA | ***Fo**nolojia ya **Ki**swahili **Sa**nifu* |

Hata hivyo, baadhi ya vifupisho hivi hutamkwa kama neno au herufi mojamoja kutegemea mtumiaji na muktadha.

Pili, kuna akronimu zinazotamkwa kama herufi moja kwa moja. Kwa mfano:

| **Akronimu** | **Maelezo** | **Chanzo** |
|---|---|---|
| KV | ***K**onsonanti **V**okali* | Massamba (2004) |
| VVU | ***V**irusi **V**ya **U**kimwi* | TUKI (2004) |

Mawazo haya yaliunufaisha utafiti huu kwani yalielezeka namna ufupishaji unavyoweza kutokea. Hali hii ilikuza maarifa yetu kuhusu mbinu hii hali iliyosaidia utafiti huu kuchanganua mbinu hii inavyopelekea kuunda anthroponimu za Wamaragoli.

#### 2.3.1.4.2 Ufupishaji-Mkato

Ufupishaji-mkato au utemaji ni mbinu ya kufupisha maneno kwa kudondoa baadhi ya silabi au sehemu mojawapo ya neno (Mcarthur, 1998). Kuna aina nne za udondoshaji. Tazama Jedwali 2.1 hapa chini kwa mifamo:

**Jedwali 2.1 Aina za Udondoshaji katika Ufupisho-Mkato**


| **Na** | **Aina** | **Sehemu** | **Mifano** |
|---|---|---|---|
| 1) | Udondoshaji tamati | Mwisho wa neno | Bi (Bibi), Eka (Ekari) |
| 2) | Udondoshaji mwanzo | Mwanzo wa neno | Mapambazuko (Pambazuko) |
| 3) | Udondoshaji kati | Katikati ya neno | Choko (Chokoro), Fungutenzi (Fungukitenzi) |
| 4) | Udondoshaji changamani | Sehemu kadhaa, hasa za maneno ambatani | Bwanamkubwa (Bwamkubwa) |

**Chanzo: TUKI (2004)**

Kwa mujibu wa Jedwali 2.1 hapo juu, mbinu hii husaidia kuunda maneno yaliyo rahisi kutamkwa na kuandika baada ya sehemu fulani kudondoshwa.

**2.3.1.4.3 Uhulutishaji**

Uhulutishaji pia huitwa ufupisho-mchanganyiko (Kiango, 2004). Uhulutishaji ni mojawapo ya mbinu tatu za kuunda maneno kwa kufupisha kikundi cha maneno ili kupata neno moja jipya. Uhulutishaji ni mbinu iunganishayo vipashio vya maneno tofautitofauti yaliyo katika fungu la maneno ili kuunda neno moja jipya. Dhana inayobebwa na nenounde aghalabu huwa changamano (Kahigi, 2007). Vijisehemu vinavyohusika si lazima vijisimamie kama maneno kamili au mofimu kamili kama ilivyo katika mbinu ya mwambatano na unyambulishaji mtawalia. Hata hivyo, kuna uwezekano wa vipashio vinavyounganishwa kuwa mashina kamili. Tazama mifano miwili katika Kielelezo 2.1 kifuatacho:




**Kielelezo 2.1 Uundaji Maneno kwa Mbinu ya Uhulutishaji**

Katika mfano (a) {cha} ni mofu ilhali [mcha] si mofu. Katika mfano (b) vijenzi vyote ni mofu. Utaratibu unaotumika kuunda maneno ya aina hii hudhihirisha kukosekana kwa mantiki au ruwaza maalum. Hakuna kanuni zinazobainika zinazoongoza katika uteuzi au kutabiri kijisehemu kitakachoteuliwa katika kuunda neno. Kwa mfano:

**Kidu**du + su**kari** → kidukari

**Kiua** + wa**dudu** → kiuadudu

(Kiango, 2004)

Uafiti huu ulinufaika na mawazo haya kwamba yalikuza elewa yetu kuhusu namna mofimu mbalimbali zinavyohulutishwa na kutengeneza neno hali ambayo ilirahisisha utambuzi na uchanganuzi wa mbinu hii katika anthroponimu za Wamaragoli.

#### 2.3.1.5 Uradidi

Mbinu ya uradidi pia hujulikana kama urudufishaji wa maneno (Mrikaria, 2004) au takriri (Kiango, 2004). Uradidi ni utaratibu utumikao katika lugha ambapo sehemu ya neno au hata neno lote hurudiwa ili kuunda neno jipya au kuongeza maana ya kisarufi (Frawley, 2003; Massamba, 2004). Katika uradidi, silabi, mofimu, sehemu ya neno lote hurudiwa mara mbili au zaidi. Sehemu au kipashio kinachorudiwa si lazima kiwe silabi au mofimu kamili (Katamba, 1993). Katika lugha nyingi, ikiwemo lugha ya Kiswahili, kuna uradidi kamili na uradidi nusu. Uradidi kamili ni pale ambapo neno zima hurudiwa mara moja au zaidi. Uradidi nusu ni ambapo sehemu tu ya neno hurudiwa (Massamba, 2004). Mifano ya uradidi kamili :

tinga → Tingatinga
wazi → Waziwazi
tofauti → Tofautitofauti

Mifano ya uradidi nusu:

peta → pepeta
zote → zozote

Kiradidiwa kinaweza kupachikwa kutoka upande wa kushoto au upande wa kulia wa shina. Mara nyingi uradidi unaokopa sehemu ya mwanzo wa shina huchukua mwelekeo wa kushoto - kulia na ule ambao huchukua sehemu ya mwisho ya shina huchukua mwelekeo wa kulia - kushoto (Katamba, 2004).

Aidha, uradidi huhusisha vipengele vya kifonolojia vinavyohusu konsonanti na vokali pamoja na vipengele vya kiarudhi. Kwa mfano, mbinu ya onomatopoeia, yaani tanakali ya sauti huhusisha midundo, miigo au tanakali ya sauti fulani. Katika mfumo wa Kiswahili, maneno yanayoundwa kwa utaratibu huu ni kama *shaghala-baghala*, *kinaga -ubaga*, *pikipiki* nk. Uradidi huibua na hupelekea kubadilika kwa maana ya maneno yanayohusika (Frawley, 2003). Kauli hii inaonyesha kuwa ingawa uradidi ni mbinu muhimu katika uundaji wa maneno mbalimbali katika lugha, maana ya maneno hayo yanaeleweka zaidi katika muktadha wa matumizi unapotiliwa maanani. Mawazo ya wataalamu wa mbinu hii yalikuwa muhimu katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu kwani yalitupa msingi na vilevile kukuza kwa undani elewa yetu kuhusu mbinu hii.

#### 2.3.1.6 Ubunaji

Mbinu hii hupelekea uundaji au uvumbuzi wa neno jipya kabisa ambalo halikuwa katika matumizi ya lugha inayohusika. Nenounde hatimaye hupachikwa maana. Mara nyingi ubunaji unapofanywa maneno yanayoundwa yanafaa kushabihiana au kuingiliana na masuala ya kifonolojia na kimofolojia ya lugha inayohusika. Zipo njia mbili za kubuni msamiati mpya. Kuna njia kubuni kinasibu pamoja na kubuni kwa kuhusisha kiashiriwa na sifa maalum kama umbo, tabia au matumizi.

##### 2.3.1.6.1 Kubuni Kinasibu

Katika ubunaji kinasibu, maneno mapya huundwa kwa kuzingatia kanuni za kiisimu za lugha inayohusika na kisha kuyapachikia dhana mbalimbali. Mwanalugha ana uhuru wa kuunda umbo lolote japo analazimika kutia maanani muundo wa lugha inayohusika kifonolojia. Kwa mfano, katika Kiswahili sharti atumie muundo wa silabi unaokubalika ili nenounde likubalike kama neno la Kiswahili. Uhuru alionao muundamaneno haumruhusu kuunda maneno kama **kxayart au *yapkaaty*, ambayo hayana muundo wa Kiswahili.

Kazi hii ya uundaji maneno kinasibu inaweza kufanywa kiurahisi kwa kutumia programu za kompyuta (Mdee, 1986). Utumiaji wa tarakilishi husaidia kutatua tatizo la kuchukua maneno ambayo tayari yamo katika lugha na kuyashindilia mzigo mwingine. Maneno yanayoundwa kinasibu huwa na ubuye unaoletwa na kukosa kuhusisha na nenounde na sifa za kiashiriwa. Mifano wa maneno ya Kiswahili yaliyoundwa kupitia mbinu hii ni pamoja na: golo - *solar system*, nasidi - *configure*, n.k. Mawazo ya Mdee (1986) yalikuza welewa wetu kuhusu mbinu za kimofolojia za uundaji maneno.

##### 2.3.1.6.2 Uhusishaji

Hapa utaratibu wa kubuni huongozwa na vigezo maalum kama vile sifa za kimaumbile, tabia au matumizi ya kitu kiashiriwa. Sifa hizi zinaangaliwa na kisha kubuni neno linalozingatia mojawapo ya sifa zinazohusika (Kiango, 2004). Anafafanua aina za uhusishaji kwa kuzingatia sifa kama vile maumbile, tabia na matumizi.

Sifa za kimaumbile zinafafanuliwa kuhusisha namna kitu kilivyoundwa au kinavyoonekana. Sifa ya dhana iliyoundiwa neno inatumiwa kama msingi wa kubuni msamiati mpya. Kwa mfano, neno *kipanya* lilibuniwa kuashiria kifaa katika tarakilishi kinachofanana na mnyama mdogo anayeitwa panya. Nalo neno ‘ndege’ yaani, chombo cha angani, lilihusishwa na sifa za ndege ambaye ni mnyama, yaani nyuni.

Katika kuzingatia sifa za kitabia, neno hubuniwa kwa kuzingatia tabia au hulka za kitajwa. Kwa mfano, katika kubuni neno *garimoshi* sifa ya kutoa moshi mwingi ilizingatiwa nalo neno *kifauwongo*, sifa ya mnyama kujifanya amekufa na mmea kujifanya umenyauka unapoguswa ilizingatiwa.

Kwa kurejelea sifa za kimatumizi, neno hubuniwa kwa kuhusisha dhana na matumizi yake moja kwa moja. Mbinu hii ni zalishi katika kuunda maneno. Kwa mfano, kipimamvua ni kifaa cha kisayansi cha kupima kiasi cha mvua. Kuna maneno kadhaa ambayo yameundwa kwa kuzingatia utaratibu huu, nayo ni pamoja na: *kionambali, kipimajoto, kipimahewa, kirekodisauti, kitambulisho,* n.k maneno haya yanaashiria matumizi ya kifaa kinachohusika.

Maneno yanayobuniwa kwa uhusishaji yanaibua hisia fulani kwa watumiaji na mara nyingi huwa angavu kwa kutoa fununu ya maana ya kiashiriwa (Kiango, 2004). Maneno hayo basi yanakuwa rahisi kukubalika na wazungumzaji wa lugha husika. Kutokana na maelezo haya, utafiti huu ulipata msingi wa kuchanganua mbinu hii namna inavyopelekea uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli. Mawazo haya yalitufaa katika kutambua aina mbalimbali za uhusishaji na namna unavyoweza kujitokeza.

#### 2.3.1.7 Uhamishaji Maana

Uhamishaji maana pia huitwa upanuzi wa maana au uwasilishaji. Neno ambalo tayari linatumiwa katika lugha hupewa maana mpya katika muktadha wa matumizi. Neno linapanuliwa kimaana na kutumiwa kuwakilisha dhana nyingine mpya kabisa. Massamba (2004) anasema kuwa huu ni utaratibu wa uundaji wa maneno kwa namna ambayo neno ambalo lilikuwa na uamilifu A huchukua uamilifu B bila kubadili umbo lake. Kwa mfano, neno ambalo kimsingi huwa kitenzi linabadilika na kuwa kivumishi bila kubadilisha umbo lake. Bauer (1983) na Katamba (1993) wanasema kuwa ni unyambulishaji ambao neno hubadilisha kategoria bila kuongeza kiambishi chochote au kubadilisha umbo lake. Kwa mfano, neno ambalo kimsingi huwa kitenzi linabadilishwa na kuwa nomino, au nomino kuwa kivumishi bila kubadilisha umbo lake. Uchaguzi wa maneno haya si wa bahati nasibu; maneno yachaguliwayo huibua fikra au dhana fulani (Kiango, 2004). Uhamishaji maana ni njia ya kuchukua neno lililo katika kategoria moja na kuunda neno au maneno ya kategoria nyingine (Mrikaria, 2004). Kwa mfano, neno ‘baki’ ni kitenzi kinachoeleza hali ya mtu au kitu kutoondoka na pia, ni nomino yenye maana ya ‘salio’ kama inavyooneshwa katika tungo zifuatazo:

*Mwanafunzi alibaki darasani (hakuondoka darasani).*
*Baki kwenye akaunti yake ni sufuri (hakuna salio kwenye akaunti yake).*

Ingawa baadhi ya mbinu za uundaji wa maneno hazikujitokeza moja kwa moja, mawazo na maelezo ya wataalamu mbalimbali katika sehemu hii yalikuwa muhimu kukuza maarifa yetu kuhusu mbinu za kimofolojia za uundaji wa maneno. Hali hii basi ilipelekea kupata mwanga zaidi katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu.

### 2.4 Mabadiliko ya Kisemantiki katika Maneno ya Lugha

Dhana ya mabadiliko ya maana ilizungumziwa mwanzoni na Sapir anayeeleza kuwa kila neno na kila elementi ya kiisimu hubadilika polepole (Sapir katika Ullman, 1977). Mabadiliko ni sehemu muhimu katika maisha; bila mabadiliko, maisha hukoma (Keith & Shuttlewoth, 2000). Mabadiliko ya maana hujitokeza neno linapotumiwa kuwasilisha maana ambayo awali haikuhusishwwa nalo (Lourens & wenzie, 1992). Maelezo ya wataalam hawa yalitupa msingi katika kuelewa dhana ya mabadiliko ya maana. Bloomfield (1930) anajadili aina mbalimbali za mabadiliko ya maana. Anataja aina kama vile: upanuzi wa kimaana, upanuzi wa kisitiari na chuku. Anadai kuwa kila badiliko la kimaana huathiri maneno katika kikoa maaana. Ingawa utafiti huu haukuchunguza moja kwa moja athari hizo, kutokana na kazi ya Bloomfield (ameshatajwa), utafiti huu ulipata mwelekeo wa kujadili mabadiliko ya maana yanayojitokeza katika anthroponimu za Wamaragoli.

Naye Blank (1998) anayafafanua mabadiliko ya kimaana kwa kuangazia hali mbalimbali zinazosababisha mabadiliko ya aina hii. Blank anahusisha chanzo cha mabadiliko ya kimaana na masuala ya kiisimu katika lugha inayohusika. Kwake, maneno yanaweza kutumika kwenye miktadha anuwai kuibua maana tofauti tofauti zinazonuiwa kuwasilishwa na msemaji anayehusika. Isitoshe, hali za kisaikolojia zinazoweza kuathiri uteuzi na matumizi ya maneno kwa mujibu wa uchukulio wa wahusika kuhusu maneno hayo zinafafanuliwa. Mawazo hayo yalinufaisha utafiti huu haswa katika kuelewa mabadiliko ya maana. Hata hivyo, utafiti huu umejitenga na kuchunguza vyanzo vya mabadiliko ya maana suala alilochunguza Blank katika utafiti wake. Vilevile, utafiti wake ulijikita katika uchanganuzi wa usemi wakati ambapo utafiti huu umejikita katika mabadiliko ya maana katika taaluma ya onomastiki.

Tafiti nyinginezo zinazohusiana na suala la mabadiliko katika maana zinaonekana katika kazi za Habwe (1999), Polyton (1982), Carston (2002), Mukuyu (2009), Njimu (2010), Ochoki (2010), Ochichi (2013), Gerba (2014), Okyere (2015), Mensah (2017) miongoni mwa wataalamu wengine. Akiongozwa na nadharia ya Ushirikiano miongoni mwa nadharia

nyinginezo, Habwe (1999) anachanganua matini za hotuba za kisiasa. Anazamia ufafanuzi wa uundwaji wa kidokezi kwenye ufasiri wa ujumbe uliomo kwenye matamko ya wanasiasa. Hata hivyo, uchunguzi huu ulijishughulisha na mabadiliko ya maana katika majina ya Kimaragoli yanayobuniwa kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili ukiongozwa na nadharia ya Pragmatiki Leksia wakati ambapo Habwe (ameshatajwa) alichunguza diskosi ya hotuba za kisiasa. Aidha, utafiti wake ulitufaa katika kuelewa jinsi masuala ya kipragmatiki huelezwa wakati wa kujadili mabadiliko ya maana katika majina ya Wamaragoli.

Polyton (1982) katika Wierzibickar (1992) anasema majina ya Kiingereza hutofautiana kimaana kutegemea viwango vya matamshi kwa mfano: *Pamela* - *Pammie, Catherine* - *Cathie, James* - *Jimmie, Deborah* - *Debbie, Thomas* - *Tom.* Polyton (ameshatajwa) anajikita katika uchunguzi wa dhana ya utoto/uchanga inavyodhihirika katika muktadha wa kijamii. Anafafanua kwamba mama anapomwita mtoto wake *Jim* huwa anamwona kama ‘mtoto’ hii ni kwa sababu kuna maana iliyowekewa jina *Jim* na *Jimmy.* Anatoa mifano ya majina mengine kama vile: Sally - Sarah, Suzie – Susan, n.k. ambayo anasema kuwa yanajenga dhana ya utoto. Dhana ya ‘utoto’ katika majina inafafanuliwa pia katika kazi ya Superanskaja (1978) anayesema kuwa majina ya kitoto aghalabu hufupishwa na hasa hutumiwa nyumbani kwa mfano, *Egoruska* - *Egor, Anniska* - *Anna, Nikituska – Nikita,* n.k. Anasema kuwa majina ya kitoto huwa na hisia dhahania yanapotumika. Ingawa watafiti hawa wameshughulikia maana katika majina, hawakujishughulisha na mabadiliko ya maana katika majina hayo.

Hussein (2007) anachunguza namna ambavyo maana za maneno yenye asili ya Kiarabu hubadilika yanapoingizwa kwenye mfumo wa lugha ya Kiswahili. Anajihusisha na namna maneno yalivyobadilika kimaana kutoka Kiarabu na kuchukua maana nyingine baada ya kuingizwa katika mfumo wa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, neno *taajir* la Kiarabu lina maana ya mfanyabiashara wa aina yeyote mkubwa au mdogo aidha, akionekana kukubaliana na hoja hii Shembilu (2017) anaongezea kuwa neno *taajir* lilitumiwa kurejelea ‘mfanyibiashara aliyemiliki duka’. Hata hivyo, katika fahiwa ya sasa si lazima tajiri awe mmiliki wa duka wala mfanyibiashara. Neno ‘tajiri’ linaweza kurejelea mfanyakazi wa aina yoyote mradi ana mali nyingi. Tajiri ni mtu anayehusishwa na maisha na hali nzuri kiuchumi. Yaani, mtu anayemiliki mali nyingi. Aidha, neno la Kiarabu *hanaa* lina maana ya ‘kupongeza au kutoa hongera.’ Katika mfumo wa lugha ya Kiswahili neno *hana* lina maana ya ‘kutoa rambirambi au mkono wa pole, hasa kwa mtu aliyefikwa na msiba.’ Tafiti hizi zilirutubisha maarifa ya utafiti huu kuhusu mabadiliko ya maana hata ingawa zilitofautiana kwa kiasi kikubwa hivi kwamba, wakati utafiti huu unachunguza mabadiliko ya maana katika

anthroponimu zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili, tafiti hizo zilichunguza mabadiliko ya maana ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili.

Mukuyu (2009) anachunguza ujitokezaji wa uchanganyaji lugha kwenye matini za matangazo ya benki ya *Commercial* pamoja na *Mobile Telecommunications* kwa mwongozo wa nadharia ya Pragmatiki Leksika. Anafafanua usimbaji na usimbuliwaji wa dhana ili kushawishi na kuwavutia wateja wanaolengwa. Utafiti wake uliimarisha maarifa yetu na uelewa kuhusu nadharia ya Pragmatiki Leksika mbali na kutupa mwelekeo wa jinsi maneno huweza kusimbwa na kusimbuliwa. Aidha, utafiti huu umejikita katika uchanganuzi wa anthroponimu za Wamaragoli ili kuchunguza mabadiliko ya maana na wala si uchanganyaji lugha.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Pragmatiki Leksika, Njimu (2010) anachunguza leksimu zinavyotumika kwenye magazeti ya michezo nchini Kenya. Azma yake ni kuonyesha dhima ya muktadha katika kuakisi dhana za dharura. Anajikita katika magazeti matatu: *The Standard, The Star* na *The Daily Nation.* Utafiti huu ulinufaika na utafiti wake, kwani uliuwezesha kuelewa maana inavyobadilika kwenye muktadha, mbali na kukuza uelewa wetu wa nadharia ya Pragmatiki Leksika zaidi. Kwa upande mwingine, Ochoki (2010) anachunguza maana inavyosimbwa katika nyimbo za *Hip hop* nchini Kenya akiongozwa na nadharia ya Pragmatiki Leksika. Usimbaji wa maana unafafanuliwa kwa matumizi ya michakato ya ubanaji na upanuzi wa maana. Utafiti wake ulitufanya tuelewe zaidi jinsi dhana zinavyosimbwa na kusimbuliwa, hali iliyotupa mwanga zaidi wa kuchanganua ubadilikaji wa maana katika anthroponimu za Wamaragoli.

Akidah (2013) anachunguza maneno mkopo ya Kiarabu kwenye mfumo wa lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia mabadiliko ya kisemantiki na ya kifonetiki. Anafafanua michakato mbalimbali inayohusishwa katika ukopaji wa maneno ya Kiarabu kwenda kwenye mfumo wa lugha ya Kiswahili. Vilevile, anabainisha michakato anuwai inayosababisha mabadiliko ya maana kama vile upanuzi, udhalilikaji na ufinyizi wa maana. Kwa mfano, anaeleza kuwa neno, ‘msherati’ linanorejea maana ya, ‘mtu ambaye ni ashiki wa tabia ya kujiingiza kwenye tendo la mapenzi haramu’, linatokana na leksimu ya Kiarabu, [جiڵrat] inayowasilisha maana chanya ya, ‘uhusiano wa karibu.’ Utafiti huu ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu kwani ulifafanua mabadiliko mbalimbali ya maana.

Ochichi (2013) anatafitia umaanisho na usimbaji wa maana kimazungumzo katika lugha ya Kiswahili na Ekegusi akiongozwa na nadharia ya Pragmatiki Leksia. Anabainisha uwazi na umaanisho wa kauli za Ekegusii na Kiswahili. Utafiti wake ulikuza maarifa yetu zaidi kuhusu

nadharia na suala zima la ubadilikaji wa maana kimuktadha hata ingawa utafiti huu ulitofautiana na utafiti wake pakubwa, kwa vile yeye alilenga usimbaji wa maana katika mazungumzo ya lugha ya Kiswahili na Ekegusii wakati utafiti huu ulilenga kuchunguza mabadiliko ya maana katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili.

Gerba (2014) anasema kuwa maana ya majina katika jamii ya Oromo kule Uhabeshi inaibuka kutokana na kuongeza mofu kwenye mzizi wa neno, kwa mfano; mzizi *Lalis- (kukua)* unaweza kuongezwa mofu *-tuu* na kutengeneza jina *Lalistuu* (anayekua) jina la jinsia ya kiume au kuongezwa mofu *-ee* kutengeneza jina *Lalisee* la jinsia ya kike lenye maana hiyo ya 'anayekua'. Anabainisha mofimu zinazobeba maana *-tuu* na *-ee* zikipachikwa kwenye mzizi wa kitenzi. Ingawa katika utafiti wake anajishughulisha na maana ya majina yajengwayo kutokana na vitenzi kwa kutumia nadharia ya Semantiki, hakujishughulisha na mabadiliko ya maana; suala ambalo utafiti ulilenga kulichunguza katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili.

Akiongozwa na nadharia ya Sarufi Amilifu, Shemilu (2015) anachunguza namna nomino za mkopo zinavyopokelewa kisemantiki katika Kiswahili. Ufafanuzi wa sababu ambazo hupelekea mabadiliko ya maana wakati nomino mkopo zinapokewa katika mfumo wa lugha ya Kiswahili unabainishwa. Utafiti wake ulibainisha sababu mbili kuu zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika mapokezi hayo ya kisemantiki. Sababu ya kwanza ni matakwa ya kifahiwa. Endapo hitaji la kuiongezea maana leksimu inayohusika litatokea, mchakato wa upanuzi wa maana hujiri. Hata hivyo, iwapo leksimu ina maana nyingi ambazo hazihitajiki kwenye mfumo wa lugha kopaji, maana hizo zinapunguzwa. Tofauti za kiutamaduni baina ya lugha kopaji na ile kopwaji ndiyo sababu ya pili. Mathalan, kwenye utamaduni wa Waingereza vazi la *gauni* huvaliwa na wanawake pamoja na wanaume. Huvaliwa na wanawake harusini na majaji kortini. Pia, huvaliwa kwenye sherehe ya mahafali na hospitalini. Hata hivyo, katika utamaduni wa Kiswahili *gauni* ni kanzu au vazi linalovaliwa na wanawake. Hivyo basi, tofauti za kitamaduni zinaifinya maana ya 'gauni' hadi kusalia moja tu. Utafiti wa Shemilu (ameshatatajwa) uliimarisha maarifa kuhusu mabadiliko ya maana hata ingawa utafiti huu haukuchunguza sababu za mabadiliko ya maana katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

Okyere (2015) anachunguza utoaji wa majina na maana ya majina katika jamii ya Bukusu wa Kenya. Anabainisha maana katika mofu zinazounda majina katika jamii hii. Kwa mfano,

anabainisha mofu zinazopachikwa kwenye mzizi wa neno ili kutofautisha jinsia, mofu {wa-} huonyesha majina ya kiume na mofu {na-} majina ya kike kama vile; ***Wa**njala* (kiume) ***Na**njala* (kiume), ***Wa**ngila* (kiume) ***Na**ngila* (kike) na ***Wa**nyama* (kiume) na ***Na**nyama* (kike). Katika utafiti wake hakujishughulisha na mabadiliko ya maana katika majina hayo pia hakushughulikia mbinu za uundaji wa majina hayo. Hata hivyo, utafiti wake ulitufaa sana katika kuelewa maana ya majina ya watu kileksia japo utafiti huu ulipiga hatua kuchunguza mabadiliko ya maana katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

Katika utafiti mwingine, Hussein (2016) anachunguza mabadiliko ya kifonolojia na kisemantiki katika maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Pamoja na kutalii athari ya maingiliano ya kiutamaduni, kidini na kijamii, utafiti huu pia unaangazia uhusiano wa kihistoria baina ya Kiswahili na Kiarabu. Inagundulika kwamba baadhi ya maneno yanapewa maana nyingine kinyume na ile maana ya asili au wakati mwingine maana hizo katika Kiswahili hazina mantiki yoyote wala usahihi. Utafiti wa Hussein (ameshatajwa) haukujihusisha na anthroponimu hata hivyo ulifaidi utafiti huu hasa katika kuelewa mabadiliko yanavyotokea katika maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu.

Babusa (2017) anachunguza etimolojia na ubadilikaji wa sauti na maana kutoka mfumo wa lugha ya Kiarabu kuelekea Kiswahili. Mabadiliko anuwai ya maana za maneno kwenye mchakato wa ukopaji yanadhihirishwa. Mathalan, maana msingi ya leksimu *dar* kwenye mfumo wa Kiarabu ilikuwa 'nyumba'. Hata hivyo, inapokopwa na kuingizwa katika mfumo wa Kiswahili inabadilika na kuwa, 'sehemu iliyo chini ya paa la nyumba'. Leksimu *'dar'* inapatikana pia katika jina la mji, Dar es Salaam, kwa maana ya 'nyumba ya amani'. Ingawa utafiti wa Babusa (ameshatajwa) ulilenga mabadiliko ya maana katika mchakato wa ukopaji haukushughulikia anthroponimu. Hata hivyo, utafiti wake ulitueleweshа namna ambavyo mabadiliko ya kimaana hutokea katika mfumo wa lugha ya Kiswahili.

Mensah (2017) anaonyesha namna ambavyo majina katika jamii ya Ibibo kule Naijeria hutumika kuwasilisha ujumbe wa moja kwa moja. Anatumia mifano kama vile: *Nnamso*-nimefanya nini? *Ayatmo* - wacha iwaume, *Imoodoufen* - kuwa na utajiri ni mateso. Majina haya yanatumika kuwasilisha hisia za watoa majina kwa jamii au kwa mtu binafsi. Utafiti wake uliufaa utafiti huu kuelewa zaidi namna majina yanavyobeba ujumbe na kuuwasilisha kwa jamii. Ingawa utafiti huu ulilenga hasa suala la mabadiliko ya maana katika anthroponimu, suala ambalo utafiti wa Mensah (2017) haukujihusisha nalo.

Utoaji majina ni njia ya kupasha ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Obeng (1999) anatoa kauli hii anapochunguza michakato ya kuwasiliana isiyo ya moja kwa moja katika jamii ya Akan akirejelea majina ya wanyama. Anadokeza kuwa mtu akichukizwa na matendo ya jirani yake na hataki kumwambia moja kwa moja ili aepuke kuwa na ugomvi naye, anaweza kumpa mbwa wake jina linalopasha ujumbe kwa jirani kila mara likitajwa kwa sauti na kuashiria dhana kama "hauna asante", "kaa kwako" kama njia ya kuwasiliana na jirani katika huo muktadha wa kijamii ambapo hataki kumwambia moja kwa moja. Utafiti huu ulitufaa katika kuelewa zaidi namna wanadamu wanavyosimba ujumbe na kuuwasilisha katika majina wanayoyatoa. Ingawa alichunguza majina ya wanyama, utafiti huu ulipiga hatua na kuchunguza mabadiliko ya maana katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili. Akiishadidia dhima ya majina kwenye mchakato wa mawasiliano, Ansu-Kyeremeh (2000) aneleza kwamba katika jamii ya Bono majina yana sifa za kuwasilisha ujumbe. Katika utamaduni wa jamii hii, mtoto aghalabu hupewa jina kwa lengo la kufufua kumbukumbu fulani na kuziwasilisha kwa jamii. Ingawa utafiti huu ulikuwa muhimu katika kusaidia utafiti huu kuelewa namna majina yanaweza kuwasilisha ujumbe kwa jamii na fasiri ambazo jumbe hizo zinaweza kupata, ulitofautiana na utafiti huu. Wakati utafiti wa Ansu-Kyeremeh ulichunguza mawasiliano katika majina ya jamii ya Bono, utafiti huu ulilenga majina ya Kimaragoli yanayojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili kwa lengo la kuchunguza mabadiliko ya maana katika anthroponimu hizo.

Lusekelo (2017) anachunguza maenezi ya leksimu mbalimbali za Kiswahili zinazohusu nafaka na aina za vyakula katika lugha za Kibantu nchini Tanzania. Mabadiliko mengi ya kifonolojia na kisemantiki yanajitokeza katika leksimu zinazohusiana na nafaka pamoja na vyakula. Mathalan, leksimu mtama (*itama*) kwenye mfumo wa lugha ya Kigogo; *uhemba* ikiwa ni leksimu ya mtama. Kwenye mifumo ya lugha za Kimachache na Kipare, mahindi huitwa -*emba.* Awali, Guthrie (1971) alikuwa ametaja shina *pemba kuwakilisha 'mtama' ambalo pia hutumika kuwakilisha mahindi katika sehemu za Kaskazini Mashariki mwa Tanzania. Mfano huu unaonyesha kupanuka kwa maana ya leksia 'mtama'. Kupitia utafiti wa Lusekelo (ameshatajwa) utafiti huu ulikuza maarifa zaidi ya badiliko la upanizi wa maana na kuelewa namna maneno yanavyoathirika na mabadiliko ya kisemantiki.

Katika uchunguzi wake wa majina ya mifugo, Batoma (2009) anaonesha namna jamii ya Kabre nchini Togo inavyotumia majina ya wanyama kuwasilisha ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Anaeleza kuwa majina hayo husheheni hisia za watu wa jamii, hofu walio nayo miongoni mwa mambo mengine na kwa mahasidi wa jamii hiyo, familia hasi na jamii

nzima kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Ingawa utafiti wake uliusaidia utafiti huu katika kukuza maarifa kuhusu majina kwa ujumla, majina ya wanyama hayakuhusishwa katika utafiti huu. Aidha, utafiti wa Batoma (2009) haukushughulikia mabadiliko ya maana katika majina hayo.

Akichunguza dhima ya majina ya Sesotho, Latsoela (2015) anasema kuwa majina ya Sesotho aghalabu huwasilisha ujumbe mbalimbali, yakiwemo matukio yaliyotokea mtoto alipokuwa akizaliwa, matukio yanayohusiana na kuzaliwa kwenyewe, na kadhalika. Anatamatisha kuwa, jamii ya Sesotho haitoi jina kama kitambulisho cha mtu binafsi tu bali jina hutolewa na sababu fulani ikiwemo ya kuwasiliana. Akiishadidia hali hiyo, Mutunda (2017) anafafanua kwamba jina la mtu ni kama stakabadhi ambapo historia, utamaduni na urithi wa mtu binafsi au wa jamii unaweza kusomwa. Tafiti hizi zilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwani zilijadili kwa undani majina katika tamaduni zao na kuimarisha uelewa wetu zaidi kuhusu majina katika tamaduni mbalimbali.

Gichuru (2020) anachunguza mabadiliko ya maana za leksia za Kiswahili huku akijikita katika mtazamo linganishi wa kikale na sasa. Mifano mahususi ya leksimu za Kiswahili cha kabla na baada ya karne ya ishirini inalinganishwa kwa mujibu wa mabadiliko ya kimaana. Inabainika kuwa leksimu za Kiswahili zimeathiriwa mno na mabadiliko ya kisemantiki kama vile upanuzi wa maana ulijitokeza zalishi zaidi kwa 65% ya leksia zilizochanganuliwa, sitiari 43%, usogezi wa maana 23%, udhalilikaji 15%, ufinyizi 7%, tasfida 6%, sinedoche 6%, uimarikaji 5%, metonimu 3% na chuku 1%. Utafiti huu uliimarisha uelewa wa aina za mabadilko ya maana na namna yanavyojitokeza katika lugha.

Kwa ujumla, kazi hizi ni muhimu kwani zinahusu mabadiliko ya kimaana katika majina. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa pana tafiti chache zilizojihusisha na suala la mabadiliko ya kimaaana katika taaluma ya onomastiki, hasa katika anthroponimu zinazojengwa kwa nomino za Kiswahili. Vilevile, uwezo wa nadharia ya Pragmatiki Leksia katika taaluma ya onomastiki haujachunguzwa kikamilifu; hali iliyobainisha pengo na kuuchochea utafiti huu kufanywa ili kuchangia katika kuendeleza nadharia hii na kuchangia katika maarifa ya kiisimu kuhusu mabadiliko ya maana katika taaluma ya onomastiki.

### 2.5 Hitimisho

Sura hii imehakiki tafiti za wataalam mbalimbali zilizo na uhusiano na mada yetu ya utafiti. Mchango, tofauti, mianya na hata upungufu uliojitokeza katika tafiti na maandishi yaliyohakikiwa umejadiliwa. Imethibitika kwamba majina ya watu yanaweza kuainishwa

kwa misingi mbalimbali. Isitoshe, hakuna njia maalum shikilizi ya inayofuatwa. Mabadiliko ya majina ya jamii pia hutokea huku majina yakiweza kuundwa kutokana na mbinu mbalimbali za kimofolojia kama vile: mwambatano, unyambulishaji, ufupishaji, uradidi, ubunaji na ya uhamishaji maana. Sura inayofuata inashughulikia mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua mbinu za utafiti. Mbinu za utafiti zinafasiliwa na Kothari (2004) kuwa ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufakisha uchunguzi. Mbinu za utafiti zinaweza kugawika katika makundi mawili makuu: mbinu zitumikazo kukusanya data na mbinu zitumikazo katika uchanganuzi wa data. Kwa hivyo, sura hii inafafanua jinsi utafiti ulivyotekelezwa. Inashughulikia vipengele vya utafiti kama vile: muundo na eneo la utafiti, idadi lengwa, usampulishaji na sampuli yenyewe, njia na vifaa vya kukusanyia data pamoja na uthabiti wa data. Isitoshe, mbinu zilizotumika kuchanganua data na kuwasilisha matokeo zimeelezwa. Hatimaye, uzingatiaji wa maadili ya utafiti umeelezwa kabla ya kuwasilisha muhtasari wa yaliyomo kama hitimisho la sura.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti ni mpangilio unaotumiwa kupata majibu ya maswali ya utafiti. Ritchie na Lewis (2003) wanaufasili muundo wa utafiti kuwa ni ramani imwongozayo mtafiti katika kupata majibu ya maswali ya utafiti. Utafiti huu ulikuwa wa kistahilifu. Kama wanavyoeleza Creswell na Clark (2004), utafiti wa kistahilifu aghalabu unahusisha uchambuzi wa dhana inayohusika, ufasiri wa data zilizokusanywa na maelezo yanayohitajika. Kombo na Tromp (2009) wanafafanua kwamba utafiti wa kistahilifu huhusisha upataji wa maarifa nyanjani au maktabani. Uchanganuzi wa data hufanywa kwa mujibu wa jamii inayohusika, na pia huzingatia utoaji wa maelezo na hitimisho maalum.

Utafiti wa kistahilifu hulenga vilevile maelezo ya maneno au data na haujishughulishi sana na data za kitwakwimu (Powell & Renner, 2003; Brikci & Green, 2007). Mara nyingi utafiti wa kistahilifu huzingatia data zinazokusanywa kutokana na mbinu za uchunzaji, usaili na kurekodi data inayohusika (Mugenda & Mugenda, 1999; Baxter & Jack, 2008). Anavyoeleza Maxwell (2008), utafiti wa kistahilifu haudhihirishi muundo maalum ambao lazima uzingatiwe na mtafiti anayehusika kama tunavyoona katika tafiti mbalimbali za kitakwimu. Badala yake, unaelekea kuhusisha muundo wowote atakaochagua mtafiti mwenyewe huku uchanganuzi wa data zake ukifanywa pia kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mazingira asilia (Creswell, 2003a, 2003b; Golafshani, 2003; Flick 2009; Hancock, Ockleford & Windridge, 2009; Flick 2010). Kuhusiana na ufaafu wa mkabala huu wa kistahilifu, Mugenda na Mugenda (1999:202) wanasema kwamba:

> *Mkabala wa kithamano unafaa zaidi katika kufanya utafiti barani Afrika kwa sababu, taarifa nyingi hupitishwa kwa njia ya mdomo. Mkabala huu ni mwafaka kwani, unasisitiza zaidi usemaji pamoja na kuwapa watafitiwa fursa ya kutoa maoni yao kuhusu matatizo yanayowakumba na mbinu zinazoweza kutumiwa kuyapata.*

Utafiti huu unahusu uchanganuzi wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili kwa kuzingatia muundo wa utafiti wa kimaelezo. Muundo wa kimaelezo unahusisha kurekodi, kueleza na kuchanganua data kwa mujibu wa madhumuni husika (Kombo & Tromp, 2009). Ili kufaulisha muundo wa kimaelezo vipashio kama vile eneo mahususi la utafiti; wasailiwa, mbinu za ukusanyaji data, uchanganuzi, uwasilishaji, ufasiri na uthibitishwaji data aghalabu huzingatiwa (Creswell & Clark, 2004).

Muundo wa kimaelezo aghalabu hutumika uchunguzi unapohusisha idadi kubwa ya watafitiwa au vitafitiwa na sampuli sadifu inayoweza kuwakilisha jumuiya yote inahitajika (Kothari, 2004). Kwa kuzingatia muundo huu, data ilikusanywa moja kwa moja kutoka jamii ya Wamaragoli na kuainishwa katika makundi, kuchambuliwa na kisha maelezo kutolewa ili kuyajibu maswali ya utafiti. Mihimili ya nadharia ya utafiti ilizingatiwa, na hatimaye matokeo kuwasilishwa kinathari.

Muundo wa kimaelezo ulizingatiwa kwa sababu huzalisha data inayotegemewa haraka na kwa njia rahisi (Oso & Onen, 2006). Muundo huu ulisaidia kukusanya data ya anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili, kuichanganua data hiyo kwa kuiweka katika vikoa maana, kufafanua mabadiliko ya maana katika anthroponimu hizo na kueleza mbinu za kimofolojia zinazohusika katika uundaji wa anthroponimu hizo.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na nyanjani. Mtafiti alikusanya data ya upili ya nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli kutoka maktabani kabla ya data msingi ambayo ni anthroponimu za Kimaragoli. Trochim (1999) anaeleza kuwa mkabala wa nyanjani aghalabu hufanikisha ukusanyaji wa data za kutosha ziwezeshazo ujumlishaji wa matokeo ya utafiti na kuonesha uhusiano uliopo.

Uteuzi wa eneo la utafiti aghalabu huzingatia vigezo kama vile, idadi ya watafitiwa, uwezo wa kufikia au kupata data kwa urahisi, jamii husika na utamaduni wake, na kadhalika (Arsenault, Michael, Barke, Ravel & Gosselin, 2013). Hivyo basi, utafiti nyanjani ulitekelezwa katika eneo la kijiografia la gatuzi dogo la Sabatia lililoko katika gatuzi la Vihiga. Gatuzi la Vihiga lina magatuzi madogo matano: Emuhaya, Luanda, Vihiga, Hamisi

na Sabatia. Kimsingi, Wanyore, Watiriki, Waterik na Wamaragoli ndizo jamii kuu kwenye gatuzi hili. Wamaragoli wanapatikana katika magatuzi madogo mawili: Sabatia na Vihiga. Kutokana na kuongezeka maradufu kwa idadi ya Wamaragoli, mashamba yao yalianza kuwa madogo; hali iliyopelekea baadhi ya Wamaragoli kuhama na kutafuta makaazi mbadala katika maeneo mengine kama vile Kitale, Nakuru, Molo, Nandi, Njoro, Elburgon, Migori, Bungoma na maeneo mengine nchini Kenya (Bwonya, 1998).

Wamaragoli waliohamia kwingineko hawakushirikishwa katika utafiti huu kwa vile huenda wameathiriwa na utamaduni wa jamii nyinginezo. Gatuzi dogo la Sabatia liliteuliwa kwa kutumia sampuli dhamirifu kwa sababu Wamaragoli wanaopatikana katika sehemu hizo nyingine nje ya Vihiga walihama kutoka eneo la Sabatia na Vihiga (Bwonya, 1998). Kwa hivyo, kwa kiasi fulani, uzungumzaji wao umeathiriwa na lugha za jamii nyingine zilizowapokea.

Data ya anthroponimu ilikusanywa kutoka hospitali tatu kuu za umma zilizoko katika gatuzi dogo la Sabatia. Hospitali hizo ni: hospitali kuu ya gatuzi dogo la sabatia, hospitali ya Givudimbuli na hospitali ya Inyali. Hospitali hizi ziliteuliwa kidhamirifu kwa kuwa ndizo hospitali kuu za umma katika gatuzi la Sabatia ambazo hutoa huduma kwa wenyeji mara kwa mara kwa hivyo zilifaa katika kupata data ya majina ya wenyeji hao Wamaragoli.

Vilevile, utafiti huu ulihusu eneo la kitaaluma la kiisimu. Ulijikita katika mawanda ya onomastiki, semantiki na mofolojia. Onomastiki ni taaluma maalum inayochunguza au kutalii majina ya viumbe (Crystal, 1987). Taaluma hii inajumuisha mbinu za kutambulisha majina ya watu na mahali. Onomastiki imegawika katika matawi mawili: tawi la anthroponomastiki linalochunguza majina ya binadamu na tawi la toponomastiki linalochunguza majina ya mahali. Utafiti huu uliegemea taaluma ya anthroponomastiki ambayo hujishughulisha na uchunguzi wa anthroponimu yaani, majina ya watu. Kwa vile ulijihusisha na uchunguzi wa mbinu za kimofolojia zinazounda athroponimu hizo, utafiti huu ulitumia maarifa ya taaluma ya mofolojia. Habwe na Karanja (2004) wanasema mofolojia ni neno linalotumiwa kumaanisha utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa maneno na semantiki ni stadi ya maana. Kwa vile utafiti huu ulichunguza mababadiliko ya kimaana katika anthroponimu hizo, basi ulizingatia maarifa ya taaluma ya semantiki pia.

### 3.4 Idadi Lengwa

Bryman (2012) anafasili idadi lengwa ya utafiti kama watu, vitu vyote au matukio yote ambayo mtafiti angependa kujumuisha katika utafiti wake. Aidha, idadi lengwa huwa ni

jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika utafiti yaani, watu, taasisi, na kadhalika (Lune, 2010). Kwa ujumla, idadi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa, yaweza kuwa wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kama wanavyofafanua Palinkas na wenzie (2013) ni vigumu kuamua idadi lengwa katika tafiti za kithamano kabla ya kuanza utafiti husika ama maktabani au nyanjani hivyo basi idadi lengwa hutambulika baada ya kukusanya data.

Kwa mujibu wa Sarananavel (1992), Mugenda na Mugenda (1999) na Nyandemo (2007), ugumu wa kubashiri idadi lengwa huchangia kuwepo kwa mlegezo kwa watafiti hasa kuhusu idadi husika ya kuchunguzwa au asilimia ya idadi hiyo. Hivyo basi, mtafiti aghalabu huelekea kuzingatia madhumuni na wakati wa utafiti ili kuweza kutoa uamuzi wa idadi ya data inayotakikana ambayo inaweza kuwa idadi yote au yoyote atakayochagua ili kutosheleza mahitaji ya utafiti wake (Mugo, 2002; SAGE, 2008). Utafiti huu ulilenga majina ya Kimaragoli yanayojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

### 3.5 Usampulishaji na Sampuli

Uteuzi wa sampuli kama anavyoeleza Bryman (2004) ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kutumiwa katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalochunguzwa kwa sababu siyo rahisi kutafitia kundi zima. Usampulishaji dhamirifu ulizingatiwa katika uteuzi wa anthroponimu za Wamaragoli na uteuzi wa wasailiwa. Usampulishaji dhamirifu hutumika katika tafiti nyingi za kithamno kwa minajili ya kusaidia katika uteuzi wa data faafu na vilevile idadi ya wasailiwa tarajiwa ili kufaulisha madhumuni ya utafiti (Kombo & Tromp, 2009). Hutumiwa kuchunguza data isiyoyumkinika au isiyojulikana idadi kamili inayotakikana (Nyandemo, 2007).

Usampulishaji dhamirifu hutoa uhuru wa kuteua idadi ya wasailiwa inayohusika pamoja na data isiyo kubwa wala ndogo sana (Onwuegbuzie & Leech, 2007). Hata hivyo, huzingatia ile data ambayo ni toshelevu kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti, gharama ya utafiti husika, malighafi zitakazotumiwa, sifa za wasailiwa na ujumbe unaolengwa katika utafiti (Tongco, 2007; Crossman, 2015; Guetterman, 2015).

Usampulishaji katika utafiti husaidia katika uteuzi wa sampuli inayohusika. Kama wanavyofafanua Best na Kahn (2010), sampuli ni sehemu ndogo ya jumuiya ambayo imechaguliwa kwa minajili ya kuchunguzwa kwa kina. Kwa kuchunguza sifa mbalimbali katika sampuli, Babbie (2014) anasema kuwa mtafiti hatimaye hupata uamuzi au matokeo

ambayo huyajumuisha kama matokeo ya jumuiya nzima aliyokuwa akishughulikia. Uteuzi wa sampuli ni utaratibu wa kuchagua idadi ndogo ya wahusika binafsi kutoka kwa jumuiya pana hivi kwamba ile sampuli iliyoteuliwa ina uwezo wa kuwakilisha ile jumuiya pana kikamilifu (Babbie, 2014). Kwa mujibu wa Best na Kahn (2010), uteuzi wa sampuli hutegemea aina ya usampulishaji uliozingatiwa huku mtafiti akiteua sampuli ambayo ina wahusika wenye sifa anazozitaka pekee na wale ambao anakisia kuwa watampa majibu anayotaka. Sampuli hiyo si ya kubahatisha hata hivyo mtafiti ana uhuru wa kuteua watafitiwa kwa kutegemea sifa anazozitafitia katika jumuiya yake (Creswell & Clark, 2004).

Usampulishaji dhamirifu hauzingatii ukubwa wa sampuli bali sampuli yenyewe inayomwezesha mtafiti kupata data ya kutosha itakayoshughulikia suala la utafiti kikamilifu (Patton, 1990; Lune, 2010). Aidha, sampuli haiteuliwi kiholela yaani bila utaratibu wowote ule bali hufaa kuteuliwa kwa kufuata utaratibu au vigezo maalum. Vigezo vya kuzingatiwa ili kupata sampuli husika ni kama vile kazi, tajriba, jinsia, uchumi, utamaduni, akili na mahali pa wasailiwa ambao wanalengwa (Roller, 2011).

Kwa hivyo, mbinu ya usampulishaji dhamirifu ilitumika katika utafiti ili kuteua sampuli ya hospitali tatu **(03)** za umma ambazo hutoa huduma kwa Wamaragoli katika gatuzi dogo la Sabatia ambapo data ya majina ilikusanywa. Hospitali hizi ni: hospitali kuu ya Gatuzi Dogo la sabatia, Hospitali ya Givudimbuli na Hospitali ya Inyali. Hospitali nyingine za umma kama vile: hospitali ya rufaa ya kaunti ya Vihiga, hospitali ya Kiragiru na hospitali ya Itando hazikuhusishwa katika utafiti huu kwa sababu ziko mpakani mwa magatuzi mengine madogo ambayo yako nje ya eneo letu la utafiti. Vilevile, Katika gatuzi dogo la Sabatia kuna hospitali za umma na za kibinafsi, utafiti haukuhusisha hospitali za kibinafsi kwa sababu ya mbinu ya usampulishaji kidhamirifu iliyokuwa ikitumika kusampulisha hospitali.

Data ya sampuli ya anthroponimu 224 zilizojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili zilipatikana katika sajili za hospitali. Hospitali zilihusishwa katika utafiti huu kwa vile ndiyo sajili andishi ya kwanza mtu anapopewa jina na huwa msingi wa kunakili majina ya watu wanapozaliwa, wakiugua au hata wakichanjwa. Vilevile, katika jamii ya kisasa wazazi wengi aghalabu hujifungua watoto hospitalini na ni hospitalini ambapo mtoto hupewa jina mwanzo na hatimaye kusajiliwa katika sajili za hospitali husika.

Aidha, usampulishaji dhamirifu ulitumika katika kuteua sampuli ya wasailiwa ambao walikuwa baraza la wazee Wamaragoli ili kupata maana inayowasilishwa na anthroponimu hizo na kuthibitisha uhalali na ukubalifu wa data iliyokusanywa. Kipp (2009) anasema kuwa

wazee ndio hazina na dafina ya lugha asilia na ni kupitia kwa wazee ndipo lugha hupata wazungumzaji wachanga kwa kuwa wameishi miaka mingi na wana umilisi wa vipengele vya lugha na utamaduni. Baraza la wazee la Wamaragoli liliteuliwa kwa sababu, linachukuliwa kuwa wasemaji wa jamii hii, ni wakaaji wa eneo hili, linajumuisha wazee wenye tajriba na maarifa katika lugha ya Kimaragoli na utamaduni wa jamii hii kwa hivyo, ndio wanajua mambo mengi zaidi ya utamaduni na lugha yao. Hivyo basi, ilikuwa rahisi kupata maana inayowasilishwa na anthroponimu kutoka kwao na maana ya kimsingi ya anthroponimu hizo. Kuna uchukulio kuwa wazee walioishi miaka mingi wana tajriba katika utamaduni na lugha kwani katika kuishi kwingi wamejishughulisha na mambo mengi ya utamaduni wakitumia lugha (Kipp, 2009). Vilevile, tafiti nyingi katika taaluma ya lugha zinakubaliana kwamba wazee ni kipengele muhimu katika uendelezaji na urithishaji wa tajriba na dafina zote za lugha (Sallabank, 2010; Bartolato, 2012; Odero, 2013; Okal, 2018; Sangili, 2019).

### 3.6 Mbinu na Vifaa vya Ukusanyaji Data

Cresswell (2014), anasema kuwa, kabla ya kuenda nyanjani kukusanya data, ni muhimu na sharti mtafiti awe na mpangilio wa vifaa vya kukusanya data. Anaendeleza kuwa, mtafiti anatakiwa kuteua kwa makini mbinu za ukusanyaji wa data ambazo zikitumiwa ipasavyo zitamwezesha kufanikiwa kwa lengo lililokusudiwa la utafiti. Kothari (2008) anasema kwamba ukusanyaji data ni zoezi la utafiti ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti hata hivyo, vifaa vya utafiti vinatokana na mbinu za utafiti zilizotumika kutika utafiti. Anaendelea kusema kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data. Mugenda na Mugenda (2008) wanasisitiza kuhakikisha kuwa mbinu za utafiti zinatoa aina ya taarifa zinazohitajika kujibu maswali ya utafiti. Utafiti huu ulitumia mbinu na vifaa vifuatavyo kukusanyia data iliyotumika kujibu maswali ya utafiti.

#### 3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji Data

Ukusanyaji data katika utafiti huu ulitekelezwa kupitia mbinu za upekuzi wa sajili za majina hospitalini na kupitia usaili wa baraza kuu la wazee Wamaragoli.

#### 3.6.1.1 Upekuzi

Mbinu ya upekuzi ilitumika kukusanyia data ya nomino za kawaida za Kiswahili sanifu kutoka kwa vyanzo vya maktabani vilivyojumuisha vitabu vya Kiswahili kama vile kamusi, vitabu vya fasihi, sarufi, na kadhalika. Nomino zilizokusanywa maktabani ni zile tu zinazochangia uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli.

Aidha, upekuzi wa sajili za majina kwenye maktaba ya hospitali zilizosampulishwa ulizalisha data ya anthroponimu za Kimaragoli zilizoundwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili ambazo zilichanganuliwa kimofosemantiki baada ya kusaili baraza kuu la wazee Wamaragoli. Milroy (1987) anasema kuwa mtafiti anayechunguza lugha yake asilia anaweza pia kutumia umilisi wake wa lugha inayohusika kupekua data ya utafiti kwani atajihusisha moja kwa moja na kile kitakachomsaidia kupata data inayohitajika.

Upekuzi ulilenga  majina ya wamaragoli yenye sifa zilizoafiki malengo na mihimili ya nadharia ya utafiti. Upekuzi ulitekelezwa kwa mwongozo wa orodhahakiki (Kiambatisho 2). Pasco na wenzie (2008) wanasema kuwa, vigezo vinavyotumiwa katika orodha ya uchunzaji huundwa kwa utaratibu maalumu ili kupata data inayohitajika. Vigezo vya orodha ya uchunzaji viliafikiwa na kurazinishwa baada ya utafiti mwigo. Hivyo basi, orodha ya uchunzaji ilitumika kama mpangilio maalum wa kumwongoza mtafiti hatua kwa hatua wakati wa upekuzi wa athnthroponimu za Wamaragoli. Milroy (1987) anaendeleza kuwa mbinu ya upekuzi inaweza kuwa na mapendeleo hivyo basi ili kufidia mapungufu ya mbinu hii, utafiti ulihusisha mbinu nyingine ya pili.

#### 3.6.1.2 Usaili

Usaili ni mbinu ya ukusanyaji data ambayo mara nyingi huwa ni ya ana kwa ana ambapo mtafiti hukutana ana kwa ana na watafitiwa wake kisha kuwauliza maswali moja kwa moja na kupata majibu ya haraka. Usaili huhusisha mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na watafitiwa ili kupata maelezo zaidi kuhusu baadhi ya mambo ambayo yasingeweza kuwekwa bayana kupitia mbinu nyingine ya utafiti(Babbie 1992). Mbinu hii huruhusu utoaji wa ufafanuzi pale inapoonekana kuwa dhana fulani haijaeleweka vyema katika swali lililoulizwa. Pia, mbinu hii hatimaye husaidia kuweka bayana istilahi ambazo zinaonekana kutoeleweka kwa watafitiwa kwa kufafanuliwa zaidi (Kothari, 2008).

Usaili unaweza kuainishwa katika makundi matatu - usaili wa ana kwa ana, usaili wa kikundi na usaili wa simu (Kothari, 2008). Ingawa mbinu hii inaweza kufanywa kwa aina hizo zote, utafiti huu ulizingatia aina ya usaili wa ana kwa ana. Aina hii iliteuliwa kutumika katika

utafiti huu kwa sababu inaruhusu unyumbukaji katika mchakato wa kuuliza maswali, kuweka bayana istilahi ambazo zinaonekana hazieleweki kwa watafitiwa ili kupata taarifa zaidi na za kina ambazo zilitumika kujibu maswali ya utafiti.

Baaada ya kupekua anthroponimu za Kimaragoli zilizojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili kutoka sajili za hospitali, mbinu ya usaili usorasmi wa ana kwa ana ilitumia kuhoji baraza kuu la wazee wa jamii ya Wamaragoli ili kuthibitisha maana za anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili zilizokuwa zimekusanywa kwa upekuzi wa vitabu maktabani pamoja na sajili za majina hospitalini. Baraza kuu la wazee lilijumuisha wazee wenye tajriba, maarifa ya kitamaduni, kijamii na umilisi mkubwa wa lugha ya Kimaragoli na utamaduni wa jamii hii. Usaili ulifanikishwa na mwongozo wa usaili wa Baraza la wazee (Kiambatisho 3).

### 3.6.2 Vifaa vya Ukusanyaji Data

Mugenda na Mugenda (2008) wanasisitiza umuhimu wa kutumia vifaa mbalimbali katika utafiti. Vifaa hivyo ndivyo husaidia mbinu za ukusanyaji data nyanjani na kufanikisha mchakato mzima wa ukusanyaji data. Kuthibitisha data iliyokusanywa na kuhakikisha kwamba kifaa kimoja kikifeli kingine kinaendelea kutumika, vifaa kama vile orodhahakiki, mwongozo wa usaili na kinasa sauti vilihusishwa.

Vifaa vya utafiti viliaandaliwa na kufanyiwa majaribio kabla ya utafiti, ili kubaini uthabiti na utegemevu wa data inayokusanywa nyanjani. Majaribio ya vifaa vya utafiti yalifanywa wakati wa utafiti awali. Matokeo ya utafiti awali yalisaidia kuviboresha na kuhakikisha utegemevu na uwezo wavyo kuzalisha data iliyokusudiwa kuyafikia malengo ya utafiti.

#### 3.6.2.1 Orodhahakiki

Upekuzi wa majina kutoka maktabani na kwa sajili za hospitali ulitekelezwa kwa mwongozo wa Orodhahakiki iliyoambatishwa (Kiambatisho cha 2).Orodha hakiki ulisaidia kufanikisha upekuzi wa data.

#### 3.6.2.2 Kinasa Sauti

Kinasa sauti  ni kifaa mojawapo  ambacho hutumika katika ukusanyaji wa data wakati wa utafiti (Kothari, 2008). Kinasa sauti kina uwezo wa kunasa sauti za  wahusika au katika mandhari ya utafiti. Wakati wa utafiti, kinasa sauti kilirekodi maelezo ya watafitiwa wakati wa kuwasaili. Kifaa hiki kiliufaa utafiti huu kwa sababu kilirekodi shughuli nzima ya usaili kwa vile mtafiti hana kasi ya kuandika kila kitu, hivyo basi kilikuwa hazina bora ya data.

Baada ya kurekodi, data hiyo ilihifadhiwa kwenye tarakilishi ili kifaa hicho kisije kikajaa na kushindwa kurekodi data zaidi. Kinasa sauti kina umuhimu mkubwa katika utafiti kurekodi data kwani, ina kasi ya juu ikilinganishwa na kasi ya mtafiti ya kuandikwa wakati wa usaili (Tessier, 2012).

#### 3.6.2.3 Mwongozo wa Usaili

Mwongozo wa Usaili ulitumiwa kama kifaa cha kuelekeza usaili wa baraza la wazee. Maswali yake yalikuwa mafupi mafupi na yenye kulenga madhumuni ya utafiti. Mwongozo wenyewe ulijumuisha orodha ya anthroponimu ambazo zilikwisha kupekuliwa kutoka kwa sajili za hospitali. Usaili wa baraza la wazee uliazimiwa kupata maana iwasilishwayo na anthroponimu mbalimbali za Kimaragoli (Kiambatisho 3).

Isitoshe, matumizi ya vifaa vya utafiti kama vile, kalamu na karatasi ni bora, kwani ni vifaa vya jadi vya utafiti na hapana shaka vitaendelea kutumika miaka mingi ijayo kwa vile ni vifaa rahisi kupatikana, vyepesi kubeba na rahisi kutumika kwa vile havihitaji utaalamu wa pekee kutumia (Mulokozi, 2003). Hivyo basi, kalamu na karatasi vilitumika katika utafiti huu wakati wa upekuzi maktabani na hosipitalini na wakati wa usaili kuandika anthroponimu pamoja na maana zake.

## 3.7 Utafiti Awali

Utafiti awali hubainisha udhaifu wa vifaa vya utafiti na kurekebisha makosa yaliyomo kabla ya kuvitumia katika utafiti wenyewe. Majaribio hayo pia hudhihirisha uhalali na utumainifu wa vifaa hivyo (Mugenda & Mugenda, 2008). Hivyo basi, utafiti awali ni hatua mojawapo katika utafiti na hufanywa kwa ajili ya kutambua changamoto zinazoweza kutokea, udhaifu katika vifaa vya utafiti na nadharia kabla ya utekelezaji kamili wa utafiti.

Kwa vile, utegemezi na ukubalifu wa data hutegemea vifaa na mbinu zinazotumika katika ukusanyaji wa data, utafiti awali ulitupa fursa halisi ya kuvifanyia vifaa vya utafiti na njia za utafiti majaribio nyanjani tukitumia idadi ndogo ya watafitiwa. Lengo kuu la utafiti awali lilikuwa kubaini iwapo kuna dosari yoyote katika Mwongozo wa Usaili, kama vile utata katika maswali hayo, kutoeleweka vyema au kutokuwa wazi kwa maswali hayo kwa watafitiwa miongoni mwa masuala mengine. Aidha, mtafiti ulipata fursa ya kupima iwapo vifaa vya utafiti vitaibua data ya kutosha au la na iwapo data itakayopatikana kutoka kwa watafitiwa itakuwa mwafaka katika kujibu maswali ya utafiti.

Hatua ya utafiti awali ilitekelezwa baada ya wasimamizi kuvipitia vifaa vya utafiti, kutoa ushauri na mapendekezo yao na mtafiti kutilia maanani masuala yote kutoka kwa wasimamizi ili kuhakikisha kuwa vifaa hivi vitatumika kukusanya data ya utafiti kwa utegemevu wa hali ya juu. Vifaa vya utafiti vilifanyiwa majaribio katika gatuzi dogo la Vihiga, hospitali kuu ya gatuzi la Vihiga kule Vihiga ambayo haikuhusishwa katika utafiti huu. Katika awamu ya kwanza usampulishaji dhamirifu ulizingatiwa na takriban anthroponimu **10** zilikusanywa kutoka hospitali kuu ya gatuzi dogo la Vihiga kutumia mbinu ya upekuzi.

Mwongozo wa Usaili ulitayarishwa na anthroponimu hizo kujumuishwa kisha kufanyiwa majaribio kwa usaili wa kundi moja la wazee wa kawaida watano **(5)** walioteuliwa kidhamirifu. Kundi hili lilijumuisha tu wazee ambao hawashirikishwa kwenye vikao vya baraza la wazee la Wamaragoli. Wazee wastaafu baraza hilo ndio walioshirikishwa katika zoezi hili. Wakati wa usaili, kinasa sauti kilitumika kurekodi ili kubaini iwapo ina uwezo wa kurekodi kwa usahihi kwa muda mrefu. Data hiyo ilipangwa kwa mujibu wa maswali ya utafiti na ikachanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya utafiti kisha matokeo kuwasilishwa kwa wasimamizi.

Utafiti awali ulitumika kupima ufaavu wa mbinu na vifaa vya ukusanyaji data, hususan vipengele vya maswali kwenye Mwongozo wa Usaili na Orodhahakiki. Hata hivyo, iwapo pangebainika matatizo katika vifaa vya utafiti katika utafiti awali wa awamu ya kwanza, matatizo hayo yangerekebishwa kisha kutekeleza utafiti awali awamu ya pili ili kupima iwapo matatizo yaliyopatikana katika vifaa vya utafiti wakati wa majaribio awamu ya kwanza yangekuwa yamesuluhishwa. Kwa vile hapakutokea tatizo lolote, kwenye vifaa vya utafiti wakati wa awamu ya kwanza ya utafiti awali, awamu ya pili haikutekelezwa. Hivyo basi, matokeo ya utafiti awali yalisaidia kuboresha vifaa vya kukusanyia data na kuhakikisha upatikanaji wa data iliyotarajiwa.

### 3.8 Utegemevu na Ukubalifu wa Vifaa vya Ukusanyaji Data

Utegemevu ni hali ya kufungamana, kuaminika na kuthibitika kwa data zilizokusanywa na kuchunguzwa (Baxter & Jack, 2008). Ukubalifu nao ni uhalali wa data hizo zinazokusanywa na kuchunguzwa (Golafshani, 2003). Kama wanavyodokeza Long na Johnson (2000), utegemevu na ukubalifu katika utafiti mwingi wa kithamano hufanywa kwa kurejelea masuala kama vile: chanzo cha data, suala husika la utafiti, data msingi kutoka kwa wasailiwa, hali ya urudiaji wa ukusanyaji data mara kwa mara, kujadiliana kuhusu data, watu wenye tajriba nyingi au wataalamu wenye umilisi kuhusu mada husika, na vilevile kuhusisha

matumizi ya uthibitishwaji. Kufanikisha utegemevu na ukubalifu wa vifaa vya ukusanyaji data, uthabiti wa yaliyomo kwenye vifaa unapaswa kuhakikishwa ili suala linalochunguzwa lishughulikiwe kwa utoshelevu (Saunders, 2009). Utafiti huu ulizingatia maoni ya wasimamizi ambao walitathmini utegemevu na ukubalifu wa vifaa vya utafiti baada ya utafili awali kukamilika. Ushauri, maoni na mapendekezo yao yalizingatiwa katika uimarishaji na uboreshaji wa vifaa vilivyotumika katika utafiti huu.

Suala la uthibitishwaji wa data lilizinduliwa katika uchunguzi mahuluti wa kuyakinisha data inayohusika (Hussein, 2009). Istilahi hii ilibuniwa kwa sababu tafiti nyingi zilidhihirisha kuwa matumizi ya mbinu moja tu ya utafiti yalielekea kutozingatia suala la uthibitishwaji kikamilifu ili kuonyesha ukubalifu na utegemezi wa data (Golafshani, 2003; Cohen & Crabtree, 2006; Hussein, 2009). Hali ambayo ingesababisha upotoshi mwingi wa data na uchanganuzi wake. Kimsingi, mbinu ya uthibitishwaji huwasaidia watafiti kuongezea upeo na kina cha maarifa kuhusu data wanazozishughulikia, kuepuka kufikia uamuzi wa data bila ithibati au ukubalifu, kutoafikiana au kuafikiana kwa matokeo ya data anuwai pamoja na uyakinishi wa data hizo, hasa kwa kulenga nyanja, mbinu na taaluma nyinginezo ili kufikia uamuzi faafu wa uchanganuzi (Cohen & Cabtree, 2006; Hussein, 2009).

Ingawa kuna mitindo anuwai ya uthibitishwaji kama vile: wa chimbuko la data, mtafiti au mchanganuzi, kinadharia, kimbinu, kimazingira na kiuchanganuzi (Cohen & Crabtree, 2006: Hussein, 2009), utafiti huu ulizingatia uthibitishwaji mtafiti ambao hushirikisha wachunguzi au wataalam anuawai wa nyanja husika kuchunguza data za utafiti. Hivyo basi, anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili zilipekuliwa kutoka maktabani, zikathibitishwa kwenye sajili za hospitali zilozosampulishwa kisha kupelekwa kwa baraza kuu la wazee la Wamaragoli ambao ni wataalam na wenye tajriba katika masuala ya lugha hii na utamaduni wake ili kuthibitisha zaidi na kwa minajili ya kupata maana yake.

### 3.9 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Uchanganuzi wa data ni uchambuzi makini wa data iliyokusanywa nyanjani ili kufanya uamuzi fulani kuihusu. Uchanganuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupanga vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambavyo inawezesha kukamilisha malengo ya utafiti husika au kujibu maswali ya utafiti (Babbie, 2014). Data ya utafiti ilichanganuliwa kimaudhui huku mihimili ya nadharia ya Pragmatiki Leksia ikiongoza uchanganuzi huo. Uchanganuzi wa data kimaudhui unahusu hasa usomaji, utambuzi wa maudhui na hatimaye kuzipa utambulisho

data hizo kutokana na ruwaza zinazojitokeza (Brikci & Green, 2007; Kombo & Tromp, 2009).

Shughuli ya uchanganuzi wa data ilianza kwa kupanga data kutoka nyanjani katika makundi kwa mujibu wa maswali ya utafiti; nomino za kawaida za Kiswahili zinazotumika kujenga anthroponimu za Kimaragoli zilipangwa kwa utaratibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya Pragmatiki Leksika ambapo hizo ziliainishwa katika vikoa maana mbalimbali; hoja muhimu zilizokusanywa kutoka usaili zilizoandikwa kwenye daftari ziliunganishwa pamoja; rekodi za usaili kwenye simu ya kisasa kusikilizwa kisha kuzingatia michakato ya kipragmatiki kileksia ambao ni mhimili wa pili wa nadharia ya utafiti kujadili swala la mabadiliko ya maana na mbinu za kimofolojia zinazopelekea kuundwa kwa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili.

Baada ya uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo ya uchanganuzi wa data ulifanywa kwa njia ya maelezo. Maelezo hayo yamehimiliwa kwa mchango wa wataalamu walio kwenye sura ya uhakiki wa maandishi, nadharia, mifano na majedwali. Taarifa muhimu zinahusu ubainishaji wa nomino za kawaida za Kiswahili zinazotumika kujenga anthroponimu za Kimaragoli katika vikoa maana, ufafanuzi wa mabadiliko kisemantiki katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili na uchanganuzi wa mbinu za kimofolojia za uundaji wa anthroponimu hizo zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili zimetolewa kwa kuzingatia maudhui ya utafiti.

Matokeo ya utafiti wenyewe yamewasilishwa katika sura tano zinazojumuisha taarifa mbalimbali. Sura ya kwanza inahusu misingi ya utafiti; sura ya pili inajadili uhakiki wa maandishi; sura ya tatu inafafanua mbinu za utafiti; sura ya nne ni uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo; na kisha sura ya tano ni muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Kwa ufupi, uchanganuzi wa data ulilenga kujibu maswali yaliyoongoza utafiti huu.

### 3.10 Maadili ya Utafiti

Zoezi la utafiti aghalabu hukumbwa na masuala mengi ya kimaadili ambayo huibuka wakati wa ukusanyaji data nyanjani, wakati wa uchanganuzi na hata usambazaji wa ripoti (Cresswell, 2007). Gerg (2001) anafafanua chanzo cha uzingatiaji wa maadili ya kitafiti kwa kudai kwamba haja ya kuzingatia maadili ya utafiti ilitokana na utafiti wa kijanja uliofanywa na matabibu wa Kinazi, wakati wa vita vya pili vikuu vya dunia. Watafitiwa walihadaiwa kuwa, walikuwa wanatumiwa katika utafiti wa kisayansi wa tiba, kumbe, lengo lilikuwa ni kuwaangamiza kwa kuwapa sumu, virusi hatari, kuwaambukiza ugonjwa wa malaria.

Kwa maana hiyo basi, kila mtafiti hana budi kuzingatia maadili ya kitafiti kwa kutii sheria na kanuni zilizowekwa ili kuibuka na matokeo ya utafiti ambayo ni halali na ya kukubalika. Maadili ya kiutafiti hufasiliwa kuwa ni mbinu zinazotumika kukusanya data pamoja na kuwasilisha matokeo ya utafiti ambayo ni ya kuaminika bila kuwadhuru wasailiwa (Rubin & Rubin, 1995). Maadili ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu ulihusu kuingiliana na kutagusana na watu mbalimbali moja kwa moja katika jamii; wazee kutoka baraza kuu la wazee Wamaragoli. Bryman (2006) anashadidia kuwa, mtafiti yeyote anayeshughulikia masuala ya kijamii anapaswa kuwaza kwa makini kuhusu maadili ya utafiti. Hii ni kwa sababu, utafiti usio wa kitakwimu aghalabu, hugusa maisha ya watu na hata kuingilia maisha yao ya siri.

Utafiti huu basi ulizingatia maadili ya utafiti kikamilifu kabla ya, wakati wa na baada ya utafiti. Kwa mujibu wa Anol (2012), kabla ya kuenda nyanjani kukusanya data, mtafiti anapaswa kupata idhini. Hivyo basi, mtafiti aliomba ridhaa kutoka kwa kamati ya maadili ya chuo kikuu cha Maseno, MUERC (Kiambatisho 4). Ridhaa hiyo ilitumika kuomba na kupata kibali cha utafiti kutoka NACOSTI (Kiambatisho 6). Ridhaa kutoka MUERC pamoja na kibali kutoka NACOSTI ziliwasilishwa kwa afisa msimamizi wa afya katika gatuzi la Vihiga ambapo mtafiti alipewa barua ya kumtambulisha katika hospitali zilizosampulishwa kwa manajili ya kukusanya data (Kiambatisho 6). Kibali cha utafiti, ridhaa ya utafiti na barua zote za kumtambulisha mtafiti zilitumika kwa minajili ya utafiti pekee.

Kabla ya kuanza ukusanyaji wa data mtafiti alitumia stakabadhi zote za utafiti alizokuwa amezipata kutafuta ridhaa kutoka kwa uongozi wa baraza kuu la wazee la Wamaragoli. Mtafiti alipata ridhaa hiyo kwa njia ya mdomo kutoka kwa uongozi wa baraza la wazee ambao una mamlaka ya kijamii ya kutoa ridhaa yenyewe kwa niaba ya jamii tafitiwa. Mtafii aliipata ridhaa hii bila maandishi kwa kuzingatia misingi ya Gerg (2001) anaposema kuwa watafitiwa ambao wametumia ridhaa iliyoandikwa na inayotolewa kabla ya utafiti kufanywa, wameripoti kuwa, kuna uwezekano mkubwa wa kupata habari ambazo sio kamilifu kwa sababu wasailiwa ama wanakataa kuhojiwa au wanajiondoa wakati utafiti unapoendelea au wanapinga utafiti husika. Ili kukwepa hali hii, watafiti wengi hutumia mbinu ya kupata ridhaa kwa njia ya moja kwa moja. Anaendeleza kuwa, baada ya kuwaeleza watafitiwa malengo ya utafiti husika, kama hawakatai, basi wamempa mtafiti ridhaa.

Hivyo basi, ridhaa aliyopata mtafiti ilimwezesha kukusanya data kwa kuwasaili wazee wa baraza kuu la wazee la jamii ya Wamaragoli. Utafiti ulizingatia uwazi ambapo vifaa vyote

vya utafiti viliwekwa wazi, mtafiti aliwapa wasailiwa wote uhuru wa kuchagua kwa hiari yao, ama kushiriki au kutoshiriki katika utafiti huu bila shuruti wala hadaa yoyote. Aidha, wasailiwa walielezwa kuwa, hakuna athari yoyote chanya wala hasi itakayowakumba wale ambao wangeamua kutoshiriki katika utafiti huu. Fomu ya idhini ya watafitiwa (Kiambatisho 1) ilitumika kufanikisha elimu kwa watafitiwa kabla ya kushiriki katika utafiti, ikiwemo kuwaeleza umuhimu wa utafiti kwao. Leedy (1997) anasema kuwa, utafiti haupaswi kufanywa kabla ya malengo na manufaa yake kuwekwa bayana kwa watafitiwa kwa sababu ni hatia kumhadaa mtafitiwa yeyote akubali kushiriki katika utafiti wowote ule bila ya yeye kujua manufaa na hasara zinazotokana na kushiriki au kutoshiriki kwake katika utafiti.

Watafitiwa wote walisomewa fomu hii kwa utaratibu hadi wakaelewa kwa nini wanashirikishwa katika utafiti. Fomu hii ya kibali inajumuisha maelezo muhimu kuhusu faida za kushiriki, hatari za kushiriki na maswala mengine yanayohusiana na kushiriki au kutoshiriki kwao. Maswala yote ya utafiti ambayo yameelezwa katika fomu ya idhini ya mtafitiwa yalizingatiwa kikamilifu. Hili lilichochewa na maoni ya Gerg (2001) anaposema kuwa moja kati ya mahitaji ya maadili ya kitafiti ni kwamba, watafitiwa sharti waambiwe hatari au faida ambazo watazipata kutokana na kushiriki kwao katika utafiti husika. Anol (2012) anaendelea kuhoji kuwa wakati wa uchanganuzi wa data, usiri wa taarifa zilizotolewa unafaa kutiliwa maanani.

Data iliyokusanywa nyanjani imetumika tu kwa ajili ya utafiti pekee wala si kwa shughuli nyinginezo zozote. Ni jukumu la kila mtafiti kulinda data aliyopata kutoka kwa watafitiwa. Ulinzi wa data unahusisha kanuni za uchakataji habari za kibinafsi kama vile nyaraka zilizowekwa kama rekodi. Katika utafiti huu, data ghafi ilihifadhiwa kwenye kipakatalishi kilicho na nywila ambacho kilitumika tu na mtafiti pekee. Data hiyo haikutolewa wala kuwekwa wazi popote isipokuwa katika sehemu ya matokeo ya utafiti katika tasnifu. Isitoshe, kwa vile utafiti ulilenga kutafitia majina ya watu, maana zilizopatikana zimetumika kwa ajili ya utafiti huu pekee bali si za kubeza, kudhalilisha au kuwafanyia mzaha wahusika kwani baadhi ya majina yana maana hasi baada ya kufasiriwa.

Mbali na hayo, Mligo (2012) anasema kuwa wizi wa kitaaluma ni kinyume na maadili ya uandishi. Akitanua zaidi, wizi wa kitaaluma huhusisha wizi wa maneno, mawazo au vifungu vya maneno kutoka kwa watafitiwa au watu wengine bila kuonyesha ni ya nani au chanzo chake. Utafiti huu umezingatia maoni ya Mligo kwa kutambua mchango wa wataalamu wote

ambao kazi zao zilirejelewa katika utafiti huu na vyanzo vyote vya mawazo yao kwa kunukuu kisahihi ndani mwa tasnifu hii kisha kuorodheshwa katika sehemu ya marejeleo.

### 3.11 Hitimisho

Sura hii imeeleza mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu. Masuala yaliyofafanuliwa hapa ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, idadi lengwa, sampuli na usampulishaji. Pia, kuna maelezo kuhusu njia za utafiti, vifaa vya utafiti, namna data ilivyochanganuliwa na matokeo kuwasilishwa, na uhalali, utegemezi na ukubalifu wa data iliyokusanywa nyanjani, na hatimaye maadili ya utafiti kabla ya kuwasilisha hitimisho. Sura ya nne inayofuata inashughulikia uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Azma kuu ya uchunguzi huu ilikuwa kuchanganua kimofosemantiki anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo kwa nomino za kawaida za Kiswahili. Kuifikia azma hiyo, sura hii inawasilisha uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Matokeo yenyewe yanajadiliwa mintarafu ya malengo ya utafiti kwa mwongozo wa mihimili ya nadharia ya Pragmatiki Leksia. Data ya utafiti imekusanywa kwa matumizi ya vyanzo vya data ya msingi pamoja na vile vya data ya upili.

Data ya upili ilikusanywa maktabani kwa usomaji wa vitabu na machapisho anuwai. Nayo data ya msingi inajumuisha anthroponimu za Kimaragoli zilizokusanywa moja kwa moja nyanjani kwa matumizi ya mbinu kama vile upekuzi wa sajili za majina hospitalini, uchunzaji na usaili wa baraza la wazee. Kauli muhimu za wasailiwa zimenukuliwa au hata kudondolewa ili kushadidia na kuthibitisha data, madai na hoja zinazojengwa. Vielelezo na majedwali yametumika kuwasilisha matokeo huku maelezo yakitolewa. Kwa ujumla, data inachambuliwa kimaudhui na kuwasilishwa kimaelezo.

Muundo wa sura yenyewe unajumuisha sehemu kuu tano. Sura imeanza kwa utangulizi kabla ya kuziainisha nomino za kawaida za Kiswahili zitumikazo katika ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli katika vikoa mbalimbali vya maana. Kwenye sehemu ya tatu mabadiliko ya kisemantiki yanafafanuliwa. Hatimaye, mbinu za kimofolojia za uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zinachanganuliwa kabla ya kuwasilisha hitimisho la sura.

## 4.2 Vikoa Maana vya Nomino za Kawaida za Kiswahili

Lengo la kwanza la utafiti lilikuwa kubainisha nomino za kawaida za Kiswahili zinazotumika kujenga anthroponimu za Kimaragoli katika vikoa maana. Semantiki Leksika, mhimili wa nadharia ya Pragmatiki Leksika, ulitumika kuainisha anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili katika vikoa maana mbalimbali. Semantiki Leksika hujishulisha na maana ya maneno. Ingawa maneno aghalabu huchukuliwa kuashiria dhana au vitu katika ulimwengu kutegemea mtazamo mahususi, Wilson (2003) anasisitiza uchanganuzi wa maana kwa kuzingatia faridi leksika. Kwa mujibu wa Mbwanga (2010), vitengo vya maana katika Semantiki Kileksika ni vipashio vya kimsamiati ambavyo kwavyo

msemaji huongezea kwa mfululizo maishani pamoja na ujifunzaji wa maneno mapya na maana zake.

Semantiki Leksika hushughulikia mahusiano katika maneno kwa kuyaweka pamoja maneno yenye uhusiano wa kileksika. Katika utafiti huu, ukoa maana ulitumika kurejelea tapo la maneno yenye maana yanayohusiana kileksika. Dhana ya kikoa maana ya kisemantiki ilitumika kuainisha nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli. Ufafanuzi wa maana za nomino zinazohusika kimuktadha, ulifanikisha uainishaji wake katika makundi mbalimbali. Kwa usaidizi wa nadharia ya Semantiki Leksika, imethibitika kwamba anthroponimu za Kimaragoli 224 zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili zinadhihirisha uhusiano wa maana. Anthroponimu zenyewe zimeainishwa katika vikoa maana vya: wanyama (16), ndege (16), mimea na viungo (17), vyakula na vinywaji (9), vifaa mbalimbali (43), taaluma ya elimu (12), samani (8), magonjwa (10), sehemu za mwili (7), jamii na utaifa (8), mavazi (13), nyakati (14), silaha (7), wadudu (6), ukoo (6), taaluma za watu (12), kilimo (5), mapambo (5) na kikoa maana cha uchumi (9).

### 4.2.1 Kikoa Maana cha Wanyama

Nomino za kawaida za Kiswahili 16 zinazotumiwa kujenga anthroponimu za Kimaragoli zinathihirisha majina yenye maana ya kileksika ya wanyama. Wasailiwali walidhibitisha hali hii kwa kufafanua kuwa:

> *"Avarogori vahezanga vandu amita gi zinyama, kove nindi zinyama zinyingi zinyorekanga mu ringaha riavo. Zinyama zindara ku zio ziari zia kare na ziamenyanga mihiga jari ja hanyuma hara ndi, madiku gano zirorekaga rigaririgari da! Avandu vaveku nimihiga jakiginga ku nivo vanyara kuva vazimanya nitari avandu vakehevwa amita gizinyama yizio. Zinyama zindara nizindahi zimboma navuza izindi nizinduru noho mbore zinyara kwita umundu anoho kusaliza vudamanu. Amita mala gotova yago nigizinyama zya komenyi nangazio yengo nagandi gi zinyama ziu mmuritu anoho zyumbulimu. Zinyama kuri kibaga anoho kabaga, eng'ombe, kisungura, isimbwa, ipanya imburi, nizindi zinyingi ... Yee yizio ni zinyama zyetu kandi vandu vanyingi valangwa mita gazio, imbiti, gusimba, ndovu, chura, chui noho kachui, guruguru, kenge, ingwina, ing'amia, iswara na gandi manyingi ... ndakavoye ndi, gusimba nu gunyamanyama na lisimba ni isimbwa yagwa yu mmbulimu. (Baraza kuu la wazee Wamaragoli, Kikao cha kwanza, saa 10:00 asubuhi, 07/01/2021).*

Tafsiri:

> *'Wamaragoli huwapa watu majina ya Wanyama, kuna wanyama wengi ambao wanapatikana katika mazingira yao. Kuna wanyama ambao*

> *waliishi kitambo au walionekana kitambo katika jamii hii lakini siku hizi hawaonekani kwa urahisi, ni watu wa umri mkubwa tu wanao wajua. Hata hivyo, bado watu wanapewa majina yao. Baadhi ya wanyama ni wazuri wengine ni wakali/wabaya kwani wanaweza kudhuru mtu au hata kuua. Baadhi ya majina unayoorodhesha ni ya wanyama wanaofugwa na mengine ya wanyama mwitu. Wanyama wanaofugwa ni pamoja na paka, ng'ombe, sungura, mbwa, panya na mbuzi. Aidha, walikiri kuwa watu hupewa majina ya wanyama mwitu kama swara, simba, ndovu, chura, guruguru, kenge, ngwena, ngamia, mbiti, n.k. (Tafsiri Yetu, Usaili wa Baraza kuu la wazee Wamaragoli, Kikao cha kwanza, saa 10:00 asubuhi, 07/01/2021).*

Wasailiwa hao walisisitiza kuwa mtu anapopewa jina la mnyama huwa linawasilisha mambo mengi katika jamii ya Wamaragoli yakiwemo matarajio yao, imani zao, tamaduni na mahusiano yao na wanyama wanaohusika. Wilson & Carston (2007) wanafafanua kuwa Semantiki Leksika hujishughulisha na maana msingi ya neno na maana hizo za maneno huweza kuchukuliwa kuashiria vitu katika ulimwengu. Hivyo basi, maana kuu katika kikoa hiki ni mnyama. Kwa mujibu wa TUKI (2004) mnyama ni kiumbe mwenye uhai anayeweza kuhisi na kujongea kwa mfano, paka, mbwa na samaki. Animonimu ni majina ambayo asili yake ni majina ya wanyama na hutumiwa kuwaita watu. Mathalan, kule Marekani kuna majina kama vile *Little Bear* (Crystal, 1987), Buffalo na hata Beaver (Hatch & Brown, 1995). Uainishaji wa kikoa hiki unashadidia maoni ya Okal (2012) kwamba katika jamii za Kiafrika kuna majina yanayotokana na majina ya Wanyama. Kwa mfano, jamii ya Waluo kuna *Kwach* (chui), *Liech* (ndovu), *Simba* (Simba) na *Omuga* (Kifaru). Tofauti ni kuwa uanishaji katika utafiti huu ulikuwa wa nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli.

Kwa mujibu wa Semantiki Leksika nomino za kawaida za Kiswahili: paka, ng'ombe, sungura, mbwa, panya, mbuzi, swara, simba, ndovu, chura, chui, guruguru, kenge, ngwema, ngamia, mbiti, n.k. katika muktadha wa Wamaragoli zinaashiria au uhusiano wa maana au kikoa maana cha wanyama. Dirk (2010) anasema kuwa kikoa maana kimoja kinaweza kuzaa vikoa maana vingine vidogo vidogo. Kwa mantiki hii, kikoa hiki cha wanyama kiligawika katika makundi mawili makuu: kikoa cha wanyama wanaofugwa na kikoa cha wanyama mwitu.

#### 4.2.1.1 Wanyama Wanaofugwa

Kwa mujibu wa baraza kuu la wazee Wamaragoli, haya ni majina ya wanyama ambao walikuwa na wangali wanafugwa katika jamii hii. Hivyo basi, nomino hizi za kawaida za Kiswahili kwa mujibu wa Semantiki Leksika zina maana ya wanyama wanaofugwa. Majina

ya wanyama hawa yanatumika kama anthroponimu za kuwarejelea watu katika jamii hii. Okal (2012) anasema kuwa majina ya watu katika taaluma ya onomastiki yanaweza kuaninishwa katika makundi mbalimbali kama vile anthroponimu funge, anthroponimu siha, anthroponimu familia, anthroponimu thioforiki, anthroponimu lakabu, apotropiki, teknonimu, paidinimu, apotronimu, matronimu, patronimiki na animonimu. Animonimu ni kundi la anthroponimu zinazotokana na majina ya wanyama. Kwa hivyo, majina ya wanyama yaliyopekuliwa kutoka orodha ya sajili za hospitali yaliainishwa katika kikoa hiki kama inavyodhihirika katika Jedwali la 4.2. Animonimu hizi zinatokana na nomino za kawaida za Kiswahili ambazo hurejelea mifugo kama vile: paka, ngo'ombe, sungura, mbwa, panya na mbuzi. Neno katika kikoa maana fulani huwa na uhusiano wa karibu kimaana na neno au maneno mengine katika kumbo, nyanja au eneo linalohusika (Massamba, 2004; Matinde, 2012). Uhusiano katika kikoa maana hiki ni kwamba nomino katika kikoa maana hiki ni za wanyama wanaofugwa.

**Jedwali 4.2: Kikoa Maana cha Mifugo**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijegwayo |
|---|---|
| **Paka** | *Kibaga/Kabaga* |
| **Ng'ombe** | *Ang'ombe* |
| **Sungura** | *Sungura/Kisungura* |
| **Mbwa** | *Kasimbwa/Isimbwa/Ambwa* |
| **Panya** | *Panya* |
| **Mbuzi** | *Amburi/Imburi* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.2 linaonyesha nomino 6 za kawaida za Kiswahili zinazotumika kujenga anthroponimu za Kimaragoli zilizobainishwa katika kikoa maana cha wanyama. Kipengele kilichozingatiwa katika ubainishaji huu ni maana ya kileksika (Wilson & Carston, 2007). Katika nadharia ya Pragmatiki Leksika kipengele hiki kinashughulikia uchunguzi na uchanganuzi wa maana kwa kuzingatia faridi leksika. Aidha, hushughulikia na kutalii mahusiano ya maana ya maneno katika lugha inayohusika (Wilson & Carston, 2007). Wasailiwa walithibitisha maana hii ya kileksika na kueleza kwamba paka (*Kibaga),* ng'ombe *(Ang'ombe),* sungura *(Kisungura),* panya (*Panya*), mbwa *(Kasimbwa)* na mbuzi *(Imburi)* ni mifugo na majina yao hupewa watu katika jamii ya Wamaragoli.

Licha ya kuwa Chahine (2017) katika Ndunge (2018) anasema kuwa maana ya animonimu huwa ni tabia za wanyama ambazo huhuishwa, inakisiwa kwamba animonimu zinaweza kujengwa katika mifumo ya lugha nyingine kama ilivyo kwa athroponimu za Kimaragoli

zinajengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Isitoshe, maana kileksika za anthroponimu za mifugo ni sifa za wanyama hao katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli. Kauli hii inakinzana na kutanua mawazo katika matokeo ya utafiti wa Batoma (2009) unaoeleza majina ya wanyama wanayopewa watu kuwa ni lakabu yenye sifa chanya kama vile ujasiri, utulivu, upole n.k. Hii ni kwa sababu katika utafiti huu suala la sifa za wanyama lilijitokeza katika zile nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli ila zilichanganyika zile hasi na chanya kwa mujibu wa wasailiwa. Isitoshe, anthroponimu hizo hazikuwa lakabu bali majina halisi ya Wamaragoli.

#### 4.2.1.2 Wanyama Mwitu

Wasailiwa walithibitisha uwepo wa anthroponimu za wanyama mwitu zilizokuwa kwenye Mwongozo wa Usaili waliposailiwa. Kwa mujibu ufafanuzi wa mhimili wa Semantiki Leksika (Wilson & Carston, 2007), maana ya msingi ya viumbe wanaorejelewa na nomino za kawaida za Kiswahili kwenye tapo hili ni wanyama mwitu. Kwa hivyo, kikoa maana kinachoundwa ni cha wanyama mwitu. Katika usaili wa baraza kuu la wazee Wamaragoli ilidokezwa kwamba:

> *… amita mala kuri Iswara, Gusimba, Ndovu/Endovu, Chura, Chui/Kachui, Riguruguru, Kenge, Ingwina, Ingamia ni mbiti na mita gi zinyama zyiu mmburimu. Nitari avandu vahevwa vuzwa mmborogori muno. (Baraza kuu la wazee Wamaragoli, Kikao cha kwanza, saa 10:00 asubuhi, 07/01/2021).*

Tafsiri:

> *Majina mengine kama vile Iswara (swara) Gusimba/Kasimba (simba), Endovu (ndovu), Chura (Chura), Chui/Kachui (chui), Riguruguru (guruguru), Kenge (kenge), Ingwina (ngwena) , Ing'amia (Ngamia) na Imbiti (mbiti) ni majina ya wanyama mwitu. Lakini watu wanapewa katika jamii hii. (Tafsiri Yetu)*

Majina haya ni nomino za kawaida zinazorejelea wanyama mwitu. Jedwali 4.3 hapa chini linawasilisha muhtasari wa kikoa maana cha majina ya wanyama mwitu:

**Jedwali 4.3: Kikoa Maana cha Wanyama Mwitu**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Swara** | *Iswara* |
| **Simba** | *Gusimba/Kasimba* |
| **Ndovu** | *Ndovu/Endovu* |
| **Chura** | *Chura* |
| **Chui** | *Chui/Kachui* |
| **Guruguru** | *Riguruguru* |
| **Kenge** | *Kenge* |
| **Ngwena** | *Ingwina* |
| **Ngamia** | *Ing'amia* |
| **Mbiti** | *Imbiti* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Maana ya kileksika inayojitokeza katika anthroponimu zilizoainishwa katika Jedwali la 4.3 ni kikoa cha wanyama mwitu. Wasailiwa walieleza kwamba kiasili jamii ya Wamaragoli ilizingirwa na kuishi kwenye mazingira ya miti mingi, vichaka na nyasi nyingi. Misitu yenyewe ilikuwa makazi walimoishi wanyama mwitu kama vile swara, simba, ndovu, chura, chui, guruguru, kenge, ngwena, ngamia, mbiti, n.k. Wakati mwingine wanyama hawa wangetoka mwituni kutafuta chakula na kisha kurejea huko. Nomino za kawaida 10 za Kiswahili zinazohusu wanyama mwitu zimechangia ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli. Ubainishaji wa kikoa hiki cha nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga athroponimu za Kimaragoli unaonesha ukweli wa kauli ya Mbiti (2011) kwamba watu hupewa majina ya wanyama mwitu. Hata hivyo, Mbiti hakuchunguza namna majina hayo yanavyojengwa katika mfumo wa lugha ya Kimaragoli.

Aidha, mawazo ya baraza kuu la wazee Wamaragoli yanatanua maoni ya Anudo (2017) anayesema kuwa watu hupewa majina ya wanyama kuficha maana ambayo ikitolewa wazi huenda ikawa na athari kubwa kuliko ilivyo anthroponimu yenyewe. Kwa mujibu wa wasailiwa, jamii ya wamaragoli hutumia majina hayo ili kuwasilisha ujumbe maalumu kwa jamii; suala linaloshabihiana na kauli ya Wilson na Carston (2007) kwamba faridi za kileksika za lugha huchanganuliwa na kufasiriwa kwa utaratibu kwa mujibu wa muktadha mahususi ya kijamii.

### 4.2.2 Kikoa Maana cha Ndege

Nomino 16 za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zilidhihirisha maana inayohusiana na ndege. Ndege ni kiumbe mwenye mbawa za kupaa na manyoya mwilini anayetega mayai; nyuni (TUKI, 2019: 477). Kutokana na usaili, imebainika kwamba nomino za kawaida za Kiswahili zinajenga anthroponimu za Kimaragoli zenye dhana ya ‘ndege’ kwa mujibu wa Semantiki Leksika. Hili linathibitisha kauli ya Dirk (2010) kwamba kikoa maana kinao uwezo wa kuibua vikoa vingine vidogo vidogo. Kwa hivyo, vikundi viwili vya ndege vinaainishwa katika nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli. Vikundi vyenyewe ni ndege wafugwao na ndege mwitu:

#### 4.2.2.1 Ndege Wafugwao

Ndege wafugwao ni nyuni wanaotunzwa na wanajamii nyumbani kwa ajili ya kuuzwa, vitoweo, mayai, manyoya au hata mapambo kwenye mandhari ya nyumbani. Katika jamii ya Wamaragoli, baadhi ya anthroponimu hujengwa kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili ambazo hutumika kuwatajia baadhi ya ndege hawa. Jedwali 4.4 hapa chini

linawasilisha kikoa maana cha ndege 5 wanaofugwa nyumbani kwa Wamaragoli pamoja na anthroponinu zinazojengwa kwa majina yao.

**Jedwali 4.4: Kikoa Maana cha Ndege Wafugwao**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Jogoo** | *Jogo* |
| **Kanga** | *Rikanga* |
| **Bata** | *Gubada/Bada* |
| **Tombo** | *Etombo* |
| **Tembe** | *Ketembe* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Maana msingi ya anthroponimu zilizoko katika Jedwali 4.4 ni nyuni, yaani kiumbe mwenye mabawa na manyoya anayeruka angani. Mbwanga (2010) anafafanua kuwa Semantiki Leksika hujishughulisha na vitengo vya maana kileksika vimwezeshavyo mzungumzaji wa lugha fulani kujifunza na kuongezea maneno mapya pamoja na maana zake kwa mfululizo maishani. Mawazo ya Wilson & Carston (2007) yanaelekea kushabihiana na kauli hii wanaposisitiza dhima ya maana kileksia ya neno. Katika tapo hili la kikoa cha ndege, maana ya kileksika iliyoongoza uainishaji huu ni ndege wanaofugwa nyumbani. Wasailiwa walithibitisha fasili za anthroponimu mbalimbali zijengwazo kwa majina ya ndege. Baraza la wazee Wamaragoli lilidhibitisha kuwa *Jogo* (jogoo), *Rikanga* (Kanga), *Bada* au *Gubada* (bata), *Etombo* (tombo) na *Ketembe* (tembe) ni anthroponimu za Kimaragoli.

Nomino za kawaida za Kiswahili katika kikoa hiki zinadhihirisha kuwa maana ipo katika muktadha wa jamii inayohusika. Uelewa wa maana ya anthroponimu hizi pia hutegemea ufahamu utamaduni, imani na shughuli nyinginezo za jamii inayohusika (Okyere, 2015). Ingawa utoaji majina huyachota majina yenyewe katika jamii inayohusika, anthroponimu hizi zinaweza kueleweka vyema zaidi kwenye hali na miktdha ya jamii inayohusika. Kwa sababu nadharia ya Pragmatiki Leksia husawiri uhusiano uhusiano uliopo kati ya lugha na miktadha ya matumizi yake, muktadha unaohusika aghalabu huchangia uteuzi na matumizi ya maneno kwenye tukio la mawasiliano pamoja welewa wa maana inayodokezwa (Wilson, 2003).

### 4.2.2.2 Ndege Mwitu

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazohusu ndege mwitu kama vile: mbuni, goregore, popo, bundi, karani, magamaga, mramba, mnandi, kadogo, kondekonde, na kadhalika pia huchangia ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli. Wasailiwa walithibitisha uwepo wa anthroponimu za Kimaragoli zinazotokana na majina ya ndege mwitu. Hata hivyo, hizi

nomino za kawaida zinapotumika kama anthroponimu za Wamaragoli, faridi za kileksika zenyewe hubanwa na kufasiriwa kulingana na muktadha wa jamii hii (Wilson & Carston, 2007). Orodha ya nomino za kawaida za Kiswahili 11 pamoja na anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwazo imewasilishwa kuwa ni kikoa maana cha ndege mwitu katika Jedwali 4.5 hapa chini:

**Jedwali 4.5: Kikoa Maana cha Ndege Mwitu**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Mbuni** | *Mbuni* |
| **Goregore** | *Goregore* |
| **Popo** | *Bobo* |
| **Bundi** | *Bundi* |
| **Barabara** | *Ibarabara* |
| **Karani** | *Karani* |
| **Magamaga** | *Maga* |
| **Mramba** | *Mramba* |
| **Mnandi** | *Mnandi* |
| **Kadogo** | *Kadogo/Kedogo/Mdogo* |
| **Kondekonde** | *Konde* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.5 linajumuisha anthroponimu ambazo maana yake msingi ni ndege mwitu. Data iliyokusanywa kwa upekuzi inaonyesha kwamba nomino za kawaida za Kiswahili za majina ya ndege huchangia katika ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli. Anthroponimu zenyewe ni *Mbuni* (mbuni), *Goregore* (goregore), *Bobo* (popo), *Bundi* (bundi), *Karani* (karani), *Maga* (magamaga), *Mramba* (mramba), *Mnandi* (mnandi), *Kadogo/Kedogo/Mdogo* (kadogo) na *Konde* (kondekonde). Pamoja na kuthibitisha uwepo wa anthroponimu za aina hii, usaili wa Baraza la wazee Wamaragoli ulihusisha chanzo cha matumizi ya anthroponimu hizi na shughuli za uchumaji na uwindaji kwenye jamii hii. Baadhi ya anthroponimu zilitokana na majina ya ndege mwitu waliowindwa ilhali zingine zilitokana na migusano baina ya Wamaragoli na lugha za jamii nyinginezo. Licha ya kuafikiana na wazo la Agyekum (2006) kwamba majina yanayotolewa kwenye jamii fulani aghalabu hutokana na dhana, hali au vitu vinavyoonekana au kupatikana katika mazingira yao, imethibitika pia kwamba baadhi ya anthroponimu zinaweza kujengwa kutokana na majina ya vitu visivyokuwepo wala kuonekana miongoni mwa wanajamii wanaohusika.

Kwa ujumla, maana ya anthroponimu za Kimaragoli katika kikoa maana cha ndege inaakisi maoni ya Sommer & Sommer (2015) wanafafanua kwamba anthroponimu zinazotokana na majina ya ndege aghalabu husawiri picha hasi kuhusu watu kwa sababu nyingi huwa

humwonyesha mtu kama kiumbe mwenye maringo, tamaa, anayependa kupiga kelele, n.k. Usaili wa Baraza la wazee Wamaragoli unashadidia utokezaji wa sifa linganifu katika anthroponimu za Kimaragoli zilizoainishwa kwenye kikoa maana hiki. Nyingi katika anthroponimu zilizokusanywa kwa upekuzi wa sajili za hospitalini na kisha kuthibitishwa kwenye usaili zinakisi maana hasi katika jamii ya Wamaragoli.

Ulinganishi wa tabia za binadamu na ndege hudhihirisha kuwa wapo ndege kama vile bata wanaoashiria upole, njiwa anayeashiria amani na kuku anayeashiria upendo (Sommer & Sommer, 2015). Baadhi ya hizi sifa chanya hupelekea watu kupewa majina ya ndege hao kimajazi. Hata hivyo, hizi sifa chanya hazijitokeza katika anthroponimu za Wamaragoli zinazojengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili. Badala yake, sifa hasi ndizo zinazojitokeza sawia na lakabu za jamii ya Kabre ncnini Togo (Batoma, 2009). Kinachotofautisha sifa hizo ni kwamba katika jamii ya Kabre ni za kilakabu ilhali kwenye muktadha wa jamii ya Wamaragoli ni maana msingi. Kwa hivyo, imethibitika kwamba ufasiri wa jina au tamko umebanwa kuliko ilivyodhaniwa (Wilson & Carston, 2007).

### 4.2.3 Kikoa Maana cha Mimea na Viungo

Mmea umefasiliwa kuwa ni kitu chenye uhai ambacho kina majani, shina na mzizi aghalabu chenye rangi ya kijani kinachoota kutokana na chembe, mbegu au tawi (TUKI, 2019: 413). Nomino za kawaida za Kiswahili 17 zinazojenga anthroponimu za Wamaragoli zilizopekuliwa zilidhihirisha mimea na viungo mbalimbali. Usaili wa baraza la wazee ulidhibitisha uwepo wa anthroponimu aina hii katika jamii ya Wamaragoli. Ilifafanuliwa kwamba, katika jamii hii watu hupewa anthroponimu zinazotokana na nomino za kawaida za mboga mbalimbali katika Kiswahili. Nomino za kawaida zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zenkatika kikoa cha mboga na viungo zinaoneshwa kwa muhtasari katika Jedwali 4.6 lifuatalo:

**Jedwali 4.6: Kikoa Maana cha Mboga na Viungo**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Kitunguu** | *Kitunguru* |
| **Kabeji** | *Rikabichi/Makabichi* |
| **Sukuma wiki** | *Risuguma* |
| **Nyanya** | *Inyanya* |
| **Pilipili** | *Birabiri* |
| **Dania** | *Idania* |
| **Hoho** | *Ehoho/Hoho* |
| **Chumvi** | *Ijumbi/Kajumbi* |
| **Sukari** | *Isukari* |
| **Majani** | *Majani* |
| **Mafuta** | *Maguta/ Riguta* |
| **Bizari** | *Vinzari* |
| **Masala** | *Masala* |
| **Tangawizi** | *Dangavusi* |
| **Dalasini** | *Mdalasini* |
| **Mboga** | *Amboga/ Zimboga* |
| **Ndimu** | *Indimu* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Maana ya kileksika katika anthroponimu hizi ilikuwa mmea ambao unatumika kama mboga au kiungo. Matumizi ya anthroponimu zilizonyeshwa katika Jedwali 4.6 yalihakikishwa katika usaili wa baraza la wazee Wamaragoli. Anthroponimu zilizokusanywa kwa upekuzi ni pamoja na: *Kitunguru* (kitunguu), *Rikabichi* (kabeji), *Risuguma* (sukumawiki), *Inyanya* (nyanya), *Birabiri* (pilipili), *Idania* (dania) na *Ehoho* (hoho), *Ijumbi* (chumvi), *Isukari* (sukari), *Majani* (majani), *Maguta/Riguta* (mafuta), *Vinzari* (bizari), *Masala (*masala*),* *Dangavusi* (tangawizi), *Mdalasini* (dalasini), *Amboga* au *Zimboga (*mboga) na *Indimu* (ndimu). Kinachoibuka katika matokeo ya kikoa hiki kinakinzana na wazo kwamba majina ya mimea hutumika tu kama lakabu miongoni mwa wanajamii (Pais, 2018). Imethibitika kwamba majina ya mboga na viungo hayatumiki kama lakabu bali ni majina miongoni mwa jamii ya Wamaragoli. Kwa sababu nadharia ya Pragmatiki Leksika inahoji kuwa nia ya mtoa ujumbe huathiri uteuzi wa maneno kwenye muktadha mahususi, maana inayowasilishwa anthroponimu za Kimaragoli zinazotokana na majina ya mboga na viungo inaweza kueleweka vizuri kwenye muktadha wa jamii hii.

### 4.2.4 Kikoa Maana cha Vyakula na Vinywaji

Chakula ni kitu chochote kinacholiwa ambacho huupatia mwili nguvu. Vinywaji navyo ni vitu vioevu vinavyonywewa na binadamu. Data iliyopatikana kwa upekulizi maktabani na kuthibitishwa katika sajili za wagonjwa hospitalini ilidhihirisha nomino za kawaida za

Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zilizoorodheshwa kwenye Jedwali 4.7 lifuatalo:

**Jedwali 4.7: Kikoa Maana cha Vyakula na Vinywaji**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu inajengwayo |
|---|---|
| **Mkate** | *Mugadi* |
| **Soda** | *Soda* |
| **Njugu** | *Injugu* |
| **Andazi** | *Riandasi* |
| **Chapati** | *Chabati* |
| **Sima** | *Vuchima* |
| **Chai** | *Ichai/Ijayi* |
| **Supu** | *Subu* |
| **Nyama** | *Anyama/ Gunyama/ Kanyama* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.7 linaonyesha nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli katika kikoa maana cha vyakula na vinywaji. Kwa mujibu wa semantiki kileksika, maana ya kileksika ya nomino katika kikoa maana hiki ni ‘chakula au kinywaji.’ Yaani, vitu viliwavyo au kunywewa ili mwili upate nguvu, ndio wavu unaojenga mahusiano ya kifahiwa (Lyons, 1998). Usaili wa wazee ulithibitisha matumizi ya nomino hizi za kawaida kama anthroponimu katika jamii ya Wamaragoli. *Ichai au Ijayi* (chai), *Subu* (supu) na *Soda* (soda) ni anthroponimu zinazorejelea vinywaji ilhali *Mugadi* (mkate), *Injugu* (njugu), *Riandasi* (andazi), *Chabati* (chapati), *Vuchima* (sima) na *Anyama/ Gunyama/ Kanyama* (nyama) ni anthroponimu zinazotokana na vyakula viliwavyo miongoni mwa wanajamii hii.

Uainishaji wa kikoa maana hiki unatanua mawazo ya Halliday & Clemmer (1940) wanaoainisha msimbo wa lugha ya wafungwa katika magereza yote Marekani. Msimbo wenyewe unajumuisha vikoa maana vya ngono na mapenzi, sehemu za mwili, maelezo kuhusu wengine, pombe na dawa za kulevya pamoja na msimbo unaohusu jela na matusi. Ingawa nao wanaainisha kikoa maana cha pombe ambacho ni sehemu ya vinywaji, data ya nomino za kawaida za Kiswahili zilizokusanywa katika kikoa hiki zinajumuisha vyakula na vinywaji vinavyochaingia faridi za kileksika zitumikazo kwenye muktadha wa jamii kujenga anthroponimu. Tofauti kati ya tafiti hizi mbili ni kwamba mmoja unachunguza msimbo katika magereza ilhali mwingine unazamia matumizi yanomino za kawaida za Kiswahili katika ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli.

### 4.2.5 Kikoa Maana cha Vifaa

Kifaa ni zana, kitu au chombo kinachotumika katika kufanyia kazi au kutekelezea shughuli fulani (TUKI, 2019: 249). Nomino za kawaida 43 za Kiswahili zilizokusanywa kwa upekuzi maktabani na kuthibitishwa kwenye sajili za majina hospitalini pamoja na usaili uliohusisha baraza la wazee Wamaragoli zinadhihisha majina ya vifaa mbalimbali. Usaili wa wazee ulifanikisha uainishaji wa kikoa maana cha vifaa kwenye makundi madogo kama vile: vyombo vya usafiri (6), vyombo vya matumizi jikoni (14) na vifaa vya ujenzi (23). Hali inayoshadidia wazo la Dirk (2010) kwamba kikoa maana kina uwezo wa kuibua vikoa maana vingine vidogo vidogo.

#### 4.2.5.1 Vyombo vya Usafiri

Vyombo vya usafiri ni vifaa vya uchukuzi wa watu, vitu na mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Vyombo vya usafiri wa angani (ndege), barabarani katika nchi kavu (baiskeli, gari, trekta na lori) pamoja na chombo kimoja cha usafiri baharini (meli) ndivyo vilivyopatikana kuhusika katika uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli. Imedhahirika kwamba nomino mkopo za kawaida za vyombo vya kisasa vya usafiri ndizo zilizothibitika kuhusika katika ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli. Jedwali 4.8 hapa chini linawasilisha data hii.

**Jedwali 4.8: Kikoa Maana cha Vyombo vya Usafiri**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Ndege** | *Endege* |
| **Baiskeli** | *Ibaiskili/Ibasikeli* |
| **Gari** | *Kagari* |
| **Meli** | *Emeri* |
| **Trekta** | *Kiragita* |
| **Lori** | *Erori* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Kwa mujibu wa Jedwali 4.8 nomino za kawaida 6 za Kiswahili zinazorejelea vifaa vya usafiri na ambazo zinatumika kama athroponimu katika jamii ya Wamaragoli ni: *Endege* (ndege), *Ibaiskili* au *Ibaiskeli* (baiskeli), *Kagari* (gari*)*, *Emeri* (meli), *Kiragita* (trekta) na *Erori* (lori). Nomino hizi pamoja na anthroponimu zinazojengwa kwazo zimeorodheshwa katika Jedwali 4.8. Matokeo haya yanatofautiana na uainishaji wa wa majina katika jamii ya Wakamba ambao haubainishi anthroponimu zinazotokana na vyombo vya usafiri (King'ei & Kisovi, 2005). Ilifafanuliwa katika usaili wa wazee kwamba baadhi ya watu waliopewa anthroponimu hizo walizaliwa ndani ya vyombo hivyo. Kina mama kujifungua kwenye

vyombo vya usafiri wakipelekwa hospitalini lilikuwa jambo la kawaida. Aidha, baadhi ya anthroponimu hizi zilitumika kuhifadhi tukio la kihistoria kama vile mara ya kwanza chombo hicho cha usafiri kufika, kutumika au hata kununuliwa na kumilikiwa kwenye maeneo ya jamii hii au familia ya Kimaragoli inayohusika.

#### 4.2.5.2 Vyombo vya Matumizi Jikoni

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazorejelea vyombo vya matumizi jikoni pia zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli katika kikoa maana cha vifaa vya matumizi katika jamii. Kati ya anthroponimu zilizokusanywa kwa upekuzi wa sajili ya hospitali, 14 zilizoainishwa katika Jedwali 4.9 zipo katika kikoa maana cha vyombo vya matumizi jikoni.

**Jedwali 4.9: Kikoa Maana cha Vyombo vya Matumizi Jikoni**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Sahani** | *Sahani* |
| **Kijiko** | *Kijiko/Gujiko/Kajiko* |
| **Kikombe** | *Kekombe /Kakombe* |
| **Birika** | *Biniga /Kabiniga* |
| **Kikapu** | *Kikabo* |
| **Ndoo** | *Endoho* |
| **Mtungi** | *Mtunji* |
| **Bakuli** | *Ibakuli/ Kibakuli* |
| **Kibuyu** | *Kibuyi* |
| **Mafiga** | *Mahiga* |
| **Uma** | *Vyuma/Gwuma* |
| **Kinu** | *Kinu* |
| **Jiko** | *Majiko/Rijiko* |
| **Debe** | *Madebe/Godebe/ Kadebe/Ebede* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Kwa mujibu wa mhimili wa semantiki kileksika, anthroponimu zilizopo katika Jedwali 4.9 zinawasilisha maana msingi ya ‘vyombo vya matumizi jikoni.’ Jamii ya Wamaragoli huvitumia vifaa hivi kutekeleza shughuli mbalimbali jikoni. Hata hivyo, ni bayana kwamba majina mengi katika kikoa maana hiki yanarejelea vyombo vya kisasa; majina ya vyombo vya zamani au vya kiasili katika jamii havijatumika kujenga anthroponimu. Usaili wa wazee lithibitisha haya matumizi ya majina ya vyombo hivi katika anthroponimu kama vile *Sahani* (sahani), *Kijiko/Gujiko/kajiko* (kijiko), *Kekombe/Kakombe* (kikombe), *Biniga/Kabiniga* (birika), *Kikabo* (kikapu), *Endoho* (ndoo), *Mtunji* (mtungi), *Kibakuli* au *Ibakuli* (bakuli), *Kibuyi* (kibuyu), *Mahiga* (mafiga), *Vyuma/Gwuma* (uma), *Kinu* (kinu), *Majiko* au *Rijiko* (jiko) na *Godebe/Kadebe/Edebe/Madebe* (debe). Ilielezwa kwamba baadhi ya watu hupewa anthroponimu kutegemea sifa au tabia inayoendana na chombo cha matumizi jikoni. Ingawa

Sitati (2007) anahusisha chanzo cha anthroponimu na vitu au vyombo vipatikanavyo katika mazingira yanayoizunguka jamii inayohusika, data iliyochanganuliwa inaonesha kwamba majina ya vyombo vinavyohusika katika ujenzi wa anthroponimu yanaweza yakawa ya lugha nyingine.

#### 4.2.5.3 Vifaa vya Ujenzi

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazotumika kutajia vifaa vinavyofanikisha kazi au shughuli mbalimbali za ujenzi pia ni chanzo muhimu cha anthroponimu za Kimaragoli. Nomino 21 zilizodhihirisha maana kileksika za vifaa vya ujenzi zimewasilishwa katika Jedwali 4.10 hapa chini.

**Jedwali 4.10: Kikoa Maana cha Vifaa vya Ujenzi**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Tarimbo** | *Mudalimbo/Midalimbo* |
| **Msumeno** | *Musumeno* |
| **Chuma** | *Kichuma/Vichuma* |
| **Msumari** | *Musumari/Misumari* |
| **Kabiro** | *Ikabiro* |
| **Gamu** | *Agamu* |
| **Panga** | *Lubanga* |
| **Simiti** | *Simidi* |
| **Tupa** | *Ituba* |
| **Rangi** | *Iranji* |
| **Brashi** | *Vurasi* |
| **Kokoto** | *Zikokoto* |
| **Mpini** | *Muhini* |
| **Nyundo** | *Inyundu* |
| **Randa** | *Iranda/ Ziranda* |
| **Ngazi** | *Ingasi* |
| **Cherehani** | *Cherehani* |
| **Chapi** | *Vujabi* |
| **Mchanga** | *Mchanga* |
| **Kamba** | *Ikamba* |
| **Mabati** | *Mabadi* |
| **Waya** | *Ruwaya* |
| **Sindano** | *Sindani* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali la 4.10 linawasilisha orodha ya nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli. Maana ya kileksia ya nomino zinazoainishwa katika kikoa hiki ni, ‘vifaa vya ujenzi.’ Usaili wa wazee ulithibitisha uwepo wa anthroponimu za Kimaragoli zilizoakisi majina ya vifaa anuwai vya ujenzi. Anthroponimu kama vile *Mudalimbo/Midalimbo* (tarimbo), *Musumeno* (msumeno), *Kichuma/Vichuma* (chuma),

*Musumari/Misumari* (msumari), *Agamu* (gamu), *Lubanga* (panga), *Simidi* (simiti), *Iranji* (rangi), *Vurasi* (brashi), *Zikokoto* (kokoto), *Muhini* (mpini), *Inyundu* (nyundo) na *Iranda* (randa), *Ingasi* (ngazi), *Cherehani* (cherehani), *Vujabi* (chapi), *Mchanga* (mchanga), *Ikamba* (kamba), *Mabadi* (mabati), *Ruyawa* (waya) na *Sindani* (sindano) zilitajwa. Anthroponimu hizi hupewa wahusika kusawiri namna wanavyotegemewa. Yaani, dhima yao katika jamii inayohusika ni kuafiki mshikamano au ukuaji wake. Kikoa hiki kinaashiria kwamba anthroponimu za jamii fulani zinaweza kuchukuwa mielekeo inayotofautiana na ile iliyozoeleka kama vile nyakati, majira na sura (Kihore na wenzie, 2009). Ingawa mielekeo inayochukuliwa katika utoaji wa majina haikushughulikiwa, suala la lugha moja kuchangia ujenzi wa anthroponimu katika lugha nyingine linadhihirisha mwelekeo tofauti wa kutalii suala la uainishaji na maana ya majina kwa ujumla.

### 4.2.6 Kikoa Maana cha Elimu

Elimu ni taaluma inayopatikana kwa kujifunza au kufundishwa. Miongoni mwa nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli, 12 zilizopatikana kwa upekuzi wa sajili za hosipitali zilidhihirisha maana ya kileksia inayohusiana na 'taaluma ya elimu.' Ufafanuzi wa vikao vya usaili ulithibitisha uwepo wa anthroponimu zinazowasilisha maana ya taaluma ya elimu au ufunzaji na ujifunzaji. Muhtasari wa data hii umewasilishwa katika Jedwali 4.11 lifuatalo:

**Jedwali 4.11: Kikoa Maana cha Elimu**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Fomu** | *Ifomu* |
| **Kitambaa** | *Kitambaya* |
| **Ubao** | *Rubaho* |
| **Kalamu** | *Ikaramu* |
| **Penseli** | *Epenzo* |
| **Kitabu** | *Kitabu/Matabu* |
| **Masomo** | *Masomo/Amasomo* |
| **Baraza** | *Ibarasa* |
| **Hisabati** | *Isabu* |
| **Sayansi** | *Sayanzi* |
| **Kengele** | *Egengere* |
| **Namba** | *Inamba* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.11 linaonyesha nomino 12 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli katika kikoa maana cha taaluma ya elimu. Usaili ulithibitisha uwepo wa matumizi ya anthroponimu kama vile *Ifomu* (fomu), *Kitambaya* (kitambaa), *Rubaho* (ubao),

*Ikaramu* (kalamu), *Epenzo* (penseli), Ibarasa (baraza), *Kitabu* (kitabu), *Masomo* (masomo), *Isabu* (hisabati), *Sayanzi* (sayansi), *Egengere* (kengele) *na Inamba* (namba).

Kama inavyosisitiza nadharia ya Pragmatiki Leksia, fasili ya kikoa maana cha elimu inatokana na muktadha wa matumizo katika jamii hii. Nomino za kawaida za Kiswahili zinazohusiana na taaluma ya elimu ndizo zinatumika kujenga anthroponimu za Kimaragoli. Ingawa naye pia amejishughulisha na kikoa maana cha elimu, Mugambi (2007) anaainisha leksimu kama vile *bayo*, *kem*, *fizo* na *swa* katika msimbo wa Sheng'. Isitoshe, leksimu hizi hazihusishwi na ujenzi wa anthroponimu zozote.

### 4.2.7 Kikoa Maana cha Samani

Samani ni fenicha au vyombo vya nyumbani kama vile meza, viti, kabati, au kitanda. Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga athroponimu za Kimaragoli zenye maana kileksia ya samani kwenye muktadha wa jamii ya Wamaragoli zimeainishwa katika kikoa maana hiki. Nomino zenyewe zimeorodheshwa katika Jedwali 4.12 lifuatalo:

**Jedwali 4.12: Kikoa Maana cha Samani**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijegwayo |
|---|---|
| **Kitanda** | *Kitanda* |
| **Meza** | *Emesa* |
| **Benchi** | *Ebenji* |
| **Kabati** | *Ikabati* |
| **Mlango** | *Muriango* |
| **Dirisha** | *Madirisa* |
| **Kibago** | *Lubago* |
| **Bakora** | *Ibagora* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Maana msingi inayowasilishwa na kikoa maana kwenye Jedwali 4.12 ni samani. Usaili ulithibitisha matumizi ya nomino hizi 8 za kawaida za Kiswahili kwenye ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli. Ilisadikika kwamba *Kitanda* (kitanda), *Emesa* (meza), *Ikabati* (kabati), *Muriango* (mlango), *Madirisa* (madirisha), *Lubago* (Kibago) na *Ibagora* (bakora) ni anthroponimu katika jamii hii. Maana ya kikoa maana hiki kwenye muktadha huu kileksia ni samani, hoja inayothibitisha ukweli katika kauli ya Wilson (2003; 2012) katika nadharia ya Pragmatiki Leksia. Uainishaji wa kikoa hiki unadhihirisha kuwa anthroponimu zinaweza kujengwa kutokana na samani wala sio lakabu pekee kama anavyodai Okal (2012). Kinachofanyika hapa ni kwamba nomino za kawaida zinatumika kujenga anthroponimu ambazo hutumiwa katika maisha ya kila siku miongoni mwa Wamaragoli. Hata hivyo,

matumizi ya agoti zinazohusiana na samani kama vile *kumbao, kupiga bakora, chini ya meza, toa fomu,* n.k. yameonyeshwa kusimba ujumbe au kuficha siri miongoni mwa wafungwa wanapowasiliana gerezani (Okoth, 2019).

### 4.2.8 Kikoa Maana cha Magonjwa

Ugonjwa au ndwele ni kitu kinachosababisha mtu, mmea au mnyama kuwa katika afya mbaya (TUKI, 2019: 671). Katika nomino za kawaida za Kiswahili zilizokusanywa kwa upekuzi wa vitabu, 10 za magonjwa zilithibitishwa kutumika katika ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli zilizokusanywa kutokana na sajili za wagonjwa hospitalini. Baadhi ya nomino hizi ziligunduliwa kuakisi maradhi mbalimbali yanayoathiri watu katika jamii hii. Nominoza kawaida za Kiswahili pamoja na anthroponimu za Kimaragoli zilizothibitishwa kwenye usaili wa baraza la wazee zinawasilishwa katika Jedwali 4.13 hapa chini.

**Jedwali 4.13: Kikoa Maana cha Magonjwa**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijegwayo |
|---|---|
| **Malaria** | *Mareria* |
| **Kisonono** | *Kisununu* |
| **Homa** | *Zihoma* |
| **Mdondo** | *Mudondo* |
| **Kifafa** | *Kifafa* |
| **Anemia** | *Nemia/Gonemia* |
| **Kiungulia** | *Kirungula* |
| **Nimonia** | *Nimonia* |
| **Chunusi** | *Yunusi* |
| **Kaswende** | *Igaswende* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.13 linaonyesha nomino 10 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli. Maana msingi ya nomino zipatikazo katika kikoa maana hiki ni, ‘maradhi, uele au ukongo.’ Anthroponimu za aina hii zilitambuliwa katika usaili wa wazee. Ilifafanuliwa kwamba watu hupewa anthroponimu zinazohusiana na ugonjwa ulioowahi kuzuka katika jamii hii. Anthroponimu za aina hii zilizopewa Wamaragoli ni pamoja na: *Mareria* (malaria), *Kisununu* (kisonono), *Zihoma* (homa), *Mudondo* (mdondo), *Kifafa* (kifafa), *Gonemia/Nemia* (Anemia), *Kirungula* (kiungulia), *Nimonia* (nimonia), *Yunusi* (chunusi) na *Igaswende* (kaswende).

Uanishaji wa anthroponimu katika kikoa maana hiki unaafikiana na dai la King’ei na Kisovi (2005) kwamba majina ya watu yanaweza kutokana na matukio fulani katika jamii. Kwa mujibu wa wasailiwa baadhi ya maradhi yanayohusishwa na anthroponimu yalikuwa

yanazuka na kudhibitiwa au kupotea baada ya kipindi fulani. Licha ya milipuko ya magonjwa haya kuchangia onomastiki ya jamii hii, imethibitika kwamba anthroponimu zenyewe zilijengwa kutokana nomino za kawaida za Kiswahili wala sio msamiati asili wa Kimaragoli. Mathalan, anthroponimu *Kifafa* (kifafa) inatumika wa sio *Indurumi*, anthroponimu ambayo tungetarajia itokane na nomino ya kawaida ya Kimaragoli inayorejelea ugonjwa huo.

#### 4.2.9 Kikoa Maana cha Viungo vya Mwili

Majina ya sehemu za mwili wa binadamu pia huchangia uundaji wa anthroponimu. Mwili wa binadamu una viungo mbalimbali. Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zilidhihirisha maana kileksika ya viungo mbalimbali vya mwili wa binadamu. Anthroponimu zilizojengwa kwa utaratibu huu zilithibitishwa na usaili wa wazee kutumika katika jamii hii. Nomino 7 pamoja na anthroponimu za Kimaragoli zinazohusika zinawasilishwa katika Jedwali 4.14 lifuatalo:

**Jedwali 4.14: Kikoa Maana cha Viungo vya Mwili**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijegwayo |
|---|---|
| **Mikono** | *Rokono/ Makono / Akekono/ Mkono* |
| **Mabega** | *Rivega/ Mavega* |
| **Mgongo** | *Amugongo* |
| **Mbavu** | *Tsimbaru* |
| **Magoti** | *Magoti/ Kagoti* |
| **Meno** | *Ameno/Omeno* |
| **Moyo** | *Umwoyo* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Anthroponimu za Kimaragoli zilizoonyeshwa katika Jedwali 4.14 zinadhihirisha maana kileksika ya viungo vya mwili wa binadamu. Nomino 7 za kawaida za Kiswahili zenye maana msingi ya ‘viungo vya mwili’ ndizo zilizotumika katika ujenzi wa anthroponimu kama vile: *Rokono/Makono/Akekono/Amkono* (mikono), *Rivega/Mavega* (mabega), *Amugongo* (mgongo), *Tsimbaru* (mbavu) na *Magoti/Kagoti, (*magoti*) Omeno/Ameno (*meno*)* na *Umwoyo* (moyo).

Vinginevyo, nomino za kawaida zinazorejelea sehemu za mwili aghalabu hutumiwa kama matusi katika lakabu au majina ya kimajazi yanayopewa askarijela na wafungwa magerezani (Okoth, 2019). Hata hivyo, imeonyeshwa namna ambavyo anthroponimu zinaweza kujengwa kutokana na majina ya viungo vya mwili na kukubalika rasmi kama majina ya watu. Pamoja na haya, anthroponimu zinazohusika zimejengwa kwa nomino za kawaida za Kiswahili.

Uainishaji wa kikoa maana cha viungo vya mwili unalandana na uanishaji wa msimbo wa wafungwa katika magereza ya Marekani (Halliday & Clemmer, 1940).

### 4.2.10 Kikoa Maana cha Jamii na Utaifa

Katika kikoa maana cha jamii na utaifa, nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zinadhihirisha maana ya kileksia ya jamii, taifa au utaifa. Uwepo wa anthroponimu za aina hii ulithibitishwa na usaili wa baraza la wazee uliofafanua kwamba Wamaragoli huwapa watu majina ya majirani au marafiki zao kutoka jamii, utaifa au mataifa wanayojinasibisha nayo. Majina yenyewe yanaweza yakahusu jamii, utaifa au mataifa yanayohusika kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 4.15 lifuatalo:

**Jedwali 4.15: Kikoa Maana cha Jamii na Utaifa**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Mganda** | *Muganda* |
| **Mhindi** | *Mhindi* |
| **Mwitaliano** | *Idalia* |
| **Mswahili** | *Swairi* |
| **Mtaita** | *Mdaida* |
| **Mwingereza** | *Mungeresa/Ngereso* |
| **Mjerumani** | *Njirimani* |
| **Mzungu** | *Musungu/ sungu/ Kasungu* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.15 linaonyesha anthroponimu 8 zilizoundwa kwa nomino za kawaida ambazo maana yake msingi ni jamii, utaifa au taifa. Usaili ulibainisha kwamba chanzo cha anthroponimu *Muganda* ni nchi ya Uganda, *Muhindi* asili ya Hindi, *Idalya* asili yake nchi ya Italia, *Swairi* asili yake Uswahilini, *Mudaida* kutoka jamii ya Taita, *Ngereso/Mungeresa* ni Mwingereza kutoka Uingereza, *Njirimani* kutoka taifa la Ujerumani, kisha *Musungu/Sungu/Kasungu* kutoka uzunguni.

### 4.2.11 Kikoa Maana cha Mavazi

Vazi au libasi ni chochote ambacho huvaliwa kusitiri uchi au kwa minajili ya kujipamba. Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu zilithibitishwa na baraza la wazee Wamaragoli kuwa zina maana kileksika ya ‘mavazi’ na kuainishwa katika kikoa hiki. Majina ya mavazi yalibainishwa kutumiwa na jamii ya Wamaragoli kuhifadhi historia fulani. Nomino 13 zilizoainishwa katika kikoa maana hiki zimeorodheshwa sambamba na anthroponimu zinazojengwa kwazo katika Jedwali 4.16 lifuatalo:

**Jedwali 4.16: Kikoa Maana cha Mavazi**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Kanzu** | *Iganza* |
| **Kiatu** | *Kirato* |
| **Shati** | *Isadi* |
| **Kofia** | *Egofya* |
| **Kikoi** | *Kekoyi* |
| **Sanda** | *Sanda* |
| **Leso** | *Mareso /Aleso* |
| **Juba** | *Juba* |
| **Kilemba** | *Keremba* |
| **Kitenge** | *Ketenga* |
| **Suti** | *Isuti* |
| **Koti** | *Irikoti/ Gokoti* |
| **Suruali** | *Isuari/ Zisuari* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.16 linaonyesha nomino 13 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli. Maana zake ya msingi ni vazi, nguo au libasi. Anthroponimu *Iganza* (kanzu), *Kirato* (kiatu), *Isadi* (shati), *Egofya* (kofia), *Kekoyi* (kikoi), *Sanda* (sanda), *Aleso/Mareso* (leso), *Juba* (juba), *Keremba* (kilemba), *Ketenga* (kitenge), *Isuti* (suti), *Irikoti/ Gokoti* (koti) na *Isuari*/ *Zisuari* (suruali) zinajengwa na nomino za kawaida za Kiswahili ambazo zina uhusiano wa kileksika. Mahusiano haya ya kisemantiki yanachangia kuziainisha nomino hizi katika kokoa maana cha mavazi (Lyons, 1981).

### 4.2.12 Kikoa Maana cha Majira/Wakati

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zinadhihirisha maana kileksika ya majira au wakati katika muktadha wa jamii hii. Nomino hizi ni Zimeorodheshwa katika Jedwali 4.17 hapa chini:

**Jedwali 4.17: Kikoa Maana cha Majira/Wakati**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Saa** | *Zisaa* |
| **Saa moja** | *Samoja* |
| **Saa mbili** | *Sambiri* |
| **Saa tatu** | *Satatu* |
| **Saa nne** | *Saine* |
| **Saa tatu** | *Satano* |
| **Saa sita** | *Sasita* |
| **Saa saba** | *Sasaba* |
| **Saa nane** | *Sanane* |
| **Saa tisa** | *Satisa* |
| **Saa kumi** | *Sakomi* |
| **Mweri** | *Mweri* |
| **Mwaka** | *Mwaka* |
| **Asubuhi** | *Asubui* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Nomino 14 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zimeorodheshwa katika Jedwali 4.17. Maana msingi inayowasilishwa na nomino hizi ni wakati, majira au njeo. Uwepo wa anthroponimu hizi katika jamii ya Wamaragoli ulithibitishwa wasailiwa walipofafanua kwamba baadhi ya watu walipewa majina kuakisi nyakati, wakati au majira walipozaliwa. Athroponimu zenyewe ni pamoja na *Zisaa* (saa), *Samoja* (saa moja), *Sambiri* (saa mbili), *Satatu* (saa tatu), *Saine* (saa nne), *Satano* (Saa tano), *Sasita* (saa sita), *Sasaba* (saa saba), *Sanane* (saa nane), *Satisa* (saa tisa), *Sakomi* (Saa kumi), *Mweri* (mwezi), *Muaka* (mwaka) na *Asubui* (asubuhi).

Tafiti za zinazojishughulisha na utoaji wa majina zimeonyesha kwamba watu hupewa majina kutokana na siku waliyozaliwa, mwaka, mwezi, nyakati na majira (King'ei & Kisovi, 2005; Sitati, 2007 ; na Odesanya na wenzake, 2017 ). Ingawa matokeo ya utafiti huu yanaakisi tafiti hizo, tofauti ni kwamba anthroponimu za ya Kimaragoli hujengwa moja kwa moja kutokana na saa na/au nyakati mbalimbali zinazorejelewa na nomino za kawaida za Kiswahili.

#### 4.2.13 Kikoa Maana cha Silaha

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zinadhihirisha maana kileksika ya silaha katika muktadha wa jamii hii. Nomino zinazohusika Zimewasilishwa katika Jedwali 4.18 hapa chini:

**Jedwali 4.18: Kikoa Maana cha Silaha**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Bunduki** | *Bunduji* |
| **Ngao** | *Ingavo* |
| **Bomu** | *Ebomu/Libomu* |
| **Risasi** | *Masasi/Amasasi* |
| **Uta** | *Vuta* |
| **Kifaru** | *Ikifaru* |
| **Sumu** | *Asumu* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.18 linabainisha nomino 7 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zenye maana msingi ya silaha. Kwa mujibu wa usaili wa baraza kuu la wazee, Wamaragoli huwapa watoto anthroponimu zitokanazo na majina ya silaha. Anthroponimu zenyewe ni *Bunduji* (bunduki), *Ingavo* (ngao), *Ebomu/ Libomu* (bomu), *Amasasi/Masasi* (risasi), *Vuta* (uta), *Kifaru* (kifaru) na *Asumu* (sumu).

Ijapokuwa vigezo vya utoaji majina anavyoainisha Okal (2012) kama vile matukio maalumu, misimu, mahali alikozaliwa mtoto, tabia, n.k. havikushughulikiwa moja kwa moja,

imethibitika kwamba jamii ya Wamaragoli huwapa watoto anthroponimu zenye maana kisemantiki ya silaha kama ukumbusho wa hali fulani iliyotokea. Usaili ulifafanua kwamba anthroponimu za silaha zilitokana hali tete iliyosababisha maafa, majonzi au mauko. Aidha, utoaji wa anthroponimu yenye maana ya silaha ulitokana na matumizi ya silaha hiyo mtoto anayehusika alipozaliwa.

### 4.2.14 Kikoa Maana cha Wadudu

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zinadhihirisha maana kileksika ya wadudu katika muktadha wa jamii hii. Nomino zenyewe pamoja na anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kwazo zimeorodheshwa katika Jedwali 4.19 lifuatalo:

**Jedwali 4.19: Kikoa Maana cha Wadudu**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Kiroboto** | *Keromboto* |
| **Nzi** | *Anji* |
| **Mende** | *Omende/Amende/Mende* |
| **Nyuki** | *Nzuki* |
| **Nzige** | *Isigi* |
| **Kimulimuli** | *Kimulimuli* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.19 linabainisha nomino 6 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli. Maana ya kisemantiki ya nomino zinazoainishwa katika kikoa maana hiki ni wadudu. Uwepo wa majina kama vile *Keromboto* (kiroboto), *Anji* (nzi), *Omende/Amende/Mende* (mende), *Nzuki* (nyuki), *Isigi* (nzige) na *Kimulimuli* (kimulimuli) miongoni mwa Wamaragoli ulihakikishwa katika usaili wa baraza la wazee. Imebainika kwamba anthroponimu hizi zimejengwa na nomino za kawaida za Kiswahili na zinahusiana kimaana.

### 4.2.15 Kikoa Maana cha Ukoo

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zilidhihirisha maana kileksika ya ukoo/unasaba katika muktadha wa jamii hii. Nomino hizi pamoja na anthroponimu za Kimaragoli ambazo zimejengwa kwazo zinaonyeshwa katika Jedwali 4.20 hapa chini:

**Jedwali 4.20: Kikoa Maana cha Ukoo**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Babu** | *Babu* |
| **Kaka** | *Kaka* |
| **Ndugu** | *Ndugu* |
| **Dada** | *Dada* |
| **Mwana** | *Kana* |
| **Mtoto** | *Toto* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Nomino 6 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zimebainishwa katika Jedwali 4.20. Maana ya nomino zinazohusika kileksika ni ukoo au unasaba. Katika nomino za kawaida zilizokusanywa kwa upekuzi na kujadiliwa kwenye vikao vya usaili wa baraza la wazee Wamaragoli, anthroponimu zilizoorodheshwa hapa zilithitishwa kutumika katika jamii hii. Heshima ni suala linalopewa kipaumbele na jamii hii. Kwa mintarafu hiyo, watu huwapa watoto majina yanayoonyesha uhusiano wa kifamilia kama njia ya kuonyesha heshima. Majina kama vile *Babu*, *Kaka*, *Ndugu*, *Dada*, *Kana* (mwana), *Toto* (mtoto) yalithibitishwa kuwa anthroponimu za Wamaragoli kwenye vikao vya usaili wa baraza kuu la wazee. Anthroponimu zinazohusika hujengwa na nomino za kawaida za Kiswahili.

### 4.2.16 Kikoa Maana cha Taaluma

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zilidhihirisha maana kileksika ya taaluma mbalimbali zinazoshughulisha watu. Nomino hizi zimeorodheshwa katika Jewali 4.21 hapa chini:

**Jedwali 4.21: Kikoa Maana cha Taaluma**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Mwalimu** | *Mwalimu* |
| **Askari** | *Asigari* |
| **Dereva** | *Mundereva* |
| **Mkulima** | *Alima/Kilimo/Mkulima* |
| **Fundi** | *Afundi/ Mfundi* |
| **Mnyapara** | *Nyabara* |
| **Karani** | *Mkarani* |
| **Meneja** | *Maneja* |
| **Msusi** | *Mususi* |
| **Mhandisi** | *Mwandisi* |
| **Mganga** | *Muganga* |
| **Saisi** | *Saisi* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.21 linabainisha nomino 12 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli ambazo maana yake kileksika ni taaluma za watu. Hizi nomino za kawaida zilizokusanywa kwa upekuzi zilithibitishwa kuhusika katika ujenzi wa anthroponimu na baraza la wazee Wamaragoli. Maana kileksika ya anthroponimu unde ilithibitishwa kuwa ni taaluma mbalimbali za watu. Anthroponimu zilizojengwa ni *Mwalimu* (mwalimu), *Asigari* (askari), *Mundereva* (dereva), *Alima/Kilimo/Mkulima* (mkulima), *Afundi/Mfundi* (fundi), *Nyabara* (mnyapara). Mkarani (*karani*), *Maneja* (meneja), *Msusi* (mususi), *Mwandisi* (mhandisi), *Muganga* (mganga) na *Saisi* (saisi). Katika uainishaji wake wa anthroponimu kwa mtazamo wa kionomastiki, Okal (2012) anabainisha makundi kama vile: anthroponimu funge, siha, kifamilia, thioforiki, lakabu, apotropiki, teknonimu, aptronimu, matronimu na patronimiki. Hata hivyo, uainishaji wake haujumuishi taaluma za watu, ingawa ulitanua mawazo yetu na kuufanya utafiti huu kutambua kikoa hiki cha taaluma.

### 4.2.17 Kikoa Maana cha Sekta ya Kilimo

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zinadhihirisha maana kileksika ya pembejeo, zana, raslimali au shughuli za sekta ya kilimo katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli. Nomino za kawaida zinazohusika zimeoorodheshwa katika Jedwali 4.22 lifuatalo:

**Jedwali 4.22: Kikoa Maana cha Sekta ya Kilimo**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Jembe** | *Rigembe/ Magembe* |
| **Mbegu** | *Embego* |
| **Shamba** | *Rishamba* |
| **Kichaka** | *Kisaka* |
| **Mavuno** | *Mavuno/ Iravuna* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Nomino 5 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zimebainishwa kwenye Jedwali 4.22. Maana ya nomino zenyewe kileksika ni pembejeo au raslimali za kilimo. Matumizi ya anthroponimu hizi kwenye jamii ya Wamaragoli yalithibitisha katika usali wa baraza kuu la wazee. Anthroponimu kama vile *Rigembe/Magembe* (jembe), *Embego* (mbegu), *Rishamba* (shamba), *Kisaka* (kichaka) na *Mavuno/ Iravuna* (mavuno) zinaakisi zana, pembejeo na raslimali za kilimo. Akijishughulisha na utoaji majina pamoja na utamaduni wa jamii ya Akan nchini Ghana, Agyekum (ameshatajwa) anayafafanua majina yanayohusiana na mazingira. Hata hivyo, vikoa maana katika majina wala dhima ya lugha ya Kiswahili katika ujenzi wa majina katika jamii ya Akan haishughulikiwi.

### 4.2.18 Kikoa Maana cha Mapambo

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zinadhihirisha maana kileksika ya mapambo katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli. Nomino za kawaida zinazohusika zinaonyeshwa katika Jedwali 4.23 hapa chini:

**Jedwali 4.23: Kikoa Maana cha Mapambo**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Pete** | *Ebede* |
| **Saa** | *Isaa* |
| **Bangili** | *Bangili* |
| **Tai** | *Itayi* |
| **Mshipi** | *Msibi* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.23 linabainisha nomino 5 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zenye maana kileksika ya mapambo. Usaili ulithibitisha uwepo wa msamiati huu unaodokeza kwamba Wamaragoli wanaukumbatia ulimbwende, hasa wa wanawake. Ilifafanuliwa kwamba dhana ya urembo hurejelewa kwa nomino, *urusimbi* kama ilivyo katika kauli, *Eng'ombe yu rusimbi* (ng'ombe mrembo). Kwa hivyo, anthroponimu *Musimbi* inarejelea mrembo. Kuimarisha urembo, jamii ya Wamaragoli ilitumia mapambo mbalimbali kama majina ya watu. Matumizi ya anthroponimu kama vile *Ebede* (pete), *Isaa* (saa), *Bangili* (bangili), *Itayi* (tai) na *Msibi* (mshipi) miongoni mwa Wamaragoli yalithibitishwa kwenye usaili wa baraza la wazee.

### 4.2.19 Kikoa Maana cha Sekta ya Uchumi

Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zinadhihirisha maana kileksika ya sekta ya uchumi katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli. Nomino zinazohusika zimeorodheshwa katika Jedwali 4.24 hapa chini:

**Jedwali 4.24: Kikoa Maana cha Sekta ya Uchumi**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu Ijengwayo |
|---|---|
| **Senti** | *Visendi/Zisendi/Esendi* |
| **Shilingi** | *Sirinji* |
| **Noti** | *Enoti/Zinoti* |
| **Madeni** | *Kadeni/Madeni* |
| **Sokoni** | *Sogoni* |
| **Benki** | *Ebenji* |
| **Elfu** | *Erefu* |
| **Sumuni** | *Simoni* |
| **Pesa** | *Mabesa/Libese/Tobesa* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.24 linabainisha nomino 9 za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli ziwasilishazo maana msingi ya sekta ya uchumi. Maana na uwepo wa anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo na nomino za kawaida za Kiswahili ulithibitishwa katika usaili wa baraza la wazee. Imebainika kwamba *Visendi/ Zisendi/ Esendi* (senti), *Sirinji* (shilingi), *Enoti/Zinoti* (noti), *Madeni/ Kadeni* (deni), *Sogoni* (sokoni), *Ebenji* (benki), *Erefu* (elfu), *Simoni* (sumuni), *Mabesa/Libesa/Tobesa* (pesa) ni anthroponimu za Kimaragoli zinazohusiana na sekta ya uchumu na kwamba zinajengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Ingawa suala la magendo na uchumi linatajwa pia na Okoth (2019) katika uanishaji wa agoti za wafungwa, halihusiani moja kwa moja na taaluma ya onomastiki. Hata hivyo, hali hii linaonyesha kwamba kikoa maana hiki kinaweza kujitokeza kotekote.

## 4.3 Mofolojia ya Uundaji wa Anthroponimu za Kimaragoli

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kuchanganua mbinu za kimofolojia za uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Uundaji wa maneno pamoja na ubunaji wa maana ni kitengo ambacho hushughulikiwa na Nadharia ya Pragamatiki Leksika (Wilson 2003). Hii husaidia katika kuzalisha data zaidi kwa nadharia hii na kufanikisha welewa wa michakato ya kiakili na hali za kimaumbile ambazo zinahusika. Kevogo (2020) anatoa baadhi ya ruwaza na mbinu za kuunda maneno katika lugha. Anataja mbinu kama vile, ukopaji, uhusishaji, uhulutishaji, uradidi, uambatishaji, na tafsiri. Utafiti huu ulikubaliana na mawazo yake kwani hadi nyakati hizi pana leksimu ambazo zinaundwa au zinapata maana mpya au zinazobadilishwa miundo kimofolojia au kifonolojia na kwa njia hiyo kupata maana mpya. Utafiti ulitumia kipengele hiki cha uundaji wa maneno kujadili mbinu za uundaji wa anthroponimu za Wamaragoli. Kwa mujibu wa Jefwa (2010) uundaji wa maneno ni uambatanishaji wa mofimu moja au zaidi kufikia kiwango cha mofimu hiyo au hizo kuleta maana kileksika katika lugha yoyote ile. Kwa mujibu wa mtaalam huyu, mbinu za kimofolojia zitumikazo katika uundaji wa maneno katika lugha za ulimwengu ni pamoja na unominishaji, ukopaji, utohozi, uhulutishaji, ukatizaji, akronimu, uambatanishaji na uambishaji n.k. Kwa mujibu wa utafiti huu mbinu zifuatazo zimeangaziwa:

### 4.3.1 Mbinu ya Ukopaji

Utafiti ulibaini kuwa zipo anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili zilizoundwa kupitia njia ya ukopaji. Ukopaji ni utaratibu wa kuchukua maneno kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa (Massamba, 2004). Ukopaji ni hali inayojumuisha uhamishaji wa kipashio fulani kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine. Kwa hivyo, kuna lugha changizi na lugha pokezi (Jefwa, 2010). Ukopaji ni uhamishaji wa leksimu

mahususi au seti ya leksimu au faridi fulani kutoka lugha moja au lahaja moja hadi nyingine. Kuna aina mbili za ukopaji: ukopaji sisisi na ukopaji tohozi. Ukopaji sisisi ni pale ambapo leksimu fulani inahamishwa kutoka katika lugha changizi hadi katika lugha lengwa bila ya kufanyiwa marekebisho yoyote. Utafiti huu ulibaini kuwa anthroponimu za Wamaragoli zilizoundwa kwa kutumia mbinu hii.

**Jedwali 4.25: Ukopaji wa Kiutohozi**

| Leksimu Asili kutoka Kiswahili | Anthroponimu Mkopo katika Kimaragoli |
|---|---|
| **Bakuli** | *Kibakuri* |
| **Lori** | *Erori* |
| **Ndoo** | *Endoho* |
| **Mwezi** | *Mweri* |
| **Njugu** | *Injugu* |
| **Chapati** | *Chabati* |
| **Mtungi** | *Mtunji* |
| **Dania** | *Idania* |
| **Pilipili** | *Birabiri* |
| **Kabeji** | *Rikabichi* |
| **Madirisha** | *Madirisa* |
| **Tiketi** | *Digidi* |
| **Bata** | *Bada* |
| **Royko** | *Eroyko* |
| **Andazi** | *Riandasi* |
| **Simiti** | *Simidi* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.29 linaonyesha anthroponimu zilizokopwa. Utafiti uligundua kuwa utohozi unapofanywa nomino za kawaida za Kiswahili huchukuwa mifumo ya kifonolojia ya Kimaragoli k.v. fonimu /t/ Kiswahili hudhihirika kama /d/ katika Kimaragoli Taz. Ba**t**a-*Ba**d**a*, Mka**t**e-*Muga**d**i*, na Simi**t**i-simi**d**i. Fonimu /j/ ya Kiswahili hudhihirika kama /ch/ katika Kimaragoli Taz. *Rikabi**ch**i*-Kabe**j**i, ***Ri**anda**s**i*-anda**z**i aidha [z] hubadilika na kuwa [s]. pia fonimu /ng/ ya Kiswahili hudhihirika kama /nj/ katika Kimaragoli Taz. *Mtu**nj**i*-mtu**ng**i. Hata hivyo, wakati wa ukopaji, anthroponimu zilizokopwa zilidhihirisha kuongezwa kiambishi maalumu kabla ya mzizi wa neno k.v ***Ki**bakuri*-bakuli, ***E**rori*-Lori, ***E**mesa*-meza, ***E**ndege*-ndege, ***I**njugu*-njugu na ***I**dania*-dania. Katika baadhi ya nomino za kawaida zilizokopwa [**z]** ilibadilika na kuwa [**r]** kwa mfano *Mwe**r**i*-mwe**z**i, [**p**] huwa [**b**] kwa mfano *Cha**b**ati*-cha**p**ati, ***B**ira**b**i**r***i **-p**ili**p**i**l**i wakati huo [l] huwa [r] taz Kibaku**r**i-baku**l**i. Baadhi ya anthroponimu zinapokopwa kutoka nomino za kawaida za Kiswahili hubadili [**sh**] Kiswahili hadi [s] kwa Kimaragoli taz. *Madirisa*-madiri**sh**a.

Hali hii ya kuongeza viambishi **ki, e** na **i** n.k na kubadili kwa fonimu wakati wa kurazinisha fonolojia ya nomino za kawaida za Kiswahili kuwa anthroponimu za Kimaragoli inashadidia zaidi mawazo ya Mwangi (2015) na Lupenga (2006) kuhusu majina yanavyo akisi sarufi ya jamii . Kwa mfano: mofu {*ku-*} ikiongezwa kwenye mzizi *-guru* panapatikana jina *Kuguru* lenye maana ya mguu, mofimu {*mu*} ikipachikwa kwenye mzizi *-tundu* jina *Mutundu*. Kinachodhihirika katika utafiti huu ni kuwa fonolojia pia huweza kubadilika neno linapokopwa. Aidha, utaratibu wa ukopaji wa nomino za kawaida za Kiswahili na kuzitumia kujenga anthroponimu za kiswahili unaonyesha uhalisia wa mawazo ya Brynon (1977) na Campbell (1998) kuwa katika mbinu ya utohozi na ukopaji, maneno huchukuliwa kutoka kwa lugha ya kigeni au lugha nyingine kisha kuandikwa kwa kuzingatia lugha inayolengwa ili yaafiki masharti ya lugha pokezi kwa mfano: bank-benki, change-chenji, atlas-atlasi nk.

Aidha, utafiti ulibaini kuwa hali hii hufanyika hivi kwa anthroponimu hizi ili kurahisisha fonolojia yake, mawazo ambayo yanasisitizwa na Brynon (ameshatajwa) na Campbell (ameshatajwa). Baadhi ya nomino za kawaida za Kiswahili zilizokopwa sisi na kuunda anthroponimu za Kimaragoli ni kama tunavyoonyeshwa katika Jedwali 4.30 lifuatalo:

**Jedwali 4.26: Ukopaji Sisisi**

| Leksimu Asilia kutoka Kiswahili | Anthroponimu Mkopo katika Kimaragoli |
|---|---|
| **Sungura** | *Sungura* |
| **Panya** | *Panya* |
| **Jogoo** | *Jogoo* |
| **Mbuni** | *Mbuni* |
| **Goregore** | *Goregore* |
| **Bundi** | *Bundi* |
| **Majani** | *Majani* |
| **Soda** | *Soda* |
| **Sahani** | *Sahani* |
| **Kijiko** | *Kijiko* |
| **Kitabu** | *Kitabu* |
| **Masomo** | *Masomo* |
| **Kitanda** | *Kitanda* |
| **Sanda** | *Sanda* |
| **Taji** | *Taji* |
| **Juba** | *Juba* |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.30 linaonyesha anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili kupitia mbinu ya ukopaji sisisi kutoka Kiswahili. Utafiti huu umebaini ukweli katika kauli iliyotolewa na Poplack (1988) kuwa nomino aghalabu ndizo hukopwa sana wakati wa ukopaji. Kupitia ukopaji basi, nomino za kawaida za Kiswahili zilikopwa

ilikujenga anthroponimu za Kimaragoli. Aidha, wakati wa ukopaji anthroponimu hizi haziongezewi viambishi vyovyote hivyo basi, zinafanyiwa ukopaji sisisi. Anthroponimu hizi ni pamoja na *Sungura*-sungura, *Panya* –panya, *Jogoo*-Jogoo, *Mbuni*-mbuni, *Goregore*-goregore, *Bundi*-bundi, *Majani*-majani, *Soda*-soda, *Sahani*- sahani, *Kijiko*-kijiko, *Kitabu*-kitabu ,Masomo-masomo, Baika -baika, Sanda-sanda, Taji -taji na *Juba*-juba. Utafiti huu unaendeleza na kukuza dhana iliyoibuliwa na Kongo (2016) kuwa majina ya kisasa ya jamii ya Ewe ni ya kikristo na aghalabu yamekopwa sisisi. Hii bi kwa sababu utafiti huu onaonyesha kuwa mbali na ukopaji kutoka kwa imani fulani anthroponimu zinaweza kujengwa na nomino za kawaida zilizokopwa sisisi.

#### 4.3.2 Mbinu ya Uhusishaji

Hapa utaratibu wa kubuni huongozwa na vigezo maalum kama vile sifa za kimaumbile, tabia au matumizi ya kitu kiashiriwa. Sifa hizi zinaangaliwa na kisha kubuni neno linalozingatia mojawapo ya sifa zinazohusika (Kiango, 2004). Anaendelea kufafanua aina mbalimbali za uhusishaji kama vile uhusishaji wa kimaumbile na kitabia.

##### 4.3.2.1 Sifa za Kimaumbile

Kiango (ameshatajwa) anafafanua kuwa sifa za kimaumbile zinahusu namna kitu kilivyoundwa au kinavyoonekana, sifa ya dhana iliyoundiwa neno inatumiwa kama msingi wa kubuni neno jipya. Kwa mfano, neno *kipanya* lilibuniwa kuashiria kifaa katika tarakilishi kinachofanana na mnyama mdogo anayeitwa panya. Nalo neno ndege (chombo cha angani) lilihusishwa na sifa za ndege ambaye ni mnyama, yaani nyuni. Uchanganuzi wetu ulidhihirisha kuwa anthroponimu za jamii ya Wamaragoli zimeundwa kupitia mbinu hii ya uhusishaji. Jedwali la 4.31 linadhihirisha anthroponimu hizo.

**Jedwali 4.27: Uhusishaji Kimaumbile**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu ya Kimaragoli | Maana Itokanayo na Uhusishaji Kimaumbile |
|---|---|---|
| **Nyanya** | *Inyanya* | Mwenye uso mweupe usio na alama yoyote |
| **Mkono** | *Rokono* | Ana mkono mdogo |
| **Magoti** | *Magoti* | Ana miguu mirefu |
| **Sahani** | *Sahani* | Ana mdomo mpana |
| **Chapati** | *Chabati* | Ana pachi pachi usoni |
| **Nyundo** | *Inyundu* | Mfupi sana |
| **Mbavu** | *Tsimbaru* | Mkondefu |
| **Mikono** | *Makono* | Ana mikono minene |
| **Mgongo** | *Amugongo* | Amepinda mgongo |
| **Bega** | *Rivega* | Ana mabega mapana |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Jedwali 4.31 linaonyesha anthroponimu zilizoundwa kupitia mbinu ya uhusishaji kimaumbile. Baraza la wazee lilidhibitisha hili wakati wa usaili kwa kusema kuwa sifa hizi huangaliwa kisha kupewa neno linalozingatia mojawapo wa sifa za kirejelewa au zilizonuiwa kuwasilishwa, mawazo ambayo yanashabihiana na mawazo ya Kiango (ameshatajwa). Utafiti huu uligundua kuwa anthroponimu zilizoundwa kupitia mbinu hii zilizingatia hasa sifa za kimaumbile zinazohusu namna mtu alivyoonekana, sifa hiyo ndiyo ilitumika kuundia anthroponimu hizo, mawazo ambayo wataalamu wa kiisimu kutoka jamii hii walikubaliana nayo.

#### 4.3.2.2 Sifa za Kitabia

Katika mbinu hii, neno hubuniwa kwa kuzingatia tabia au hulka za kitajwa. Kwa mfano, katika kubuni neno *gari moshi* sifa ya kutoa moshi mwingi ilizingatiwa nalo neno *kifauwongo*, sifa ya mnyama kujifanya amekufa na mmea kujifanya umenyauka unapoguswa ilizingatiwa. Kuna majina yaliyoundwa kutoka na sifa za kitabia katika jamii ya Wamaragoli. Mifano ya anthroponimu hizi zinadhihirika katika Jedwali la 4.32

**Jedwali 4.28: Uhusishaji Kisifa**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu za Kimaragoli | Maana Itokanayo Na Uhusishaji Kisifa |
|---|---|---|
| **Chuma** | *Kichuma* | Hasikii aghalabu hatoi machozi au kulia anapopigwa |
| **Gamu** | *Agamu* | Tabia za kukwamia |
| **Mkono** | *Rokono* | Mchoyo |
| **Bega** | *Mavega* | Anapenda kusakata mziki |
| **Chui** | *Chui* | Tabia za kugwara wenzake |
| **Simba** | *Gusimba* | Mkali kwa wengine |
| **Swara** | *Iswara* | Ana mbio |
| **Kenge** | *Ekenge* | Mjinga |
| **Pilipili** | *Birabiri* | Mkali |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**


Wataalamu wa kiisimu kutoka jamii ya Wamaragoli walidhibitisha kuwa mbinu ya uhusishaji kisifa pia ilitumika kuunda anthroponimu za Wamaragoli. Anthroponimu. Kiango (ameshatajwa) anasema kuwa mbinu hii neno hubuniwa kwa kuzingatia tabia au hulka za kitajwa. Utafiti huu basi ulidadavua kuwa athroponimu katika jedwali la 4.32 ziliundwa kutokana na sifa za kitabia miongoni mwa Wamaragoli.

### 4.3.3 Mbinu ya Uhulutishaji

Uhulutishaji pia huitwa ufupisho –mchanganyiko (Kiango, 2004). Uhulutishaji ni mojawapo ya mbinu za kuunda maneno kwa kufupisha neno au kikundi cha maneno ili kupata neno


moja jipya. Uhulutishaji ni mbinu ya kuunganisha vijisehemu vya maneno mbalimbali yaliyo katika fungu la maneno ili kuunda neno moja jipya. Mara nyingi dhana inayobebwa na nenounde huwa changamani (Kahigi, *ameshatajwa*). Vijisehemu vinavyohusika si lazima vijisimamie kama maneno kamili au mofimu kamili kama ilivyo katika mbinu ya mwambatano na unyambulishaji mtawalia. Hata hivyo, kuna uwezekano wa vipashio vinavyounganishwa kuwa mashina kamili.

Data ilidhihirisha kuwa anthroponimu za Wamaragoli zinaundwa na nomino za kawaida za Kiswahili zinaudwa kwa njia ya uhulutishaji. Utafiti huu ulibaini kuwa anthroponimu za Wamaragoli zinaundwa kupitia mbinu ya uhulutishaji mchanganyiko ambapo sehemu ya neno la kwanza ya neno la pili zinachanganywa ili kuunda neno moja. Kahigi (ameshatajwa) anasema kuwa katika uhulutishaji vijisehemu vya maneno mbalimbali yaliyo katika fungu la maneno huunganishwa ili kuunda neno moja jipya. Hali hii inadhihirika katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili ambapo fungu la maneno linahulutishwa huku vijisehemu vyake vikiunganishwa na kuunda neno. Kwa mfano:




**Kielelezo 4.2: Uundaji wa Anthroponimu *Samoja* kwa Uhulitishaji**


Wataalam wote wa kiisimu walithibitisha na kukubaliana na utafiti huu kuwa mbinu ya uhulutishaji inachangia katika uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Walieleza utafiti huu kuwa mswahili huanza kuhesabu siku yake kuanzia wakati jua linapochomoza, saa moja asubuhi. Kupitia uhulutishaji nomino inayotumiwa kurejelea wakati jua linapochomoza hufupishwa na hivyo basi kujenga anthroponimu *Samoja.* Anhroponimu za kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili zinazoundwa kwa mbinu hii ni kama ifuatavyo:




**Kielelezo 4.3: Uundaji wa Anthroponimu *Sambili* kwa Uhulitishaji**


Anthroponimu *Sambili* inaundwa kupitia mbinu ya uhulutishaji. Maneno saa mbili yanafupishwa kisha kuunganishwa pamoja. Aidha, wataalamu walishindilia kuwa kuna watu


ambao wanaweza kutumia *Sambi**li*** au *Sambi**ri***. Hii ni kwa sababu herufi {l} aghalabu hutamkwa {r}, hivi kwamba hata wakiandika *Sambili* watatamka *Sambi**ri.***





**Kielelezo 4: Uundaji wa Anthroponimu *Satatu* kwa Uhulitishaji**

Aidha, maneno saa tatu yanahulutishwa na kujenga anthroponimu *Satatu*. Kinachobanika hapa ni kuwa maneno haya yanafupishwa kisha yanaunganishwa. Hali hii inadhihirika kwa anthroponimu *Satano*, *Sasita* na *Sakomi* kama ifuatavyo:




**Kielelezo 4.5: Uundaji wa Anthroponimu *Satano, Sasita na Sakomi***

### 4.4 Mabadiliko ya Maana katika Anthroponimu za Kimaragoli

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kufafanua mabadiliko ya kisemantiki katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Sampuli za data zilizochanganuliwa katika sehemi ya 4.2 kuhusu vikoa maana ndizo zimechanganuliwa katika sehemu hii ili kuonyesha mabadiliko ya kimaana yanayotokea. Blutner (2011)

akimrejelea Wilson (2003), anafafanua masuala ya kimsingi ambayo yanashughulikiwa katika nadharia ya Pragmatiki Leksia kama; kubanika kwa maana ya neno, kupanuka kwa maana ya neno na kukisia maana ya neno. Michakato hii ya kipragmatiki leksika ulitumiwa kufafanua mabadiliko ya kimaana yanayojitokeza katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Michakato hii ya kipragmatiki leksika hutekeleza majukumu maalum kwani kila mojawapo humwezesha msikilizaji kufasiri tamko la lugha kwa njia tofauti na ule ufasiri wa kisemantiki. Mabadiliko hayo yanadhihirika kutokana na ubanaji wa kileksia, upanuzi wa kileksika na kisio la maana.

### 4.4.1 Ubanaji wa Kileksia

Utafiti ulizingatia mhimili wa nadharia ya Pragmatiki Leksika wa ubanaji wa kileksika kufafanua mabadiliko ya kisemantiki katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Kwa mujibu wa Kolaiti na Wilson (2012), ubanaji wa kileksika ni mchakato ambao unahusu matumizi ya neno au kirai katika kuonyesha dhana mahususi zaidi ambayo ina maana finyu kuliko maana iliyosimbwa kiisimu, yaani maana pana ya neno ndiyo iliyosimbwa kiisimu. Ubanaji unapofanywa, dhana ndogo hupatikana katika muktadha wa matumizi. Maana inayojitokeza huwa ni kisehemu tu cha maana pana ambayo imesimbwa. Anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili zilidhihirisha ubanaji wa kimaana. Nomino za kawaida za Kiswahili kama vile: sungura, pilipili, paka, kiatu, chuma na kikapu zinaonyesha ubanifu wa kileksia zinapotumiwa kama anthroponimu za Kimaragoli kama inavyooneshwa katika Jedwali 4.25 lifuatalo:

**Jedwali 4.29: Ubanaji wa Kileksia**

| Nomino za Kawaida (Kiswahili) | Anthroponimu ya Kimaragoli | Maana Iliyobanika katika Kimaragoli |
|---|---|---|
| **Sungura** | *Kisungura* | Mjanja |
| **Pilipili** | *Birabiri* | Mkali |
| **Paka** | *kibaga* | Safi |
| **Kiatu** | *Kirato* | Bure kabisa |
| **Chuma** | *Kichuma* | Haogopi |
| **Kikapu** | *Kikabo* | Hashibi |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Blutner (1998) anafafanua ubanaji maana kuwa ni kutumia faridi leksika kuwasilisha ufasiri uliobanwa zaidi kuliko ule uliosimbwa kisemantiki. Anusu (2015) anashadidia hoja hii anaposema kuwa maana iliyosimbwa inaweza kubanwa katika viwango tofauti kutegemea muktadha. Hivyo basi, Jedwali 4.25 linaonesha anthroponimu zinajengwa na nomino za

kawaida za Kiswahili zilizobanika kimaana kama vile *Kisungura, Birabiri, Kibaga, Sahani, Kichuma na Kikabo*. Anthroponimu hizi zinasimba fahiwa mahususi na finyu zaidi katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli. Ili kuelewa maana iliyosimbwa, sharti msikilizaji afanye ufasiri kutegemea muktadha. Hii ni kwa sababu maana ya anthroponimu hizi ni pana kwa kiwango fulani. Kwa hali hiyo, ubanaji kwa kiwango kikubwa ni mchakato ambao unaweza kusawazishwa na hutegemea muktadha (Horn & Ward, 2004).

Maana kileksia ya sungura (*kisungura)* ni mnyama mdogo mwenye miguu mifupi, masikio marefu ambayo husimama wima na mkia mfupi wenye manyoya mengi anayedaiwa kuwa mwerevu katika kuwakwepa maadui wake na aghalabu anaamika kuwa mjanja katika ngano. Maana hii ya kileksika ni pana sana, ikilinganishwa na maana finyu zaidi inayowasilishwa na anthroponimu hii katika muktadha wa jamii hii. Kwamba *Kisungura* ni tabia za kidanganyifu au kijanja. Pamoja na kuwa mnyama anayefugwa nyumbani, usaili wa baraza la wazee, ulieleza *Kisungura* kuwa mhusika katika ngano za Kimaragoli. Ni mnyama ambaye hujifanya amelala kumbe hajalala, hujifanya analia au hata amekasirika na si rahisi mtu amshike. Hivyo basi, mtu ambaye anadhihirisha tabia za kijanja hupewa anthroponimu *Kisungura* kuwasilisha ujumbe kwa jamii kuwa mtu ni mjanja au anadhihirisha tabia za kijanja. Aidha, baraza lilisisitiza kwa kusema kuwa *Kisungura charange mzingano zya Varogoori, chagadanga isimba, mwami wi zinyama* (sungura alikuwa katika hadithi za Wamaragoli kama mhusika aliyesheheni tabia za kijanja na aghalabu alimdanganya simba ambaye alikuwa mfalme wa wanyama). Ingawa maelezo ya baraza kuu la wazee Wamaragoli yanashabihiana na mawazo ya Mutunda (2017) kuwa jina la mtu ni kama stakabadhi ambapo historia, utamaduni na urithi wa jamii unaweza kusomwa, imebainika kuwa majina ya wanyama yanapotumika anthroponimu huonyesha fahiwa mahususi zaidi kuliko ile iliyosibwa katika nomino ya kawaida iliyoijenga.

Anthroponimu *Birabiri* imesimba dhana ya **ukali**. Kwa mujibu wa Blutner (1998) ubanaji ni kutumia faridi leksika kupitisha maana ambayo imebanwa zaidi kuliko ile ambayo imesimbwa kisemantiki. Kisemantiki, pilipili *(ibirabiri)* ni tunda dogo refu lililonyooka au duara lililo la kijani ambalo likiiva huwa jekundu na hutumiwa kama kiungo cha kitoweo na ganda na mbegu zake huwasha sana. Katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli, anthroponimu *Birabiri* ina maana ya **mtu mkali**. Usaili wa baraza la wazee ulibainisha kuwa sifa nyingine za mmea huu zimetengwa katika muktadha huu. Kubanika kwa maana husababisha ufinyizi wa maana ya neno (Anttila, 1972). Maana ya pilipili inabanika katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli na kupata maana ya **mtu mkali**. Imedhihirika kwamba

katika ubanaji maana msingi ya neno huchukuliwa na nyingine zikaachwa (Kolaiti & Wilson, 2012). Aidha, maana ya jumla hupotea na kurejelea zile maana zilizo bayana zaidi kuliko za zamani. Hivyo basi, katika muktadha wa jamii hii maana nyingine za nomino za kawaida za Kiswahili zinatoweka anthroponimu hii inapojengwa kwa ubanaji au ufinyizi kimaana.

Mchakato wa ubanaji umetumika kuonyesha fahiwa mahususi zaidi kuliko ile iliyosimbwa katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili; hali iliyotufaa katika ubainishaji wa maana finyu zaidi ya anthroponimu zinazohusika. Umeonyesha namna msikilizaji anavyojenga dhana mbalimbali pamoja na michakato ya kipragmatiki, hasa ile iliyofafanuliwa na Carston (2002). Aidha, anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili zilizoathiriwa na badiliko hili la ubanaji zilitumia faridi leksika katika kuwasilisha maana iliyobanwa zaidi ya ile iliyosimbwa kisemantiki; hali iliyopelekea utafiti huu kukubaliana na Blutner (1998) kwamba maana ya neno inaweza kubanwa zaidi ikilinganishwa na maana pana ya leksimu, kwani hali hii imedhihirika katika anthroponimu za Kimaragoli zilizojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili.

### 4.4.2 Upanuzi wa Kileksia

Mchakato wa pili wa kileksia katika Nadharia ya Pragmatiki ni upanuzi wa kimaana. Kwa mujibu wa Fromkin na wenzie (2011) upanuzi wa kileksika ni mchakato ambao kwao maana ya neno hutanuka. Yaani, neno linamaanisha kila kitu kilichokuwa kikimaanishwa na kuzidisha maana nyingine. Tunaweza kusema kuwa neno linalopanuka kimaana huwa limeongezewa vitajwa na kujumuisha vitajwa vingine. Kroeger (2018) anafafanua kuwa maneno yanapewa maana moja banifu au zaidi bila ya maana asilia kupotea. Ile maana asilia na maana ya pili zinatumika upande - upande bora tu kusiwepo na mikinzano (Anusu, 2015). Mchakato huu ulisaidia utafiti huu kuonyesha namna maana za anthroponimu za Wamaragoli zilivyopanuka kimaana bila ya maana yake asili kupotea.

Upanuzi wa maana hutokea pale maana ya neno hubadilika na kuwa pana kuliko ile ya asilia (Krsten, 1991). Maana ya neno hupanuka pale linapopata maana zaidi ya ile ya awali (Fromkin na wenzie, 2011). Anthroponimu za Kimaragoli zinazoundwa na nomino za kawaida za Kiswahili zimeibua maana mpya katika muktadha wa jamii hii. Upanuzi wa kileksika unajumuisha: upanuzi wa kisitiari na chuku. Kama inavyofafanuliwa katika vijisehemu vifuatayo:

#### 4.4.2.1 Upanuzi wa Kisitiari

Simiyu (2016) anaeleza upanuzi wa kisitiari kuwa ni mchakato ambao kwao maana ya neno ipo mbali na maana wazi. Yaani, maana ya neno fulani katika muktadha wa mazungumzo ni tofauti kabisa na maana ya neno hilo kiisimu. Katika upanuzi wa kisitiari, maana ya neno huwa mbali na maana halisi kwa kuhamisha maana ya neno hilo toka kwa kiashiria kimoja hadi kiashiria kingine. Hivyo basi, anthroponimu hizo zimefuata kanuni ya upanuzi wa maana kama inavyojidhihirisha katika Jedwali 4.26. Matokeo katika jedwali hili yanaonyesha namna anthroponimu za Wamaragoli zinazojegwa na nomino za kawaida za Kiswahili zinavyopanuliwa kimaana.

**Jedwali 4.30: Upanuzi wa Kisitiari**

| Nomino za Kawaida za Kiswahili | Anthroponimu za Kimaragoli | Maana Iliyopanuliwa Kisitiari katika Kimaragoli |
|---|---|---|
| **Mikono** | *Makono* | Aghalabu husabaisha mkosi |
| **Bata** | *Gubada* | Hana msimamo |
| **Kijiko** | *Kijiko* | Anayetumiwa kutekeleza maovu |
| **Sahani** | *Sahani* | Ana mdomo mpana |
| **Bakuli** | *Kibakuri* | Mlafi |
| **Birika** | *Biniga* | Mchoyo |
| **Moyo** | *Umwoyo* | Haogopi chochote |
| **Jogoo** | *Jogoo* | Anapenda wanawake wengi |
| **Nyanya** | *Inyanya* | Mweupe /mrembo |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Upanuzi wa kisitiari aghalabu hutumika kuficha ujumbe unaowasilishwa (Bloomfield, 1933). Badala ya kusema waziwazi kinachowasilishwa hapa, upanuzi wa kisitiari hutumika kuficha ujumbe unaowasilishwa usiwe wa njia ya moja kwa moja. Hali hii inajitokeza katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Kwa mfano, mkono (*mukono)* ni sehemu ya mwili wa mtu inayotumiwa kushikia vitu. Katika muktadha wa jamii hii, maana ya anthroponimu *Makono* hupanuliwa kumaanisha kisirani. Kutokana na usaili, baraza kuu la Wamaragoli lilifafanua kuwa kuna msemo maarufu katika jamii hii usemao kuwa, *tanyola makono madamanu* (usinisababishie kisirani au mkosi).

Aidha, maana ya nomino ya kawaida bata (*libada*) inapanuliwa hadi kujenga anthroponimu *Gubada*, yaani mtu ambaye hana msimamo thabiti kwa lolote, hufuata wenzake na huunga mkono chochote. Anayeitwa *Kijiko* anafanya mambo haraka haraka na aghalabu hutumiwa kutekeleza maovu. Maana iliyopanuliwa ya anthroponimu hizi inashabihiana na mawazo ya Ullamann (1970) kwamba maneno yanapewa maana moja bainifu bila ya maana yake asilia kupotea. Vilevile, anthroponimu *Sahani* inajengwa kutokana na nomino ya kawaida sahani (*isahani*), yaani kifaa cha nyumbani kilicho na umbo la mduara kilichotengenezwa kwa bati,

chuma, kauri ama plastiki ambacho hutumiwa kutilia chakula. Maana hii hupanuliwa kisitiari katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli kumaanisha mtu anayependa kula sana.

Isitoshe, anthroponimu *Bakuri (*bakuli) ambayo maana yake ya kimsingi ni aina ya chombo kama sahani chenye kina kitumikacho kupakuliwa chakula hasa kitoweo ama kunywia maji, inapanuliwa kisitiari katika muktadha wa jamii ya Wamaragoli kumaanisha mtu ambaye anapenda kula na anayehitaji kula chakula kingi ndipo ashibe kutokana na kina cha bakuli. *Birika* hupanuliwa kumaanisha mchoyo, *Moyo* haogopi, *Jogoo* anapenda wanawake wengi na aghalabu amezalisha watu kisha anthroponimu *Nyanya* hupanuliwa kumaanisha mweupe sana aghalabu kwa jinsia ya kike.

Upanuzi wa kisitiari katika anthroponimu za Kimaragoli zinazoundwa na nomino za kawaida za Kiswahili unadhihirisha usimbaji wa maana katika lugha kama alivyodhihirisha Ochichi (2013) alipogundua kuwa lugha ya Kiswahili na Ekegusi zinasimba maana katika kauli zake. Imedhihirika kwamba maana haisimbwi tu katika kauli za lugha pekee bali pia inaweza kusimbwa katika anthroponimu ambazo zimepanuliwa kimaana. Anthroponimu hizi ziliweza kuathiriwa na badiliko hili, hivi kwamba zilipanuka, yaani zinamaanisha kila kitu kilichokuwa kikimaanishwa na kuzidisha maana nyingine. Mawazo ya kijumla ya Ullamann (1970) yametanuliwa kwa kupewa msingi na mifano katika lugha mahususi. Maneno ya lugha yamepewa maana moja bainifu au zaidi bila ya maana asilia kupotea na kwamba ile maana asilia na maana ya pili zinatumika upande-upande.

#### 4.4.2.2 Chuku

Kwa mujibu wa Wilson (2003) chuku ndilo badiliko linalonekana kuhusisha kiwango kikubwa zaidi cha upanuzi wa maana. Chuku hupelekea uwepo wa utengano mkubwa kutoka kwa dhana  inayosimbwa. Badiliko hili linahusisha upigaji chuku au kutia chumvi. Usaili wa baraza la wazee Wamaragoli ulidhihirisha uwepo wa chuku katika Anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Nomino namino zinazohusika ni swara, timazi, kabati, mbavu, magoti, nyundo, kabeji, sukumawiki, ngamia na chumvi kama inavyoonekana katika Jedwali 4.27 lifuatalo:

**Jedwali 4.31: Chuku**

| Nomino za Kawaida za Kiswahili | Anthroponimu za Kimaragoli | Maana Iliyotiwa Chuku |
|---|---|---|
| **Swara** | *Iswara* | Mtu mwenye mbio za ajabu |
| **Kabati** | *Ikabati* | Mnene kupindukia |
| **Mbavu** | *Tsimbaru* | Amekondeana sana |
| **Magoti** | *Magoti* | Mrefu zaidi |
| **Nyundo** | *Inyundu* | Mtu mfupi sana |
| **Kabeji** | *Rikabichi* | Mtu mnene na mtulivu |
| **Sukuma wiki** | *Risuguma* | Mtu duni aghalabu hana thamani |
| **Ngamia** | *Ingamia* | Anayeweza kustahimili hali ngumu |
| **Chumvi** | *Ijumbi* | Mtu muhimu sana |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Uchanganuzi wa data zilizoko katika Jedwali 4.27 unadhihirisha badiliko hili la chuku katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Katika badiliko hili, maelezo ya wasailiwa yalidhihirisha upigaji chuku kwani watu wanapewa sifa zisizo za kihalisia kupitia athnroponimu wanazopewa. Kwa mfano, anthroponimu *Iswara* inapanuliwa kumaanisha mtu mwenye mbio za ajabu. Wakati mwingine mbio hizo huonekana anapozaliwa, yaani alitoka haraka, anapokuwa anafanya vitu upesi kama vile kula, kutambaa au hata kutembea.

Anthroponimu *Timazi* nayo hupewa mtu aliyenyooka kimaumbile, *Ikabati* mtu mnene kupita kiasi. *Tsimbaru* (mbavu) amekondeana kupita kiasi. Hivi kwamba amebaki tu mbavu, magoti mrefu zaidi kuliko kimo cha kawaida, *Inyundu* (nyundo) ni mfupi sana, kabeji (*Rikabichi*) mtu vivi hivi asiye na thamani, mtu duni sana. Ilhali *Ingamia* (ngamia)  mtu mvumilivu sana anayeweza kustahimili mawimbi ya aina yoyote na hali zozote, ikiwemo hali ngumu, matatizo na taabu za aina yoyote kama vile ukosefu wa maji, chakula n.k. Hatimaye, *Ijumbi* (chumvi) hurejelea mtu muhimu sana.

Kutiliwa chuku kwa anthroponimu hizi za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili kunadhihirisha badiliko la maana la upanuzi kupitia chuku. Maana ya anthroponimu hizi inakiuka uhalisia katika muktadha wa jamii hii. Hali inayotanua mawazo ya Wilson (2003) kuwa kuna utenganano mkubwa kutokana na dhana zinazosimbwa katika anthroponimu hizo na uhalisia.

### 4.4.3 Kisio la Maana

Katika nadharia ya Pragmatiki Leksika, mchakato wa kipragmatiki wa tatu ni kisio la maana. Hili ni badiliko ambalo kwalo leksimu iliyo na maana thabiti kiasi hupanuliwa ukingoni na

kujumuisha mawanda ya makundi ambayo kwa hakika yanapatikana nje ya maana yake kamili ya kiisimu. Carston (2002) anasema kuwa katika kisio la maana, ile maana ya kawaida inadondoshwa ili kuwezesha kuzalika kwa maana iliyosimbwa. Jedwali 4.28 linaonyesha anthroponimu za Kimaragoli zilizoundwa kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili zinazoathirisha badiliko la kisio la maana.

**Jedwali 4.32: Kisio la Maana**

| Nomino ya Kawaida ya Kiswahili | Anthroponimu ya Kimaragoli | Kisio la Maana katika Kimaragoli |
|---|---|---|
| **Shoka** | *Shoka* | Alisabaisha kukatika kwa uhusiano |
| **Soda** | *Esoda* | Anapenda raha |
| **Ndege** | *Endege* | Ana haiba ya juu |
| **Andazi** | *Riandasi* | Kupatikana kirahisi |

**Chanzo: Data Nyanjani, 2021**

Usaili wa baraza kuu la wazee ulithibitisha uwepo wa anthroponimu za Kimaragoli zinazoundwa na nomino za kawaida za Kiswahili zilizojengwa kwa kudondosha maana yake ya kawaida ili kuweza kuzalika kwa maana nyingine iliyosimbwa. Anthroponimu hizo ni pamoja na *Shoka* (shoka) anthroponimu inayopewa mtu aliyesababisha kukatika kwa uhusiano kati ya wazazi wake au jamii anapozaliwa. Yaani, kuzaliwa kwake kunasababisha ugomvi mkali. *Mugadi* (mkate) ni mtu anayependa kula vitu vitamu vitamu, *Soda* (soda) anapenda maisha ya raha, *Endege* (ndege) anapenda kuishi maisha ya haiba ya juu kisha *Riandasi* (andazi) anapatikana kotekote kirahisi. Katika badiliko hili maana ya anthroponimu hizi hupanuliwa na kujumuisha mawanda ya makundi ambayo yanapatikana nje ya maana yake kamili ya kiisimu. Kauli ambayo inashadidiwa na Carston (2002) kuwa maana ya kawaida inadondoshwa katika kisio la maana na kuzalika kwa maana iliyosimbwa.

### 4.5 Hitimisho

Sura hii imewasilisha data na kujadili matokeo kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Anthroponimu za Wamaragoli zimeainishwa katika vikoa maana vya wanyama, ndege, mimea, vyakula na vinywaji, vifaa vya matumizi katika jamii, taaluma ya elimu, samani, magonjwa, sehemu za mwili, jamii na utaifa, mavazi, nyakati, silaha, wadudu, ukoo, taaluma za watu, kilimo, mapambo pamoja na sekta ya uchumi. Mabadiliko ya maana yanayoathiri anthroponimu za Kimaragoli yamejadiliwa pia katika sura hii. Mabadiliko hayo ni pamoja na ubanaji wa kileksika, upanuzi wa kileksika, badiliko la kisitiari, chuku pamoja na kisio la maana. Hatimaye, mbinu za kimofolojia zitumikazo katika ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli zimefafanuliwa. Mbinu zilizoelezwa ni pamoja na ukopaji, uhusishaji, uradidi,

mwambatano, uhulutishaji, uambishaji na onomatopea. Sura inayofuata inawasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari wa tasnfu kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Hitimisho linalotokana na mijadala ya matokeo ya utafiti limewasilishwa. Hatimaye, mapendekezo ya kisera na kiutekelezi pamoja na mapendekezo ya tafiti za baadaye yanatolewa.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulihusu uchanganuzi kimofosemantiki wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza inafafanua masuala ya kimsingi yaliyoongoza uchunguzi huu. Masuala yaliyofafanuliwa ni pamoja na: usuli, suala linalochunguzwa, maswali na madhumuni ya utafiti, upeo na umuhimu wa utafiti. Sura ya kwanza pia imefafanua mihimili ya nadharia iliyoongoza utafiti.

Sura ya pili imehakiki maandishi muhimu yanayochangia urazinishaji wa pengo na haja ya kutekeleza uchunguzi huu. Mawazo ya watafiti na wataalamu mbalimbali wanaojishughulisha na mada zilizoingiliana au kuhusiana na uchanganuzi kimofosemantiki wa anthroponimu yamezingatiwa. Sura ya tatu inajadili methodolojia ya utafiti. Sura hii inafafanua muundo wa utafiti, eneo la utafiti, idadi lengwa, sampuli na usampulishaji. Pia kuna maelezo kuhusu njia za utafiti, vifaa vya utafiti na namna data ilivyochanganuliwa, uwasilishaji wa matokeo, uhalali, utegemezi na ukubalifu wa data na hatimaye namna utafiti ulivyozingatia maadili.

Matokeo ya utafiti huu yamejadiliwa katika sura ya nne. Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kinathari huku majedwali yakitumiwa kuwasilisha data za kimakundi. Data hiyo imedhihirisha vikoa maana vya wanyama, ndege, mimea, vyakula na vinywaji, vifaa vya matumizi katika jamii, taaluma ya elimu, samani, magonjwa, sehemu za mwili, jamii na utaifa, mavazi, nyakati, silaha, wadudu, ukoo, taaluma za watu, kilimo, mapambo pamoja na sekta ya uchumi katika nomino za kawaida za Kiswahili zinazotumika kujenga anthroponimu za Kimaragoli. Mabadiliko ya maana kama vile ubanaji wa kileksia, upanuzi wa kileksika, upanuzi wa kisitiari, chuku na kisio la maana katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Aidha, mbinu mbalimbali za kimofolojia za uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili zimejadiliwa. Muhtasari wa utafiti, hitimisho na mapendekezo ya tafiti za baadaye na mapendekezo ya kisera na kiutekelezi yametolewa katika sura ya tano.

### 5.3 Mahitimisho

Anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa kutokana na nomino za kawaida za Kiswahili zimechunguzwa na kuchanganuliwa kimofosemantiki. Malengo mahususi yaliyoongoza uchunguzi wenyewe yalikuwa: kuainisha nomino za kawaida za Kiswahili zijengazo anthroponimu za Kimaragoli katika vikoa maana; kuchanganua mbinu za kimofolojia za uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo kwa nomino za kawaida za Kiswahili na kufafanua mabadiliko ya kisemantiki katika anthroponimu za Kimaragoli zijengwazo kwa nomino za kawaida za Kiswahili. Kutokana na matokeo ya uchanganuzi wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili, mahitimisho ya utafiti yanawasilishwa kwa mijibu wa malengo ya utafiti katika vijisehemu vifuatavyo:

#### 5.3.1 Vikoa Maana vya Nomino za Kawaida za Kiswahili

Uchanganuzi wa anthroponimu zilizopekuliwa kutoka sajili za hospitali na kupelekwa kwa baraza kuu la Wamaragoli kwa shughuli ya usaili zilidhihirisha ukoa maana. Nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga athroponimu za Kimaragoli zilidhihirisha vikoa maana kama vile: kikoa maana cha wanyama; kikoa hiki kiligawika katika kikoa maana cha wanyama wa kufugwa nyumbani na kikoa maana cha wanyama wa mwituni kv *paka, ng'ombe, sungura, mbwa, panya, mbuzi, swara, simba, ndovu, chura, chui, guruguru, kenge, ngwena, ngamia* na *mbiti*. Kikoa maana cha ndege ambacho vilevile kiligawika katika kikoa maana cha ndege wa mwituni na ndege wa nyumbani kv *jogoo, kanga, bata, tombo, tembe, mbuni, goregore, popo, bundi, karani, magamaga, mramba, mnandi, kondekonde* na *kadogo.*

Kikoa cha mimea kilidhihirisha ukoa wa mboga na viungo na kilijumuisha: *kitunguu, kabeji, sukuma wiki, nyanya, pilipili, dania, hoho, chumvi, sukari, majani, mafuta, bizari, masala, tangawizi, dalasini, mboga* na *ndimu*. Kikoa cha vyakula na vinywaji kilidhihirika kupitia nomino za kawaida kama vile: *mkate, soda, njugu, andazi, chapati, sima, chai, supu na nyama*. miti na kikoa maana cha magugu. Vilevile, kuna kikoa cha vifaa vya matumizi katika jamii ambacho kilidhihirisha vifaa vya usafiri, vifaa vya matumizi jikoni na vifaa vya ujenzi kv *ndege, baiskeli, gari, meli, trekta, lori, sahani, kijiko, kikombe, birika, kikapu, ndoo, mtungi, bakuli, kibuyu, mafiga, uma, kinu, jiko, debe, tarimbo, msumeno, chuma, msumari, mbao, gamu, panga, simiti, tupa, rangi, brashi, kokoto, mpini, nyundo, randa, ngazi,cherehani, chapi, mchanga, kamba, mabati na waya*.

Aidha, kikoa cha taaluma ya elimu kilijumuisha nomino kv: *fomu, kitambaa, ubao, kalamu, penseli, kitabu, masomo, baraza, hisabati, sayansi, kengele na namba*. Kikoa cha samani

kilikuwa nomino kv *kitanda, meza, kabati, mlango, dirisha, kibago* na *bakora*. Kikoa cha magonjwa kilijumuisha nomino kv *malaria, kisonono, homa, mdondo, kifafa, anemia, kiungulia, nimonia, chunusi na kaswende*. Kikoa cha viungo vya mwili kilijumuisha *mikono, mabega, mgongo, mbavu, magoti,* na *meno.* Kikoa cha utaifa/mataifa kilisheheni nomino kv *mganda, mhindi, mwitaliano, mswahili, mtaita, mwingereza, mjerumani na mzungu*. Kikoa cha mavazi kilikuwa na nomino kv *kanzu, baika, kiatu, shati, kofia, kikoi, sanda, leso, juba, kilemba, kitenge, suti, koti na suruali*. Pia, kuna kikoa cha majira/nyakati kv *saa moja, saa mbili, saa tatu, saa nne, saa tano, saa sita, saa saba, saa nane, saa tisa, saa kumi, mwezi, mwaka* na *asubuhi*. Kikoa cha silaha kilijumuisha nomino kv *bunduki, ngao, bomu, risasi, uta, kifaru* na *sumu*. Kikoa cha wadudu kilikuwa na nomino kama *kiroboto, nsi, mende, nyuki, nzige* na *kimulimuli.* Kikoa cha majina ya ukoo/unasaba kilijumuisha nomino kv *babu, kaka, ndugu, dada, mwana* au *mtoto*. Kikoa cha taaluma za watu kilijumuisha nomino kv *askari, dereva, mkulima, fundi, mnyapara, karani, meneja, msusi, mhandisi, mganga, saisi, mwashi na mwalimu*.

Kikoa cha sekta ya kilimo kilijumuisha *jembe, mbegu, shamba, kichaka* na *mavuno.* Kikoa cha mapambo kilikuwa na nomino kama vile pete, saa, bangili, tai, taji na mshipi. Kisha kikoa cha sekta ya uchumi kikawa na nomino kama senti, shilingi, noti, madeni, soko, benki, elfu na sumuni. Hivyo basi, kutokana na uchanganuzi wa data hiyo, ni bayana kuwa nomino za kawaida za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli zilidhihirisha uhusiano wa ukoa maana.

### 5.3.2 Mbinu za Kimofolojia za Uundaji wa Anthroponimu za Kimaragoli

Uchanganuzi wa data ulidhihirisha kuwa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili zimeundwa kupitia mbinu za kimofolojia za uundaji wa maneno. Mbinu za kimofolojia zilizobainika kuwa zilitumika kujenga anthroponimu za Kimaragoli kutoka nomino za kawaida za Kiswahili zilikuwa: ukopaji/utohozi, uhusihaji na uhulutishaji. Mbinu za kimofolojia zilizotumika sana kwa mujibu wa data iliyochanganuliwa za uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli kutokana na nomino za kawaidaza za Kiswahili ilikuwa ukopaji/utohozi na uhusishaji.

### 5.3.3 Mabadiliko ya Maana katika Anthroponimu za Kimaragoli

Uchanganuzi wa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili ulidhihirisha kuwa zilikumbwa na mabadiliko ya maana. Mabadiliko yaliyobainika kutokea katika anthroponimu zilizochanganuliwa ni pamoja na ubanaji wa kileksia. Katika

badiliko hili anthroponimu zilitumiwa katika muktadha wa jamii hii kuonesha fahiwa mahususi zaidi kuliko ile iliyosimbwa katika anthroponimu hizo. Uchanganuzi wa data ulidhihirisha kuwa anthroponimu za Wamaragoli ziliathirika na badiliko hili ambalo lilisababisha kutokea maana finyu zaidi ya ile ya kileksia katika anthroponimu hizo. Vilevile, anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili ziliathirika na badiliko la upanuzi wa kileksia. Katika badiliko hili maana ya anthroponimu hizi ilipanuka. Yaani, anthroponimu hizo zilimaanisha kitu kile zilizokuwa zikimaanisha na kuzidisha maana nyingine. Katika badiliko hili basi, anthroponimu zilipewa maana bainifu zaidi katika muktadha wa jamii hii huku ikisalia na maana yake asilia. Aidha, anthroponimu ziliathirika na badiliko la kisitiari ambalo liligawika katika badiliko la chuku na badiliko la kisio la maana. Katika badiliko la chuku anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za kiswahili zilionekana kutiwa chumvi ilhali katika badiliko la kisio la maana, uchanganuzi ulibainisha zimepanuliwa ukingoni na kujumuisha maana kutoka mawanda ya makundi ambayo yanapatikana nje yake. Hivyo basi, ni wazi kuwa anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili zimeathirika na michakato mbalimbali ya mabadiliko ya maana ya kiisimu.

### 5.4 Mapendekezo

Tasnifu hii haiwezi kushikilia kuwa imekamilisha utafiti wote unaohusiana na nomino za Kiswahili na anthroponimu za Kimaragoli. Tafiti nyingine zaidi kuhusu nomino za Kiswahili na anthroponimu zinaweza kufanywa. Hivyo basi, sehemu hii inatoa mapendekezo kulingana na madhumuni ya utafiti huu kwa kuzingatia vipengele viwili. Kipengele cha kwanza, kulingana na mapendekezo ya utafiti wa baadaye na cha pili mapendekezo ya kisera na kiutekelezaji.

#### 5.4.1 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye

Utafiti huu kwa ajili ya kuendeleza utafiti katika lugha ya Kiswahili, isimu ya lugha na tafiti katika lugha za kiafrika unapendekeza tafiti za baadaye zinazohusiana na mada hii:

i) Utafiti huu umeshughulikia nomino za kawaida pekee za Kiswahili zinazojenga anthroponimu za Kimaragoli. Utafiti zaidi ufanywe kuhusu uanishaji wa aina nyingine za nomino katika vikoa maana zinazotumiwa kujenga anthroponimu kv nomino za vitenzi jina, jamii, makundi, dhahania, mwambatano, wingi n.k. Pia, utafiti ufanywe kuhusu mchango wa aina nyingine za maneno katika ujenzi wa anthroponimu za Kimaragoli kama kv vitenzi, viunganishi, vielezi, vihisishi, viunganishi nk.

Aidha, utafiti unaohusu vikoa maana ufanywe katika matawi mengine ya onomasiki kama vile kwenye tawi la toponomastiki ukihusisha lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulihusu anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Vilevile, utafiti zaidi unahitajika ufanywe pasipo kujikita kwenye nomino za kawaida za Kiswahili pekee, hii ni kwa sababu Kimaragoli kinaweza kuwa na anthroponimu kutoka lugha nyingine kv Kiingereza, Kiarabu, Kijerumani, au hata lugha nyingine za kibantu.

ii) Utafiti huu ulijikita katika mofolojia ya uundaji wa anthroponimu zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Hili ni mojawapo ya matawi ya taaluma ya mofolojia, basi utafiti unapendekeza utafiti zaidi ufanywe utakaohusisha kwa kina zaidi mofolojia ya minyambuliko ya anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili. Kupitia utafiti huu, imebainika kwamba ukopaji ni mojawapo wa mbinu za uundaji wa anthroponimu za Kimaragoli. Ukopaji hutokea mara nyingi panapotokea mtagusano kati ya watu wa makabila tofauti. Ni kweli kuwa wamaragoli wametangamana na waswahili na maneno ya Kiswahili (nomino za kawaida) zikakopwa ili kujenga anthroponimu za Kimaragoli. Je, Waswahili nao wamekopa na kutohoa neno au maneno yoyote kutoka Kimaragoli? Utafiti ufanywe ili kubaini hali hii katika Kiswahili. Kwani utafiti huo utawanufaisha wanaisimu na wataalamu wa Kiswahili katika kujumuisha lugha zilizochangia katika uundaji wa leksimu za Kiswahili.

iii) Utafiti linganishi unaohusu mabadiliko ya maana katika anthroponimu ufanywe huku ukilinganisha mabadiliko ya maana katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili na za jamii nyingine. Aidha, utafiti huu ulishughulikia mabadiliko ya maana katika anthroponimu za Kimaragoli zinazojengwa na nomino za kawaida za Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia ya Pragmatiki Leksia. Kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu mabadiliko ya maana katika anthroponimu kwa kuzingatia nadharia nyinginezo ili kuzalisha maarifa zaidi ya kiisimu. Vilevile, utafiti ufanywe ili kuweka wazi vyanzo vya mabadiliko ya maana katika anthroponimu. Aidha, utafiti huu ulishughulikia mabadiliko ya maana katika kiwango cha leksia; vipashio vinginevyo vyenye maana kama vile virai, vishazi na sentensi havikushughulikiwa.

### 5.4.2 Mapendekezo ya Kisera na Kiutekelezi

Utafiti huu unapendekeza kwamba:

i) Vitabu anuwai viandikwe vya onomastiki kwa kutumia lugha ya Kimaragoli vikiwemo, vya paidinimu, ili kuimarisha marejeleo katika taaluma hii.

ii) Utafiti unapendekeza kwamba pawepo na vipindi maalumu vya isimu kwenye redio za kitaifa na za jamii vinavyofunza Kimaragoli ili kuimarisha umilisi na utendaji miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kimaragoli.

iii) Utafiti unapendekeza wazee wajitahidi kuweka mikakati ya kufunza watoto na vijana Kimaragoli wanapokuwa kwa vile baraza la wazee lilionyesha wasiwasi kuhusu vijana kutojua kuzungumza Kimaragoli.

iv) Utafiti unapendekeza vitabu vingine vya kiisimu na fasihi ya Kimaragoli kuandikwa ili kuendeleza uhifadhi wa lugha hii ikiwemo uundaji wa kamusi mbalimbali.

## MAREJELEO


Agyekum, K. (2006). The Sociolinguistic of Akan Personal Names. *Nordic Journal of African Studies, 15(2),* 206-235.

Aitchson, J., (2001). *Language change: Progress or decay? Toleo la 3*. New York: Cambridge University Press.

Alima, M. (2018). *Descriptive analysis of Oromo personal names and naming practices in Eastern Wollega zone of Oromia Regional State*. Addis Ababa: Addis Ababa University.

Anindo, C. (2016). *A Morphosemanti Study of Toponyms: Lulogoli Place Names.* Tasnifu ya uzamili haijachapishwa. Nairobi: University of Nairobi.

Anusu, A. (2015). *Usawazishaji Leksimu katika Kiswahili: Utafiti wa Vihiga*. Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Babbie, E. (2014). *The Basics of Social Research.* New York: Wadsworth, Cengage Learning.

Batoma, A. (2009). Onomastics and Indirect communication among the Kabre of Northern Togo. *Nordic Journal of African Studies, 18(3),* 215-234.

Baxter, P. na Jack, S. (2008). Qualitative case study methods: Study design and implementation for novice researchers. The Qualitative Report, 13(4), 544-599. http://www.nova.edu/sss/QR/QR13-14//baxter.pdf

Best, J.W. na Khan, J.V. (2010). *Research in Education.* New Jersey, USA.

Bible Society of Kenya. (1992). *Bibilia Habari njema.* Nairobi: Bible Society of Kenya.

Blunter, R, (2011). *Some Perspective on Lexical Pragmatics,* Pragmatic Reader: London Routledge.

Brikci, N. na Green, J. (2007). *A Guide to using qualitative research Methodology*.

Bwonya, U.J. (1998). *The Gender Dimension of Songs in Maragoli Marriage ceremonies*. Tasnifu ya uzamili haijachapishwa. Nairobi: University of Nairobi.

Campbell, L. (2004). *Historical Linguistics: An Introduction*, Edinburg: University press

Carston, R. (2002). *Thoughts and Utterances*: The Pragmatics of Explicit commununication. Oxford: Blackwell Publishing.

Chauke. M. T (2015). *Personal Names and Naming Practices among the Vatsonga*, The Anthropologist, 19:303-312, DIO:10.1080/09720073.2015.11891664

Creswell, J.W. (2005). *Research Design*. Thousand Oaks. C.A: Sage

Creswell, J.W., & Clark, V.L.P. (2004). Principles of Qualitative research: Designing a qualitative study. http: www.andrews.edu/leaderpart/roundTable/2004/worshops/2b/AU-Qual-071504-jwc-vpc.pdf

Cruse, D.A. (2000). *Meaning and Language*. An introduction to semantics and Pragmatics. New York: Oxford University Press.

Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Crystal, D. (2003). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. New York, Cambridge University Press. 2nd Edition.

Essien, O. (2000). *What's in a name? A linguistic and cultural explication of Ibibio Personal names.* In Ekkhard &O. Gensler (Eds), Proceedings of 2nd World Congress on African linguistics. (pp.103-130) Koln: Rudiger Koppe.

Flick, U. (2010). Introduction to Qualitative Research. London, UK: Sage Publications

Fromkin, V.&Rodman, R. (1993). *An introduction to Language*. 5th Ed. New York: Harcaourt Brace College Publisher.Fromkin, V., Rodman, R. na Hyams, N. (2011). *An Introduction to Language Toleo la 9*. Boston: Wadsworth.

Gerba, T.G. (2014). Morphosemantic analysis of Oromo Personal names. *International Journal of Innovation Research and Development* 3,252-259.

Guthrie, M. (1948). *The classification of the Bantu languages*. London: Oxford university press for the international African Institute.

Habwe, J, & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publisher,

Horns, L&Ward.G.(2004). *The Handbook of Pragmatics*, Oxford: Blackwell. http://www.nova.edu/sss/QR/QR13-4/baxter.pdf

Katamba, F. (1993). *Morphology*. New York: Palgrave.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B., &Msinjila, Y.P. (2009). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili* (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo. Chuo kikuu cha Dar es Salaam. TUKI

King'ei, K. & na Kisovi, C.N.M. (2005). *Msingi wa Fasihi simulizi*. Nairobi:, KLB.

Kipp, D. (2009). *Indigenous Language Revitalisation Encouragement, Guidance & Lessons Learned*. Arizona: North Arizona University.

Kombo, D.K.&Tromp, D.L.A. (2009). *Proposal and Thesis Writing*. An Introduction. Nairobi: Paulines Publication Africa.

Kongo, E.A. (2016). Language Learning: *A Mophosemantic Analysis of contemporary Ewe personal names*. International Journal of Humanities and social sciences (9)610-619

Kongo, E.A. (2016). Language Learning: *A Mophosemantic Analysis of contemporary Ewe personal names*. International Journal of Humanities and social sciences (9)610-619

Kothari, C.R. (2008), *Research Methodogy*: Methods and Techniques. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Kroeger, P.R. (2018). *Analyzing meaning: An introduction to semantics and pragmatics*. Berlin: Language Science Press.

Latsoela, P.M. (2015). A Seamantic Analysis of Sesotho place Names. Evidence from Bus stops Names. *International journal of English Language and Translation Studies.*

Levishon, S.C. (1983). *Pragmatics.* Cambridge: Cambridge University Press

Lune, H. et al. (2010). *Perspective in Social Research Methods and Analysis*. Thousand Oaks: SAGE Publication inc.

Lupenga, M. (2006). *Naming and Linguistic Africanisms in African American Culture.*Colombus: Ohio State Univeristy.

Lwangale, D.W. (2016). *A Geneological Linguistic Implication of the Abaluhya Naming System.* International Journal of Sociol Sciences &Humanities Research.vol.2(7)77-92

Lyons, J. (1981). *Language and Linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Malande, J.O.M. (2011). What's in a name? An analysis of the semantics of Lulogooli Personal Nouns. *International Journal of Humanities and Social science 1(20)*, pp211-218.

Maxwell, J.A. (2008). *Designing a qualitative Study*. www.corwin.com/upm-data/23772.ch7.pdf accesed 23/3/2020

Mbwanga, K. (2010). *New words and meaning on facebook*: A Lexical Pragmatic analysis, Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mdee, J.S., Ngogu.K., Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn.

Mensah, E. (2017). *The communicative significance of Ngemba Personal Names*, African identities.DIO:10.80/14725843.2017.1319753.

Milroy, L. (1987). *Observing and Analysing natural languages*. New York. Backwell Publishers.inc

Mohochi, S.E. (2005). *Mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili na athari zake katika matokeo ya mtihani wa Kiswahili wa kidato cha nne katika mikoa ya Pwani na Nyanza , Kenya*. Tasnifu ya uzamifu, haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Msanjila, Y. P na wenzake (2010). *Isimujamii*: Sekondari na vyuo. TUKI. Dar es Salaam

Mugenda, A.G. (2008). *Social Science Research: Theory & Principle*. Nairobi: Applied Research & Training Services

Musere, J. (2000). *Traditional African names*. http://www.amazon.com//Accessed on 04/09/2019.

Mutunda, S. (2017). Luvale personal Names and Naming Practices: *A Socio-Cultural Analysis. International Journal of Education, Culture and Society.Vol,1No3,2016pp75-81*

Mwangi, P.K. (2015). *What's in a name? An exposition of Gikuyu Grammar through personal names.* International Journal of Humanities and Social Sciences,5(9)1

Obeng, S.G. (1999). In future if I buy a dog, I'll call it Okyeman-is-ungrateful: Indirect response to potentially difficult Communicative Situations: *The case of Akan Dog names*. International Journal of the Sociology of Language, 140, 83-104

Obuchi, S.M., & Mukwana, A. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*. Nairobi: A~Flame Publishers.

Odawo, A.M. (2015). *Uhamishaji maana katika sajili ya mchezo wa kandanda.* Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa : Kenyatta University.

Odesanya, A., Sunday, O. & Akinjogbin, K. (2017). *Names as message vectors in communication*: oduological analysis of traditional Yoruba Personal Names from Ifa. Journal of the Linguistic Association of Nigeria, 20(1)248-259.

Odoyo, B.O. (2006). *Uchanganuzi wa kileksika wa hiponimia katika Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu Cha Moi.

Oduyoye, M. (1982). *Yoruba names: Their structure and Meaning*. London: Karnak House.

Ogunwale, J.A. (2012). Reflection of discourse assignment in the configuration of Yoruba Personal Names. *Mediterranean Journal of Social Sciences, 3(13),* 174-187.

Ohly, R. (1977). Patterns of New coined Abstract Terms (nominal forms) in modern Swahili. *Kiswahili, 47(1),*

Okal, B.O. (2012). Nafasi ya Tafsiri katika taaluma ya Onomastiki: Uhakiki wa mbinu zake katika Tafsiri ya Toponomastiki. *Kiswahili, 75 (1)*, 27-42.

Okyere-Marjie, S. (2015). A Linguistic Survey of types of names among the Babukusu of Kenya. *Global Journal of Human-Social Science,15(1)*, 35-42.

Onwuegbuzie, A.J. & Leech, N.L. (2007). Sampling Design in Qualitative Research: Making the sampling process more public. *The Qualitative Report, 12(2),* 238-258. http:www.nova.edu/sss/QR/QR12-2/onwuegbuziel.pdf

Oso, W.Y., & Onen, D. (2006). *A General guide to writing research proposals and reports*. A handbook for beginning researchers (2nd Ed.). Kampala: Makerere University.

Patton, M. (2002). *Qualitative Evaluation and Research Methods* (pp169-186) Beverly Hills, CA: Sage Publications.

Powell, E.T., & Renner, M. (2003). *Analyzing Qualitative Data*. http://learningstere.uwex.edu/.../g3658-12... Accesed 12/1/2020

Rachel, P. (2001). *Haida Culture in Custody*. Washington: University of Washington.

Richards, J., Platt, J. & Weiber, H. (1985). *Longman Dictionary of Language and Teaching*. Applied Linguistics. Edinburg Gate: Pearson Education.

Riemer, N. (2010). *Introducing Semantics*. New York. Cambridge University Press

Ritchel, J.& Lewis, J. (2003) *Qualitative Research Practice*: A Guide for Social Sciences Students and Researchers. Sage Publications: London.

Rubanza, I. (2000). *The linguistic creativity of Haya Personal Names*.

Sapir, E. (1949). Language: *An Introduction to the study of Speech*. London, Hart-Devis

Shillington, K. (1995). *History of Africa*. London and Basingstone. Macmillan Education Shukla, S. &Linton, J.C (2006). *Language Change, Introduction to Language and Linguistics*. New York: Cambridge University Press.

Shitemi, N.L. (2011). *Kubidhaisha na kuwezesha lugha kama sarafu ya kiuchumi na kijamii: kielelezo cha taaluma za Kiswahili na tafsri*. Moi university press.

Simiyu, C. (2016). *The Portayal of men and women in selected Bukusu Circumcision Songs: A Lexical Pragmatic Approach*. Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Sitati, V.W. (2007). *Comprehensive Name Dictionary*. Nairobi: Sas Enterprise.

Thiong'o, N. (1986). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. London: *J. Currey*.

Trochim, B. (1999). *Bil Trochim's Center for Social Research Methods*.http: www.trochim.human.cornell.edu/.20/12/2019.

Ullman, S. (1970). *Semantics: An Introduction to the Science of meaning*. Oxford: Basil

Wijaya, D. T &Yenitererzi, R. (2011). *Understanding Semantics change of words over centuries* United Kingdom: Glasgow.

Wilson, D. (2003). Relevance and Lexical Pragmatics. *In Italian Journal of linguistics*: Italy.

Wilson, D. (2012). Corpus Analysis and Lexical Pragmatics: An Overview. *http.www.phon.ucl.ac.uk? home/derived 01/3/2020.*

Wilson, D.& Cartson, R. (2007). *A Unitary Approach to Lexical Pragmatics*: Relevance, Inference and ad hoc Concepts.

www.fieldreseach.msf.org/msf/bitstream/10144/8423/1/Qualitative%20Methodology.pdf.

Yarlesis, C.et al (2009). *Morphology & Syntax Summary*.www.slideshare-net/morphostudent/copia-de-morhology-and-syntax-summary-unitedstar accesed 3/2/2020

## VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO 1: FOMU YA IDHINI YA MTAFITIWA

**CHUO KIKUU CHA MASENO**
**SHULE YA SANAA NA SAYANSI JAMII**
**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**
**SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

***Lazima mtafiti asome au asomewe kwa sauti maelezo katika fomu hii ya idhini kabla ya kushirikishwa katika utafiti***

Mnaalikwa kushiriki katika utafiti unaotekelezwa na mwanafunzi wa uzamili kutoka Chuo kikuu cha Maseno. Jina langu ni **MORRIS ODARI SALANO** nambari ya usajili **MA/FA/00037/2017.** Kushiriki katika utafiti ni hiari yako. Tafadhali chukua muda wako kusoma na kuelewa ujumbe uliomo katika fomu hii. Iwapo utasomewa basi, **sisitiza** usomewe kwa makini na uwe huru kuuliza ufafanuzi wowote.

### LENGO LA UTAFITI

Tunakuomba ushiriki katika utafiti huu kwa kutupa data ya ukweli itakayotumika kuchanganua mfumo wa upeanaji majina wa jamii ya Wamaragoli na ujumbe unaojitokeza katika majina hayo.

### UTARATIBU

Mtaulizwa maswali machache yanayohusu majina ya jamii ya Wamaragoli. Kwa idhini yenu mnaweza kurekodiwa wakati wa kujibu au mnaweza kukataa iwapo hampendi kurekodiwa. Sababu ya kutumia simu kurekodi ni kuwa wakati wa kujibu maswali mtafiti anaweza kukosa kunakili hoja muhimu, kwa kurekodi basi baadaye anaweza kuipata na ikamfaa kuandika ripoti yake. Iwapo mtakubali kurekodiwa, rekodi ya sauti zenu itahifadhiwa vyema na haitachezwa popote ila tu kwa shughuli ya utafiti huu.

### HATARI ZINAZOWEZA KUIBUKA AU IWAPO HUTAJIHISI HURU

Hautalipishwa chochote ili kushiriki katika utafiti huu. Pia, hutanufaika moja kwa moja na utafiti wenyewe kwa sasa baadaye utafiti utanufaisha jamii ya Wamaragoli kwa ujumla kwani, utasaidia kufidia pengo la utafiti la majina ambapo ripoti ya utafiti itaandikwa na kuwasilishwa kwa chuo kikuu cha Maseno na itarejelewa na watafiti wa baadaye pia tutachapisha kitabu ambacho kitapasha maarifa ya majina kwa wasomaji na kuhifadhi utamaduni wenyewe kwa vizazi vijavyo.

**MALIPO**

Hutapokea malipo yoyote baada ya kushirikishwa katika utafiti huu.

**USIRI**

Nakuhakikishia kuwa ujumbe wowote utakaonipa wakati wa utafiti huu utasalia kuwa wa siri na **HAKUNA** mtu yeyote atakayejuwa wala kupokezwa kwa vyovyote vile kwa mujibu wa sheria za utafiti. Hata ukitaka tulibane jina lako wakati wa kuwasilisha matokeo tutafanya hivyo kwa kukupa jina la msimbo ambalo halitakutambulisha moja kwa moja. Hakuna mtu yeyote atakayepokezwa hata sehemu ya ujumbe utakaotupa ikiwemo rekodi tutakazo zinasa kwa simu. Kila kitu utakachotueleza kitatumika tu kwa ajili ya utafiti pekee.

**KUSHIRIKI AU KUJIONDOA**

Ni haki yako kufanya uamuzi kushirikishwa katika utafiti huu hadi mwisho au kujiondoa katikati. Una uhuru wa kushiriki au kukataa kushiriki vilevile. Si hatia kukataa kushiriki, iwapo utakubali kushiriki unaweza kujiondoa wakati wowote na hutachukuliwa hatua yoyote. Una uhuru pia wa kukataa kujibu baadhi ya maswali na kujibu mengine na hutalazimishwa kujibu yale ambayo hujui au hutaki kujibu.

**HAKI ZAKO KAMA MTAFITIWA**

Wewe kama mtafitiwa una haki zako za kimsingi. Kwa vyovyote vile hazifai kukiukwa wakati unaposhirikishwa katika utafiti huu. Ni haki yako kukubali kushiriki au kukataa kushiriki bila kushurutishwa au kulazimishwa. Ni haki yako kujiondoa wakati wowote katika utafiti huu na hutachukuliwa hatua yoyote. Ni haki yako pia kuuliza mtu yeyote asiyehusika na utafiti huu moja kwa moja haki zako za kushiriki, athari za kushiriki na iwapo una uhuru wa kuwasiliana na chuo kikuu cha maseno iwapo utahisi haki zako zimekiukwa.

**UTAMBULISHO WA MTAFITI**

Kama una maswali yoyote kuhusu utafiti huu, maoni, malalamishi kuhusu mtafiti, kuonewa, kudhulumiwa au kulazimishwa, jihisi huru tafadhali kuwasiliana na chuo kikuu cha Maseno kupitia kwa wasimamizi wa utafiti huu:

**Prof. Indede Florence**
**Mkuu wa Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika**
**S.L.P. PRIVATE BAG,**
**MASENO.**

**0722452087**

**Au**

**Dkt. Okal Benard**
**Mhadhiri Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika,**
**S.L.P. PRIVATE BAG,**
**MASENO.**
**0720856280**

**HATI YA KUKUBALI KUSHIRIKI**

Kutia sahihi fomu hii ina maana kuwa umechukua muda wako ukasoma kwa makini fomu hii au umesomewa kwa utaratibu unaostahili ukaelewa na kwa hivyo kwa hiari yako unakubali kushirikishwa katika utafiti wenyewe kama mtafitiwa kutoa ujumbe wa ukweli kama mtafitiwa. Utapokezwa nakala ya fomu hii baada ya kutia sahihi yako.

Ninakubali bila kulazimishwa kushirikishwa katika utafiti kama mtafitiwa.

**KIAMBATISHO 2: ORODHAHAKIKI**

**CHUO KIKUU CHA MASENO**

**SHULE YA SANAA NA SAYANSI JAMII**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**Jina la Hospitali: …………………………………. Tarehe……………………….**

| Maktaba | Hospitali | Baraza Kuu la Wazee Wamaragoli |
|---|---|---|
| Senti | Visendi/Zisendi | ✓ |
| Pete | Ebede | ✓ |
| Jembe | Rigembe/Magembe | ✓ |
| Askari | Asigari | ✓ |
| Kiroboto | Keromboto | ✓ |
| Kitunguu | Kitunguru | ✓ |
| Majani | Majani | ✓ |
| Njugu | Injugu | ✓ |
| Ndege | Endege | ✓ |
| Simiti | Simidi | ✓ |
| Waya | Ruwaya | ✓ |
| Ndoo | Endoho | ✓ |
| Debe | Madebe | ✓ |
| Randa | Iranda | ✓ |
| Kitabu | Kitabu | ✓ |
| Masomo | Amasomo/Masomo | ✓ |
| Ngazi | Ingasi | ✓ |
| Mikono | Rokono/Makono/Akekono | ✓ |
| Moyo | Umwoyo | ✓ |
| Bakora | Ibagora | ✓ |
| Kisonono | Kisununu/ Sununu | ✓ |
| Homa | Zihoma | ✓ |
| Kitenge | Ketenga | ✓ |
| Bunduki | Bunduji | ✓ |

## KIAMBATISHO 3: MWONGOZO WA USAILI WA BARAZA LA WAZEE

**CHUO KIKUU CHA MASENO**
**SHULE YA SANAA NA SAYANSI JAMII**
**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**
**SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**UTANGUZI**

Jina langu ni MORRIS ODARI SALANO. Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika Kiswahili wa Chuo kikuu cha Maseno. Ninafanya utafiti wa kiisimu wenye mada **Uchanganuzi wa kimofosemantiki wa Anthroponimu za Wamaragoli.**

**A. LENGO**

Ninaomba niwaulize maswali yanayohusiana na majina ya Wamaragoli haswa maana yake ili niandike ripoti itakayonisaidia kukamilisha kazi yangu na kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili.

**B. UMUHIMU WA UTAFITI**

Maana ya majina mtakayonipa mbali na kunisaidia kuandika ripoti itakayowasilishwa kwa Chuo kikuu cha Maseno, itachangia kudumisha lugha hii na kuelimisha vizazi vijavyo kususu majina.

**C. MUDA**

Shukran kwa kufika kwenu. Naomba *Niwasaili kwa muda mchache na tutakuwa na mapumziko mafupi katikati. Tafadhali jihisi huru kuchangia. Mchango wenu ni wa maana sana katika utafiti huu. Nina simu, kifaa ambacho nitakitumia kurekodi majadiliano yetu. Je kuna yeyote ambaye anashida na kurekodiwa?*

1. Kundi hili linaitwaje?
2. Muundo wa kundi hili huwa vipi?
3. Jamii ya Wamaragoli
   - ✓ Wamaragoli ni kina nani?
   - ✓ Historia yao
   - ✓ Lugha yao
   - ✓ Namna wanavyojikimu kimaisha
4. Utamaduni wa Wamaragoli
   - ✓ Wamaragoli wanazingatia tamaduni zipi?
   - ✓ Nielezeni zaidi kuhusu huo utamaduni wa kuwapa watoto majina katika hii jamii.

- ✓ Vigezo vipi vinavyozingatiwa wakati wa upeanaji majina katika jamii ya Wamaragoli?

5. Majina kutoka sajili za hospitalini
   - ✓ Hili ni jina la Wamaragoli?
   - ✓ Hili jina lina maana gani katika jamii ya Wamaragoli?
   - ✓ Je, lina maana nyingine yeyote?

S**hukran sana kwa kushiriki Mungu awabariki**

**KIAMBATISHO 4: KIBALI CHA SGS**

**MASENO UNIVERSITY**

**SCHOOL OF GRADUATE STUDIES**

***Office of the Dean***

**Our Ref:** MA/FA/00037/2017

Private Bag, MASENO, KENYA
Tel:(057)351 22/351008/351011
FAX: 254-057-351153/351221
Email: sgs@maseno.ac.ke

Date: 13th November, 2020

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

**RE: PROPOSAL APPROVAL FOR SALANO MORRIS ODARI — MA/FA/00037/2017**

The above named is registered in the Master of Arts in Kiswahili in the School of Arts and Social Sciences, Maseno University. This is to confirm that his research proposal titled "A Mophosemantic Analysis of Maragoli Anthroponyms." has been approved for conduct of research subject to obtaining all other permissions/clearances that may be required beforehand.

Prof. J.O. Agure
**DEAN, SCHOOL OF GRADUATE STUDIES**

*Maseno University* *ISO 9001:2008 Certified*

## KIAMBATISHO 5: KIBALI CHA MUERC

**MASENO UNIVERSITY ETHICS REVIEW COMMITTEE**

Tel: +254 057 351 622 Ext: 3050
Fax: +254 057 351 221

Private Bag – 40105, Maseno, Kenya
Email: muerc-secretariate@maseno.ac.ke

**REF:** MSU/DRPI/MUERC/00924/20

**Date:** 18th December, 2020

**TO:** Salano Morris Odari
PG/MA/FA/00037/2017
Department of Kiswahili and Other African Languages
School Arts and Social Sciences
Maseno University
P. O. Box, Private Bag, Maseno, Kenya

Dear Sir,

**RE: Uchanganuzi wa Kimofosemantiki wa Anthroponimu za Wamaragoli**

This is to inform you that **Maseno University Ethics Review Committee (MUERC)** has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is MUERC/00924/20.The approval period is 18th December, 2020 – 17th December, 2021.

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including (informed consents, study instruments, MTA) will be used.
ii. All changes including (amendments, deviations, and violations) are submitted for review and approval by Maseno University Ethics Review Committee (MUERC).
iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to Maseno University Ethics Review Committee (MUERC) within 24 hours of notification.
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affected safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to Maseno University Ethics Review Committee (MUERC) within 24 hours.
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions.
vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal.
vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to Maseno University Ethics Review Committee (MUERC).

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) https://oris.nacosti.go.ke and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely

MASENO UNIVERSITY
APPROVED
10 DEC 2020
ETHICS REVIEW COMMITTEE

Prof. Philip O. Owuor, PhD, FAAS, FKNAS
**Chairman, MUERC**

**MASENO UNIVERSITY IS ISO 9001:2008 CERTIFIED**

## KIAMBATISHO 6: KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 910782

Date of Issue: 06/January/2021

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. MORRIS ODARI SALANO of Maseno University, has been licensed to conduct research in Vihiga on the topic: UCHANGANUZI WA KIMOFOSEMANTIKI WA ANTHROPONIMU ZA WAMARAGOLI for the period ending : 06/January/2022.**

License No: **NACOSTI/P/21/8390**

**910782**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

## KIAMBATISHO 7: NOMINO ZA KAWAIDA ZA KISWAHILI ZINAZOJENGA ANTHROPONIMU ZA KIMARAGOLI ZILIZOCHANGANULIWA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Pesa | Sumuni | Elfu | Benki | Sokoni |
| Madeni | Noti | Shilingi | Senti | Mshipi |
| Taji | Tai | Bangili | Saa | Pete |
| Mavuno | Kichaka | Shamba | Mbegu | Jembe |
| Mwashi | Saisi | Mganga | Mhandisi | Msusi |
| Meneja | Karani | Mnyapara | Fundi | Askari |
| Mkulima | Dereva | Mwalimu | Mtoto | Dada |
| Mwana | Ndugu | Kimulimuli | Babu | Kaka |
| Nzige | Nyuki | Mende | Kiroboto | Nsi |
| Kifaru | Sumu | Uta | Risasi | Bomu |
| Ngao | Bunduki | Asubuhi | Mwaka | Mwezi |
| Saa Kumi | Saa Tisa | Saa Nane | Saa Saba | Saa |
| Saa Sita | Saa Tano | Saa Nne | Saa Tatu | Koti |
| Saa Mbili | Saa Moja | Suruali | Suti | Juba |
| Kitenge | Kilemba | Leso | Sanda | Kikoi |
| Kofia | Shati | Kiatu | Kanzu | Meno |
| Mzungu | Mjerumani | Mwingereza | Moyo | Waya |
| Mtaita | Mswahili | Mwitaliano | Mhindi | Homa |
| Mganda | Magoti | Mbavu | Mgongo | Bati |
| Mabega | Mikono | Kaswende | Chunusi | Soda |
| Nimonia | Kiungulia | Anemia | Kifafa | Meza |
| Mdondo | Kisonono | Maleria | Bakora | Kibago |
| Dirisha | Mlango | Kabati | Kitanda | Namba |
| Kengele | Sayansi | Hisabati | Baraza | Kitabu |
| Masomo | Penseli | Kalamu | Kitambaa | Ubao |
| Fomu | Kamba | Mchanga | Chapi | Randa |
| Cherehani | Ngazi | Nyundo | Mpini | Kokoto |
| Brashi | Rangi | Tupa | Simiti | Panga |
| Gamu | Mbao | Msumari | Tarimbo | Chuma |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Msumeno | Debe | Jiko | Kinu | Uma |
| Mafiga | Kibuyu | Bakuli | Mtungi | Ndoo |
| Kikapu | Birika | Kikombe | Kijiko | Sahani |
| Lori | Trekta | Meli | Baiskeli | Gari |
| Ndege | Nyama | Supu | Chai | Sima |
| Chapati | Andazi | Njugu | Ndimu | Mboga |
| Dalasini | Tangawizi | Masala | | |